# TASWIRA YA JAGINA: ULINGANISHI WA NABII ISA NA SUNDIATA

**NA**

**RUTH NZAMBI JOSEPH C50/89824/2016**

**TASNIFU HII IMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI (M.A) KATIKA CHUO KIKUU CHA NAIROBI.**

## UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijawahi kutolewa kwa mahitaji ya shahada katika chuo kikuu chochote.

RUTH NZAMBI JOSEPH

Sahihi ………………………………….. Tarehe 23/2/2022

NAMBARI YA USAJILI C50/89824/2016

Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi wa kazi hii walioteuliwa na Chuo Kikuu cha Nairobi.

PROF. KINEENE WA MUTISO

Sahihi………………………………………… Tarehe 23/2/22

PROF. RAYYA TIMAMMY

Sahihi……………………………………….. Tarehe 23/2/2022

## TABARUKU

Tasnifu hii nawatabarukia mume wangu mpendwa Simon Kilonzi Mutemi na wanangu Amos Wakili na Sasha Milla ambao walizivumilia changamoto zilizotokana na uamuzi huu wa kujitosa katika masomo ya shahada ya uzamili.

## SHUKRANI

Shukrani zangu kwanza ni kwa mwenyezi Mungu kwa kunijalia siha njema na akili pevu tangu nijitoze kwenye masomo haya na kwa kuniwezesha kutimiza ndoto yangu ya kupata shahada ya uzamili. Shukrani za dhati ni kwa wasimamizi wangu Profesa Kineene Wa Mutiso na Profesa Rayya Timamy kwa mawaidha na kunielekeza ipasavyo katika kuiandika tasnifu hii. Walilibeba jukumu la kuisimamia vyema kazi hii. Wamekuwa na uvumilivu mkubwa tokea hatua ya kuandika pendekezo la utafiti hadi kumalizika kwa kazi hii. Wao walinivumilia sana kwa udhaifu wangu kama mwanafunzi na mafanikio ya kazi hii yametokana pakubwa na juhudi zao za kuisoma kazi yangu, kuikosoa, kuirekebisha, kunielekeza na kunishauri. Hawakuchoka. Sina cha kuwalipa ila tu kuwaombea dua kwa Mwenyezi Mungu. Mungu awape maisha marefu na awazidishie nguvu ili waweze kuwanoa wengine zaidi.

Shukrani zangu aidha ni kwa wahadhiri wangu walioninoa katika kazi hii nao ni: Prof.Iribe Mwangi, Prof. John Habwe, Prof. Mwenda Mbatia , Dkt, Evans Mbuthia, Dkt. Jefwa Mweri, Dkt. Jerono, Dkt. Leo Sanja na wahadhiri wote wa Idara ya Isimu na Lugha za Kiafrika kwa uelekezi wao kabambe walionipa mpaka nikafikia kiwango hiki. Siwezi kamwe kuwasahau wanafunzi wenzangu kwa juhudi na ukarimu wao wa kufaana kwa jua na mvua katika masomo haya. Nawashukuru kwa ushirikiano wao kwa kipindi chote cha masomo ya uzamili. Shukrani za dhati ziwaendee Agnes Mueni Muteti, Jacinta Anuko, Joseph Nyagetiria Musiori, Rehema, Dickens, Jomo, Daniel, Njoroge, Violet miongoni mwa wengine. Mola awazidishie moyo wa kupendana na kusaidiana.

Nashukuru pia aila yangu akiwemo mume wangu mpendwa Simon Kilonzi Mutemi ambaye huienzi elimu na kuikubatia kwa dhati, umenipa mshawasha wa kuyamaliza masomo haya. Umenilipia karo na kunipa msingi wa maisha katika dunia hii. Mungu akukirimie matamu maishani. Watoto wangu Wakili na Sasha, Rabuka awajalie myachote maji ya elimu, myabugie na yawanoe mnoleke. Mpwangu Alex Mutemi, Rabuka amekujalia akili pevu, itumie kuleta mabadiliko chanya katika familia yetu. Namshukuru pia kijakazi wangu Sylvia Ateba, Mungu akujalie mema maishani.

Sitawasahau wazazi wangu marehemu babangu Joseph Mutemi na marehemu mamangu Ngaa. Shukrani za dhati kwa kunizaa na kuniendeleza kielimu hadi kufikia hatua mlioiweza. Shukrani za kipekee kwa mwalimu mwenzangu na rafiki wa karibu Ustadh Said Mohamed mwalimu wa Kiswahili na Dini, shule ya CPS kwa kunifunza mengi kuhusu dini ya kiislamu bila kuchoka. Mungu akukirimie tende, halua, asali, maziwa na matamu yote ya maisha.

# IKISIRI

Katika utafiti huu wetu tumeshughulikia taswira ya jagina kwa kuwarejelea majagina Nabii Isa kama alivyoelezwa katika Utenzi wa Nabii Isa, wake Musa Mzenga (1977), na Sundiata katika Utenzi wa Sundiata ulioandikwa na Djibril Tamsir Niane (1960). Lengo letu kuu katika utafiti huu lilikuwa kulinganisha sifa za kijagina za Nabii Isa na Sundiata kwa nia ya kudhibitisha kuwa sifa za majagina waliosawiriwa katika aina mbili za kazi za kifasihi na waliotoka maeneo tofauti ya kimazingira zinaweza kufanana. Katika sura ya kwanza ni tatizo la utafiti, madhumuni ya utafiti, maswali ya utafiti, sababu za kuchagua mada, upeo na mipaka, msingi wa kinadharia, yalioandikwa kuhusu mada na mbinu za utafiti. Sura ya pili imeshughulikia historia ya Nabii Isa na Sundiata pamoja na historia ya jamii zilizowazaa na kuwakuza. Katika sura ya tatu tumezinganisha sifa za kijagina za Nabii Isa na Sundiata. Sura ya nne tumeshughulikia umuhimu wa Nabii Isa na Sundiata katika jamii zao. Sura ya tano ni hitimisho ambapo tumeangazia matokeo ya utafiti na mapendekezo kuhusu utafiti wa baadaye. Utafiti wetu umeongozwa na nadharia ya vikale tukijikita hasa katika mtazamo wake Northrop Frye.

## ORODHA YA VIFUPISHO VILIVYOTUMIKA

| | |
|---|---|
| B.K | Baada ya Kristo |
| Khj | Kama hapo juu |
| K.K | Kabla ya Kristo |
| Mh | Mhariri |
| Na | Nambari |
| n.k | Na kadhalika |
| N.W | Na wengine |
| taz | Tazama |
| TUKIT | aasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili |
| T.YT | afsiri yetu |
| ub | Ubeti |
| Uk | Ukurasa |

## YALIYOMO

**UNGAMO** ................................................ ii
**TABARUKU** ................................................ iii
**SHUKRANI** ................................................ iv
**IKISIRI** ................................................ vi
**ORODHA YA VIFUPISHO VILIVYOTUMIKA** ................................................ vii
**YALIYOMO** ................................................ viii

**SURA YA KWANZA** ................................................ 1
1.0 Utangulizi ................................................ 1
1.1 Tatizo la Utafiti ................................................ 6
1.2 Malengo na Madhumuni ya Utafiti ................................................ 7
1.3 Maswali ya Utafiti ................................................ 7
1.4 Sababu za Kuchagua Mada ................................................ 7
1.5 Upeo na Mipaka ................................................ 8
1.6. Msingi wa Kinadharia ................................................ 9
  1.6.1 Aina za Vikale ................................................ 11
1.6.2 Mihimili ya Nadharia ya Uhakiki wa Vikale ................................................ 15
1.7 Yaliyoandikwa kuhusu Mada ................................................ 20
1.8 Mbinu za Utafiti ................................................ 24
1.9 Hitimisho ................................................ 26

**SURA YA PILI: MAPISI YA NABII ISA NA SUNDIATA PAMOJA NA HISTORIA YA JAMII ZILIZOWAZAA NA KUWAKUZA.** ................................................ 27
2.0 Utangulizi ................................................ 27
2.1 Historia ya wayahudi ................................................ 27
2.2 Misukosuko ya Kivita Iliyoikumba Jamii ya Wayaudi ................................................ 29
2.3 Historia ya Nabii Isa ................................................ 30
2.5 Historia ya Himaya ya Mali ................................................ 34
2.6 Historia ya Sundiata ................................................ 36
  2.6.1 Kuzaliwa kwa Sundiata ................................................ 37
  2.6.2 Utoto wa Sundiata ................................................ 38

2.6.3 Kifo cha Mfalme Maghan ... 38
2.6.4 Muujiza wa Sundiata Kutembea ... 38
2.7 Hitimisho ... 41

**SURA TA TATU: KULINGANISHA SIFA ZA KIJAGINA ZA NABII ISA NA SUNDIATA** ... 42
3.0 Utangulizi ... 42
3.1 Kuzuka kwa Majagina ... 42
3.1.1 Utabiri wa Kuzaliwa kwa Mashujaa ... 43
3.1.2 Jagina Hutokana Ukoo wa Kifalme au Familia Bora ... 45
3.1.3 Jina la Jagina ... 46
3.1.4 Jagina kwa Kawaida huwa ni Mwanamume ... 47
3.1.5 Utoto na Ujana wa Shujaa. ... 48
3.1.7 Utetezi wa Cheo ... 49
3.1.8 Mahasidi wa Jagina ... 50
3.1.9 Shujaa huwa mwenye Akili Pevu ... 52
3.2 Kugura kwa Shujaa ... 53
3.2.1 Majagina kwa Kawaida huwa ni Washairi ... 54
3.2.2 Maisha ya Shujaa huwa ni Dhiki Tupu ... 55
3.2.3. Maisha na Matendo ya Jagina huwa ni ya Kimiujiza ... 56
3.2.4 Majagina huwa Hawaeleweki kwa Uwazi. ... 57
3.2.5 Mapenzi ya Mama Mzazi kwa Shujaa. ... 57
3.2.6 Kimo na Nguvu za Jagina ... 58
3.2.7 Mashujaa mara nyingi huwa Magwiji Vitani ... 59
3.2.8 Jagina na Suala la Ndoa ... 59
3.2.9 Kifuasi cha Jagina ... 59
3.3 Jagina huwa wa Jamii Nyingi ... 60
3.3.1 Usaliti na Kifo cha Jagina ... 61
3.3.2 Kurudi kwa Jagina katika Safari ya Mwisho ... 62
3.4 Hitimisho ... 63

**SURA YA NNE: UMUHIMU WA NABII ISA NA SUNDIATA KWA JAMII ZAO.** ... 65
4.0 Utangulizi ... 65

4.1.1 Historia ya Jamii/Kioo cha Jamii ..... 65
4.1.2 Kitambulisho cha Jamii ..... 66
4.1.3 Mabadiliko katika Mfumo wa Jamii. ..... 67
4.1.4 Ukombozi na Muungano wa Jamii ..... 68
4.1.5 Fahari ya Jamii ..... 69
4.1.6 Mfano Bora wa Kufuatwa na Jamii ..... 70
4.1.7 Ukuzaji wa Utamaduni wa Jamii ..... 70
4.2 Hitimisho ..... 71

**SURA YA TANO: HITIMISHO NA MAPENDEKEZO ..... 73**
5.0 Utangulizi ..... 73
5.1 Muhtasari ..... 73
5.3 Hitimisho ..... 75
5.3 Mapendekezo ya Utafiti ..... 76

# SURA YA KWANZA

## 1.0 Utangulizi

Kunao wataalamu wengi ambao wameifafanua dhana ya taswira. Kwa mujibu wa Njogu na Chimera (1999), taswira huwa ni picha ambazo hujitokeza katika kazi za kifasihi kutokana na uteuzi na mpangilio wa maneno kiufundi. Wataalamu hawa vilevile wanaeleza taswira kama picha wanazozipata hadhira za kazi za kifasihi. Kulingana nao, taswira hufumba maana kiufundi katika kupitisha ujumbe. Taswira hizi huzindua wanajamii dhidi ya masuala yanayowaathiri maishani mwao. Taswira ni mbinu inayoibua masuala nyeti na muhimu katika jamii kama vile dini, siasa, uchumi miongoni mwa mengine. Kutokana na maelezo ya hawa wataalamu, taswira hutumika katika kujenga picha za matukio na hali tofauti tofauti katika akili za wanajamii. Katika utafiti wetu tumeangazia Utenzi wa Nabii Isa na Utenzi wa Sundiata ili kuona picha au taswira ya majagina hawa.

Jamii nyingi aghalabu huwa na mfumo ambao una asasi nyingi. Asasi hizi zinaingiliana, kutegemeana na hata kukamilishana kwa minajili ya wanajamii kwa jumla. Asasi hizi husaidia katika kuyakidhi mahitaji ya wanajamii katika kipindi fulani. Asasi katika jamii ni kama vile sheria, elimu, uchumi, ndoa, afya miongoni mwa nyingine. Ujagina ni mojawapo ya asasi katika jamii. Majagina walikuwepo tangu wakati wa mababu na mababu zetu. Kila jamii huwaenzi majagina wake na mara nyingi huonekana kama zawadi kutoka kwa Mungu. Wanajamii huamini kuwa jagina hutumwa kwao na Mungu katika wakati na kipindi fulani kwa malengo mahususi. Ingawa majagina wote si mitume, aghalabu jamii nyingi huamini majagina wengi huwa mitume waliotumwa kuzitatua shida na taabu za wanajamii.

Kunao majagina wa kidini na wale wa kihistoria. Majagina wa kidini ni kama vile Mtume Muhammad, jagina wa waislamu, Yesu Kristo, jagina wa Wakristo. Majagina wa kihistoria ni kama vile Fumo Liyongo wa Waswahili, Shaka Zulu, jagina wa Wazulu, miongoni mwa wengine. Kunao majagina ambao wanakuwa wahusika wakuu katika kazi za kifasihi kama vile Mfalme Edipode kama alivyosawiriwa katika tafsiri ya tamthlia ya Mfalme Edipode (1971) iliyoandikwa na Sophocles na kutafsiriwa S. Mushi kwa Kiswahili.

Ujagina wa majagina katika jamii hupitishwa kutoka kizazi hadi kizazi kwa njia ya kutungiwa tenzi, ngano, au nyimbo. Kwa mfano, utenzi wa Nabii Isa ni utenzi unaohusu maisha ya Nabii Isa na mafunzo yake kwa wanajamii wake. Usawiri wa majagina ulimwenguni unaweza kupatikana katika hadithi na nyimbo ambazo huwasawiri majagina kwa njia ambayo ni ya kipekee. Katika kazi zilizofanywa na watafiti wengi kuwahusu majagina zimezoa sifa za majagina ambazo ni bia. Sifa za majagina wengi hulandana na kukaribiana.

Sifa hizi bia ni kama vile kutabiriwa kwa kuzaliwa kwa jagina kama vile kutabiriwa kwa kuzaliwa kwa Yesu Kristo, misukosuko ya kijamii kabla ya kuzaliwa kwa jagina, kuwepo kwa mgogoro mkubwa katika maisha ya shujaa, kusalitiwa kwa jagina na mtu wa karibu sana naye, kifo cha ghafla cha jagina, kuwaletea wanajamii mabadiliko katika jamii yake, miongoni mwa sifa nyinginezo. Hivyo basi, ni kwa misingi hii ambayo tumeitumia kuwalinganisha majagina wawili; Nabii Isa na Sundiata. Katika utafiti wetu tumejikita katika kazi hizi mbili kama kazi za kifasihi. Katika kazi yetu hatujajishughulisha na masuala ya kidini bali tumewaangalia Nabii Isa na Sundiata kama wahusika tu wa kazi za kifasihi. Hatuna nia ya kudunisha wala kuikuza dini yoyote.

Utangulizi wa Utenzi wa Nabii Isa uliandikwa na Abdalla Abdilattif ambaye anasema kuwa Mzenga, jina lake la kishairi ni "Ustadh Shirazi" na amebobea katika utunzi wa mashairi. Abdalla anasema kwamba, Musa Mzenga ni mzaliwa wa jamii ya uswahilini ambayo ilimsaidia sana katika kumtia ari na kumuongezea ujuzi wa kutunga mashairi. Abdalla anaeleza kuwa utenzi wa Nabii Isa, ni utenzi unaoelezea kisa cha Nabii Isa kuanzia ukoo wa mamaye, kuzaliwa kwake kimiujiza, unabii wake na kupaa kwake mbinguni. Kwa ufupi, ni utenzi unaoelezea historia ya Nabii Isa. Utenzi huu wa Nabii Isa ndicho kitabu cha kwanza cha Musa Mzenga kuchapishwa.

Utenzi wa Sundiata ni kisa cha kale kuhusu jagina Sundiata. Kunao waandishi wengi ambao wamesimulia kisa cha Mfalme Sundiata. Hata hivyo, utafiti huu utajikita katika Utenzi wa Sundiata uliyoandikwa na D.T. Niane (1960). Djibril Tamsir Niane ni mzaliwa wa nchi ya Guinea mwaka wa 1932. Ni mwandishi na mwanahistoria wa kiafrika. Riwaya ya Sundiata ni kisa cha kale cha nchi ya Mali. Ni masimulizi ya maisha na nyakati za mwanzilishi wa ufalme wa Mali katika miaka ya karne ya kumi na tatu.

Kunao wataalamu wengi ambao wamefafanua dhana ya utenzi. Gibbe (1980) akimnukuu Shabaan Robert anaeleza utenzi kama sanaa ya vina inayopambanuliwa kimukhutasari au kwa maneno machache. Abedi (1954:1) anaeleza utenzi kama wimbo na iwapo shairi halitaimbika basi si shairi. Kutokana na maelezo ya hawa wataalamu, tumeutazama utenzi kama sanaa iliyoandikwa au kuimbwa, yenye mpangilio maalumu wa vina, ambayo huandikwa kwa mukhutasari na kwa lugha yenye mvuto kwa madhumuni ya kufunza, kutumbuiza na kueleza juu ya mwanadamu na mazingira yake. Onchwati (2016), anapowanukuu wataalamu wengineo kama vile Mulokozi (1996) na Wamitila (2003), anaeleza utenzi kama hadithi au kisa kinachoelezea historia ya mtu wa kawaida au shujaa anayeaminika kuwa aliwahi kuishi. Hivyo basi, utenzi unaweza kuelezea historia za mashujaa kwa mapana na marefu. Utafiti wetu umejikita katika kisa cha shujaa wa kihistoria na wa kidini na kingine cha shujaa wa kihistoria. Tumerejelea taswira ya jagina tukiurejelea Utenzi wa Nabii Isa ulioandikwa na Mzenga (1977) na Utenzi wa Sundiata ulioandikwa na Niane (1960).

Kunao wataalamu ambao wameieleza dhana ya ujagina. Mutiso (1999:1) anamweleza jagina kiutatu kwa vile anaeleza aina tatu za majagina. Kwanza, jagina ni kiumbe ambaye ni wa ukweli, aliyekuzwa na jamii na pia kujikuza mwenyewe. Kiumbe huyu husifiwa na wanajamii kwa sababu ya ujasiri wake. Wanajamii huamini hata kama ana ulemavu wowote, ulemavu ule huchukuliwa kuwa onyo ambapo kiumbe huyu atakuwa na nguvu za kiajabu baadaye. Kiumbe huyu huaminika kuleta mambo yote mazuri katika jamii hata kama hakuhusika kamwe. Jagina huyu kwa kawaida hutokana na familia au jamii maskini lakini wanajamii huamini yeye ametokana na familia ya kifalme ambayo ni tajiri. Jagina huyu huaminika kuzitatua shida za jamii yake na hivyo maisha yake hukumbwa na dhiki na taabu katika kuyatimiza majukumu haya. Jamii huamini kiumbe huyu hata akifa huwa anayaona yote yatendekayo katika jamii yake na hivyo kuabudiwa baada ya kifo chake.

Mutiso anaieleza aina ya pili ya jagina kuwa kiumbe wa kihurafa ambaye jamii humchukulia kuwa Mungu au mtoto wake au humchukulia kuwa yote mawili. Jamii huamini kuwa kiumbe huyu ndiye mzazi wa jamii. Aina ya tatu ni mhusika mkuu katika kazi za kifasihi kama vile katika tenzi, riwaya, tamthiliya, ngano, hadithi miongoni mwa kazi zingine. Hata hivyo, mpaka kati ya aina

alizozitaja Mutiso ni finyu mno kwani mhusika mkuu katika kazi yoyote ile anaweza kuwa na sifa za aina nyingine mbili za majagina. Hivyo basi, jagina ni kiumbe ambaye ni wa kweli, aliyekuzwa na wanajamii na pia kujikuza mwenyewe kufikia kiwango cha mwonekano wa kiumbe ambaye ni wa ajabu. Kiumbe huyu huwa ni jasiri, anasifika na kuwa mashuhuri. Gichamba (2005:1), anadai kuwa jagina ni mwanajamii mwenye tabia za kipekee na ambazo huwastaajabisha wanajamii. Sifa hizi za kipekee humwezesha kuwepo kama mtetezi na mwokozi wa jamii husika. Maelezo haya ya Gichamba, yametuwezesha kumweleza shujaa kama mwanajamii mwenye sifa za kipekee.

Sifa hizi za kipekee humpa jagina huyu upekee unaompa sifa za kiumbe ambaye sio wa kawaida. Maelezo ya wataalamu hawa, yametuwezesha kumweleza jagina kama kiumbe mwenye sifa za kipekee zenye uhalisi ajabu mwingi. Mara nyingi hukuzwa na jamii na pia hujikuza mwenyewe na kujikuza huku huwa na uwezekano wa kupigiwa chuku. Aidha jagina huzuka katika kipindi fulani kwa madhumuni ya kuwatatulia wanajamii shida na dhiki zinazowakumba. Sifa za majagina hupitishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine kwa kutungiwa kama vile utenzi, kutungiwa nyimbo, kupitia kwa hadithi miongoni mwa njia nyingine.

Kunazo kazi nyingi kuwahusu majagina wengi duniani. Kutokana na tafiti zilizofanywa kuwahusu majagina, majagina takriban wote wana sifa ambazo zina ukaribu mwingi ulioshabihiana. Majagina wengi huzaliwa kimiujiza kama Yesu Kristo, huifanya miujiza mingi, hukabiliwa na migogoro mingi na mikubwa katika maisha yao, husalitiwa na jamaa au wandani wao, hufa au huangamizwa na wasio na uwezo mkubwa kama wao miongoni mwa sifa nyingine. Katika utafiti huu tumewalinganisha majagina Isa na Sundiata kwa mujibu wa sifa tulizozitaja hapo juu kama walivyosawiriwa na Musa Mzenga na D.T. Niane.

Utenzi wa Nabii Isa ni utenzi wa kihistoria na kidini ambao unasimulia kisa chenye mnato wa kiuhalisia ajabu. Kisa hiki kinahusu shujaa kwa jina Nabii Isa aliyezaliwa na Mariyamu bintiye Imrani ambaye mara nyingi alikuwa akiabudu msikitini na ninaye. Maryam alichukuliwa na mtume Zakaria ambaye alimlea kwa kumfunza mambo ya dini msikitini. Maryam alitabiriwa kuzaliwa kwa Nabii Isa na malaika Jibrili aliyemvivia nguo na hivyo basi akapata mimba pasi kukutana na mwanamume kimwili. Nabii Isa anazaliwa na kisha kuzungumza wakati huo huo. Kuzungumza huku kulimwondolea lawama mamaye kuwa mimba yake haikuwa ya kawaida.

Nabii Isa alitumwa na Mwenyezi Mungu kuja ulimwenguni kuyatia nguvu mafundisho ya Nabii Musa kuyahusu Torati. Nabii Isa alipofikisha umri wa miaka thelathini, alichukua hatamu ya kuwaongoza wana wa Israeli kama alivyofanya Musa. Wana wa Israeli walikuwa wamepotoka kutoka mienendo aliyowaonyesha Musa hata wakaanza kuabudu masanamu. Uongozi wa Nabii Isa ulikuwa thabiti kwani aliwaongoza kwa mapenzi na upole. Aliwapenda wengine kama alivyojipenda mwenyewe. Alitembea kwote na kuhubiri injili kwa kuwaonyesha heri.

Nabii Isa alihubiri huku akitenda miujiza mingi. Kwa mfano, alimweleza mmoja aliyekuwa miongoni mwa hadhira yake chakula ambacho alikuwa amekila na fedha alizokuwa nazo mfukoni na hata akiba aliyokuwa nayo nyumbani; aliwaunda ndege kwa udongo na wakawa hai na kupaa angani, miongoni mwa miujiza mingine. Ingawa Nabii Isa aliifanya miujiza mingi na kuwashangaza wengi, kunao waliomchukia na kutofautiana naye akawa na maadui miongoni mwa jamii yake. Maadui hao walimsingizia maovu ambayo yalimfanya ahukumiwe kusulubiwa. Baadaye aliokolewa pale Mungu alipomleta mtu mwingine aliyefanana naye akasulubiwa.

Utenzi wa Sundiata kwa upande ule mwingine unahusu jagina Sundiata ulioandikwa na Niane. Babaye Sundiata alikuwa mfalme wa ufalme wa Mandinka katika nchi ya Mali bara la Afrika. Kuzaliwa kwa Sundiata kulitabiriwa na nabii aliyemtabiria mfalme Konate babaye Sundiata. Mfalme Konate alitabiriwa kuwa atamwoa mwanamke mwenye sura mbaya ambaye atamzalia mtoto wa kiume atakayemrithi kama mfalme wa ufalme wa Mandinka.

Mfalme Konate baadaye alimwoa Sogolon mwanamke aliyekuwa na sura mbaya aliyeletwa kwake na wawindaji wawili kama ilivyokuwa imetabiriwa. Siku ya Sundiata kuzaliwa, hali ya anga ilibadilika ghafla kutoka hali ya kiangazi iliyokuwepo na kuwa ya mvua. Ngurumo na radi zilisikika kumkaribisha shujaa duniani. Alipozaliwa, hali ya kawaida ya kiangazi ilichukua usukani. Sundiata alipozaliwa aliitwa 'jagina wa majina mengi' kwani alikuwa na majina mengi ya kimajazi. Kimaumbile, alikuwa kiumbe tofauti na watoto wengine kwani alikuwa na kichwa kikubwa na macho makubwa.

Sundiata alizaliwa akiwa mlemavu. Ingawa alikuwa na ulemavu, mfalme Konate aliiambia jamii yake kuwa Sundiata ndiye atakayeurithi ufalme wake na kwamba atakuwa mfalme mkuu. Vilevile alimpa kiongozi ambaye alikuwa mzee mwenye hekima na mtambaji. Wazee hawa wenye hekima

waliitwa Groit. Iliaminika kuwa ni viongozi pekee waliokuwa na wazee kama hawa wa kibinafsi. Sundiata hakuweza kutembea hadi alipofikisha umri wa miaka mitatu.

Baada ya kifo cha mfalme Konate, mkemwenza wa Sogolon alimrithisha mwanawe ufalme wa Mandinka na kumnyima Sundiata nafasi ile. Sundiata na mamaye Sogolon waliandamwa na mfalme mpya hadi wakagura kutoka nchi yao na kukimbilia usalama nchi nyingine. Ufalme wa Mandinka unakumbwa na matatizo mengi hadi wanajamii wanamsaka Sundiata arudi. Sundiata anarejea Mandinka na kuwatatulia shida na dhiki zao.

**1.1 Tatizo la Utafiti**

Jamii huwa na jagina au hata majagina wake ambao wana sifa za kipekee zinazowatambulisha. Kunao wataalamu wengi ambao wameliangazia swala la mashujaa na kuzichanbua sifa ambazo ni bia za mashujaa. Wataalamu hawa ni pamoja na: Kunene (1972), Butler (1979), Mutiso (1985), Gichamba (2005), Achieng (2012) miongoni mwa wengine. Kulingana na Mutiso (1985), wengi wa watafiti wa suala la majagina wameangazia tu mashujaa kwa jumla. Mengi yameandikwa na kuangaziwa na watalaamu na waandishi wengi kuhusu ujagina katika jamii.

Kunao ulinganisho wa jagina wa kidini na wa kidini, ulinganisho wa jagina wa kihistoria na wa kihistoria. Kunao ulinganisho wa jagina wa kidini na wa kihistoria kwa mfano, Gathara (2015) amewalinganisha jagina wa kihistoria Fumo Liyongo na jagina wa kidini Nabii Isa. Utafiti huu umechunguza taswira ya jagina kwa kuvirejelea vitabu viwili; Utenzi wa Nabii Isa (1977) ulioandikwa na Musa Mzenga na Utenzi wa Sundiata (1960) ulioandikwa na Niane. Tumewalinganisha Nabii Isa na Sundiata ambao ni majagina wa kihistoria kwa mujibu wa sifa bia za mashujaa. Kunao waandishi waliowaangazia mashujaa wa kihistoria na wa kidini kama vile Mberia (1989) alimwangalia Fumo Liyongo naye Mutiso (1985) alimwaangazia Mtume Muhammad na kutoa sifa ambazo ni bia na zinazodhihirika kwa mashujaa wengi ulimwenguni.

Sifa hizi walizozitoa watafiti wengi si za pekee na iwapo mashujaa wengine wangelinganishwa, tunaweza kupata sifa zaidi za majagina. Tunaamini kwamba, ulinganishi wa majagina wawili kutoka mazingira mawili tofauti, utashadidia tafiti tangulizi kuwa majagina huwa na sifa

zilizokaribiana na kushabihiana. Ulinganishi wa Nabii Isa na Sundiata haujafanywa hapo mbeleni na hivyo utafiti wa namna hii umechangia katika kuthibitisha mfanano uliopo wa majagina ulimwenguni kote na pia umedhihirisha umuhimu wa majagina hawa katika jamii zao na hata katika jamii pana na huu ndio msingi wetu wa utafiti.

### 1.2 Malengo na Madhumuni ya Utafiti

Utafiti una malengo yafuatayo:

1. Kubaini mapisi na mazingira ya kijamii yaliyowazaa Nabii Isa na Sundiata.
2. Kubaini sifa zinazoweza kujitokeza kwa kuwatofautisha na kuwafananisha majagina Isa na Sundiata.
3. Kutathmini umuhimu wa majagina Isa na Sundiata kwa jamii zao na ulimwengu wote kwa jumla.

### 1.3 Maswali ya Utafiti

Maswali yatakayouongoza utafiti wetu ni yafuatayo:

1. Ni mazingira yepi ya kijamii yaliowazaa majagina Isa na Sundiata?
2. Ni sifa zipi huwatofautisha na kuwafananisha majagina Isa na Sundiata?
3. Je jagina Isa na Sundiata wana umuhimu gani katika jamii zao na ulimwengu wote kwa jumla?

### 1.4 Sababu za Kuchagua Mada

Mada hii tumeichagua baada ya kutalii na kuyaangalia mengi yaliyoandikwa kuhusu majagina. Kunayo makundi matatu yaliyoainisha majagina. Kwanza, kunao majagina ambao ni wa kidini kama vile jagina mtume Muhamadi katika Utenzi wa Ukawafi wa Miraji. Utenzi huu ambao umejikita katika dini ya kiislamu unamzungumzia mtume Muhamadi (S.A.W) na safari yake ya usiku mmoja kwenda mbingu ya saba. Kundi la pili ni la mashujaa wa kihistoria kama vile shujaa Fumo Liyongo katika Utenzi wa Fumo Liyongo. Katika utenzi huu Fumo Liyongo ambaye alikuwa jagina wa jamii ya Waswahili, alizuka wakati ambako kulikuwepo na misukosuko mingi katika upwa wa Afrika Mashariki. Kundi la tatu nalo ni la mashujaa wa kubuni. Shujaa wa kubuni huwa mhusika mkuu ambaye hupewa sifa zinazozipiku sifa za kawaida za binadamu. Mfano wa shujaa wa kubuni ni kama vile Tajiri katika Utenzi wa Masahibu. Katika utafiti wetu, tumewalinganisha Nabii Isa na Sundiata ambao ni majagina wa kihistoria.

Kazi nyingi tulizozisoma zimewalinganisha majagina wa aina moja au hata aina mbili. Kwa mfano wa kidini na wa kidini, wa kistoria na wa kihistoria au wa kidini na wa kihistoria. Kunazo kazi zilizowalinganisha majagina wa kidini na wa kihistoria lakini hakuna utafiti wa kina kulingana na ufahamu wetu tulioupata uliotafiti kuhusu ulinganisho wa majagina Nabii Isa na Sundiata kwa kuongozwa na nadharia ya vikale, mtazamo wake Northrop Frye. Utafiti huu wetu hivyo ulinuia kuliziba pengo hili.

Vilevile, suala la ujagina lilituvutia sana tulipofanya utafiti kuhusu majagina wa jamii ya Wakamba ili kutimiza mahitaji ya darasani katika somo la tenzi za kale. Ulinganisho wa mashujaa Nabii Isa na Sundiata unaweza kutuzolea sifa zaidi za majagina.

## 1.5 Upeo na Mipaka

Mada ya ujagina ni pana kukifanyia kila kipengele utafiti. Utafiti huu unanuia kuangazia masuala maalum; kuchunguza sifa za kishujaa za Nabii Isa na Sundiata kwa mujibu wa sifa bia za mashujaa. Utafiti umejikita katika vitabu hivi viwili, Utenzi wa Nabii Isa ulioandikwa na Mzenga (1977) na kuhaririwa na Abdilatif Abdala, na Utenzi wa Sundiata (1960) ulioandikwa na Niane. Visa kwenye vitabu hivi vimewasawiri wahusika wawili; Nabii Isa ambaye ni jagina wa kidini na kihistoria na Sundiata ambaye ni jagina wa kihistoria. Utafiti umezilinganisha na kuzitofautisha sifa za majagina hawa na kutathmini umuhimu wao kwa jamii zao na ulimwengu wote kwa jumla.

Ingawa utafiti wetu ulijikita katika vitabu viwili tulivyovitaja hapo juu; Utenzi wa Nabii Isa na Utenzi wa Sundiata, kuna vitabu vingine ambavyo tulivitalii na kuvirejelea kama vile Kurani, vitabu vya hadithi za Isa, nyimbo za kidini, hadithi za Sundiata miongoni mwa vingine ili tuweze kupata taswira kamili ya majagina hawa na umuhimu wao katika jamii zao na ulimwengu wote kwa jumla. Hatukujiingiza katika mijadala ya mambo ya kidini bali tumejikita katika vitabu hivi viwili kama kazi tu za kifasihi. Nabii Isa na Sundiata tumewachukulia tu kama wahusika wakuu katika kazi hizi mbili. Katika utafiti wetu, kwa kifupi tumeangalia dhana ya usawiri na mbinu za usawiri walizozitumia waandishi hawa katika kuwasawiri wahusika hawa. Hatujawaangazia wahusika wengine katika kazi hizi ingawa wapo. Vilevile, tumezichanganua sifa za ushujaa kwa

kurejelea matukio ya ujagina katika kazi hizi mbili. Tumeyaangazia pia mazingira yaliyowazaa majagina hawa kwa vile jagina hawezi kuzuka tu katika ombwe tupu.

### 1.6. Msingi wa Kinadharia

Utafiti huu umeongozwa na nadharia ya uhakiki wa vikale. Nadharia ya vikale ndiyo tuliyoitumia kuzilinganisha sifa za mashujaa Nabii Isa na Sundiata kwa mujibu wa sifa bia za majagina. Pia, nadharia hii vilevile imetumiwa katika kuelezea umuhimu wa majagina hawa katika jamii zao. Kulingana na maelezo ya Sengo (2009) , nadharia huwa wazo kuu, mwongozo mkuu au fikra kuu ya mwanajamii au jamii. Wamitila (2002) anasema ya kwamba nadharia ni sayansi inayohusika na sheria za kijumla ambazo hutumiwa kuchunguza swala fulani.

Njogu na Wafula (2007) wanaeleza vikale kama taswira za picha ambazo ni kongwe na hutokea katika kazi nyingi za kifasihi. Wanaeleza vikale hivi kama utamaduni wa jamii, wahusika, maudhui, miundo ya usimulizi, dini, mavazi miongoni mwa vingine. Jung na mwenzake (1972) wanaeleza vikale kama picha kongwe ambazo aghalabu hujitokeza katika mwingiliano wa mwanadamu na mazingira yake. Njogu na Wafula (khj) wanaeleza vikale kama picha ambazo ni kongwe na hurudiwarudiwa katika kazi za kifasihi. Vikale katika kazi za kifasihi ni kama vile wahusika, Mungu au shetani, maudhui, miongoni mwa vingine. Wahusika huwa wa aina nyingi kama vile nguli ambaye aghalabu huwa shujaa, huwa kuna mkinzani wa nguli ambaye hujifunga kibwebwe kuiangamiza mipango yote ya nguli na hata wakati mwingine kumwangamiza. Kuna wahusika wengine kama vile wasaidizi, wazee wa hekima, wapenzi miongoni mwa wengine. Mungu ni kikale ambacho huonyesha wema ilhali shetani ni kikale ambacho huashiria uovu.

Kulingana na Gathara (2012), kunayo mitazamo miwili mikuu ya nadharia ya vikale. Mtazamo wa kwanza ni wake Gustav Jung ambaye alikuwa mwanafunzi wake Sigmund Freud ambaye alikuwa mwaasisi wa taaluma iliyohusu uchanganuzi nafsia. Kunaye mgonjwa ambaye walikuwa wakimchunguza kuhusu matukio yaliyokuwa yanampitia akilini mwake. Gustav Jung na Sigmund Freud walitofautiana kuhusu ufasiri wa matukio wa yule mgonjwa na kuchukua misimamo tofauti pale Sigmund Freud alisisitiza kuhusu akililaza nafsia huku Jung akisisitiza kuhusu akililaza jumuishi. Wataalamu hawa wawili walitengana na Gustav Jung akaiendeleza kazi yake ya

kuzichunguza ndoto na kuzifasiri. Alizichunguza ndoto kwa muda mrefu na kuzifasiri pale alipoibua dhana ya vikale.

Kulingana na Jung, vikale ni picha ambazo ni kongwe na zinazojitokeza aghalabu mara kwa mara katika kazi yoyote ya fasihi. Aliendelea kueleza kuwa vikale hivi ni taswira zinazorudiwarudiwa na hutokana na tajriba ya mwanajamii katika maisha ya tangu wakati wa mababu zetu na zinaporithiwa huwekwa kwenye akililaza jumuishi na hurithika kama ndoto, mawazo ya mwanajamii, visasili na katika vipengele vyote vya maisha ya binadamu. Mawazo haya ya Jung' yanatuelekeza kuwa vikale ni picha kongwe ambazo hujitokeza katika mtagusano wa mwanadamu na mazingira yake na huwa akilini mwa mwanadamu

Mtazamo wa pili wa nadharia hii ya uhakiki wa vikale unadai kuwa James Frazer ndiye mwaasisi. Hili ni kutokana na vikale vilivyodhihirika katika kazi yake ya The Golden Bough. Kazi hii ya Frazer ilichapishwa katika chuo kikuu cha Cambridge na idara ya Athropolojia linganishi. Katika kazi hii ya The Golden Bough, mtaalamu Frazer aliangazia ruwaza zilizoonekana kujirudiarudia katika visasili vyote alivyoviangazia ambavyo vilikuwa vimetoka katika tamaduni anuai. Haya ni kulingana na Abraham (1971). Katika nadharia ya vikale, kunayo mitazamo miwili mikuu; mtazamo wa kwanza ni wake Gustav Jung ambaye alikuwa mwanafunzi wake Sigmund Freud ambaye alikuwa mwaasisi wa taaluma iliyohusu uchanganuzi nafsia. Kunaye mgonjwa wa kiakili waliokuwa wanamchunguza kuhusu matukio yaliyokuwa yakimpitia akilini mwake. Gustav Jung na Sigmund Freud walipotofautiana kuhusu ufasiri wa yule mgonjwa na kuchukua misimamo tofauti pale Sigmund aliposisitiza kuhusu akililaza nafsia huku Jung akisisitiza akililaza jumuishi. Jung na Sigmund walitengana na Jung akaiendeleza kazi yake ya kuzichunguza ndoto na kuzifasiri. Alizichunguza ndoto kwa muda mrefu na kuzifasiri pale alipoibua dhana ya vikale.

Tanzu za vikale vilevile huhusishwa na wataalamu Frye (1990) ambaye anaeleza kuwa aina za fasihi hutokea katika utungo mmoja na kwa hili, anaibua dhana ya monomithi. Frye ni mtaalamu aliyechangia kuiwekea mihimili nadharia hii ya uhakiki wa vikale kupitia kwa kazi yake Anatomy of Criticism. Frye alidhihirisha vile vikale vinavyohusu kuzaliwa, upanzi wa mime ana majira mbalimbali kama vile kipupwe na kiangazi vinavyoathiri fasihi. Kulingana na Frye, kuna aina tatu za vikale navyo ni: motifu, taswira na tanzu za fasihi. Motifu za vikale ni kama vile uumbaji wa

ulimwengu, ukombozi na mageuzi, kifo na jagina. Taswira za vikale hujumuisha wahusika, mandhari, maumbo, rangi, maji, jua miongoni mwa nyingine. Hata hivyo, katika utafiti wetu tumeangazia taswira ya wahusika. Tanzu za fasihi nazo ni kama vile majira kwa mfano ya vuli, masika, ulimbwende na kadhalika.

### 1.6.1 Aina za Vikale

Kutokana na maelezo ya Jung (1969), kunazo aina za vikale ambavyo ni vya kiethrografia au kianthropomofia. Kunacho kikale cha Nafsi. Hiki ni kikale ambacho ni cha kiethrografia na huashiria mwingiliano na muungano wa akili tambuzi na akili laza. Jung anasema kuwa, nafsi ndiyo humpa binadamu kujitambulisha na pia kumwezesha kuijenga tabia yake. Hivyo basi, nafsi ni kiwakilishi cha akili katika ukamilifu wake na huhusisha sehemu za ung'amuzi zote. Nafsi ni kikale kinachowakilisha maana ya jagina kwa sababu jamii hutumia jagina katika kuhifadhi tabia za jamii.

Vilevile, kuna kikale cha kivuli. Kivuli ni mojawapo ya sehemu za akili laza ya binadamu na aghalabu sehemu hii huudhi. Kivuli kinaweza kuwa nafsi. Kumbukumbu zinaweza kutolewa kutoka akili tambuzi na kuwasilishwa katika akili laza. Sehemu hii ya akili laza haina matumizi ya urazini kama vile akili tambuzi. Ingawa sehemu hii ya akili laza (kivuli) hujichora kama sehemu iliyojaa maovu na isiyo na huruma na yenye kulipiza kisasi; ni sehemu yenye hisia za huruma. Umuhimu wa kivuli ni kule kung'amua na kuzielewa tabia, mitazamo ya wanajamii na vile wanavyoyachukulia maswala yatokayo katika ulimwengu wa nje. Kivuli hivyo basi hutoa taarifa kuhusu maswala yanayoisumbua tabia ya binadamu na uozo wa jamii.

Kivuli aghalabu hujitokeza katika njozi kama viumbe au mazimwi ya kuogofya. Vilevile, kivuli hujitokeza kama mwandani au adui. Taarifa ya kina kuhusu kutokea kwa kivuli katika ndoto na maana ya kivuli vilevile, hutegemea uzoevu wa kila binadamu. Hii ni kwa sababu kivuli huibuka katika akili ya mtu wala si katika akili laza jumuishi. Kunacho kikale cha Anima ambacho ni cha kianthropomofia cha akili laza. Anima hurejelea sehemu ya kike katika mwanamume au katika akili laza rejelewa.

Hivyo basi, kikale cha Anima hujumuisha sifa za kike zinazopatikana kwa mwanamume. Anima hudhibiti uhusiano wa mwanamume na mwanamke. Kwa mfano, ni cha mwanamume katika akili yake cha kukutana na kutangamana na mwanamke. Kikale cha Animasi nacho kinarejelea sehemu ya kiume iliyomo ndani ya mwanamke katika akili laza. Kikale hiki hujumuisha sifa za kiume zinazojitokeza katika mwanamke. Jung anaeleza kuwa vikale vya Anima na Animasi ni sehemu zilizo changamano na hukamilishana.

Aidha, kuna kikale cha shujaa. Nietzsche N.W 1961:49-111), wanaeleza kuwa kunazo hatua tatu anazozipitia shujaa ili kufikia kiwango cha kuitwa shujaa. Kwanza, jagina huwa na mshawasha wa kukiuka na kuharibu kawaida za jamii za wakati huo ambazo aghalabu huwa za kidhanishi. Pili, jagina huvunja na kutupilia mbali kawaida za zamani kwa kuibua kanuni zake za kimaadili. Tatu, jagina humaliza kukataa dini kwa jamii ambako huwa na hatua tatu: mkosa maadili, mawazo huru na jagina.

Vilevile, kunacho kikale cha ajuza mwenye busara. Kikale hiki ni kiwakilishi cha maadili katika jamii. Pia, kuna kikale cha Ayari ambacho huwakilisha jagina ambaye ni roho njema ipingayo kanuni zisizowasaidia wanajamii. Ayari hupinga na kuzivunja kanuni hizi kwa kutumia ujanja. Uungu pia ni kikale ambacho hurejelea mungu ambaye huabudiwa na wanajamii. Mungu huyu hujitokeza kama mnyama, mtu, mlima au hata mti. Miungu huwa hawafi. Wanajamii huwachukulia kama viumbe wenye busara na akili nyingi kiasi cha kuwapiku wanajamii wanaowaabudu.

Kutokana na maelezo kuhusu maana ya vikale na aina za vikale, tumeona kuwa ujagina ni mojawapo wa vikale. Hivyo basi, tunanuia kuziangazia sifa za kipekee walizo nazo jagina Nabii Isa na jagina Sundiata kulingana na Musa Mzenga na Niane na kuzilinganisha kwa mujibu wa sifa bia za mashujaa na kutathmini umuhimu wao katika jamii zao huku tukiongozwa na nadharia ya uhakiki wa vikale. Abrahams na Harpham (1981), wanaeleza ya kwamba nadharia ya vikale katika uhakiki wa fasihi hutumiwa kuchanganua taswira na wahusika wanaorudiwarudiwa na ambao wamefanana katika tungo kadha za kifasihi, hasa katika visasili. Kufanana kwa vikale vingi katika kazi za kifasihi huleta dhana ya ulinganifu fulani wa ruwaza za kijadi.

Mutiso (1999), anaeleza kuwa nadharia ya vikale huhusisha uhakiki wa ruwaza bia za kimsingi ambazo mara nyingi hudhihirika katika jamii pana ya ulimwengu. Mutiso anasema kuwa vikale vikitumiwa vizuri katika kazi zozote za kifasihi huwa na mvuto mno. Maelezo ya wataalamu hawa yanadhihirisha kuwa nadharia ya vikale kimsingi hurejelea ruwaza za kimsingi katika jamii.

Uhakiki wa nadharia ya vikale huzingatia ruwaza za kimsingi katika visasili na pia kitambiko, ambazo aghalabu hujirudiarudia katika visakale na taratibu nyingi katika jamii. Haya ni kutokana na maelezo yake Carl Jung kuhusiana na akili laza (Abrahams 1999:12-14). Mtaalamu Jung alitumia istilahi ya vikale katika taswira asili za kumbukumbu ambazo mara nyingi hurudiwarudiwa na ambazo hutokana na tajriba katika maisha ambayo ni ya tangu wakati wa mababu zetu na ambazo hutumiwa kama utaratibu wa kuangazia tatizo la sifa ambazo ni bia. Jung anasema kwamba, taswira hizi za kale hurithiwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine na hutiwa katika akili laza jumuishi ya wanajamii na hupatikana katika ndoto, visasili na katika vipengele takriban vyote katika kazi za kifasihi na katika maisha ya binadamu popote alipo duniani.

Katika uhakiki wa vikale, vikale hutumiwa katika taswira zenye mfanano katika tungo za kifasihi na vipengele anuai katika jamii. Nadharia hii ya uhakiki wa vikale hueleza kuwa binadamu wote ni sawa, popote walipo ulimwenguni. Tofauti kati yao ni finyu mno na ni za kufikirika na aghalabu husababishwa na tofauti ndogo za kimazingira na kihistoria.

Mtaalamu Jung (1990), anaeleza kuwa afya njema na busara hudhihirika pale ambapo binadamu wanaelewana vyema na ishara bia katika akili laza jumuishi. Jung anasema kuwa akili ya binadamu ina sehemu mbili. Kunayo sehemu ya pili iliyoko chini ya sehemu ya kwanza ambayo anaiita akili laza ambapo ndipo panapohifadhiwa vikale vyote. Jung anaeleza kuwa yanayopatikana katika vikale hivi huashiria mchakato mzima wa akili laza jumuishi.

Nadharia hii ya uhakiki wa vikale iliibuka pale ambapo matumizi ya dhana zinazojitokeza katika elimu ya visasili na ile ya uchanganuzi wa tungo nyingi za kifasihi ilipochipuka. Uhakiki wa vikale hutumika kuhakiki jinsi ruwaza zinazojirudiarudia kama vile utamaduni, imani, taswira na mila huathiri kazi za kifasihi. Kulingana na uhakiki wa vikale, ishara fulani huwakilisha maana ileile, wakati na mahali popote pale.

Waandishi wengi pamoja na watunzi wa kazi za kifasihi huzingatia ishara fulani ili kuzifikia akili laza za wanajamii au hadhira husika. Vikale hivi hutumiwa na watunzi kama udongo wa kuufinyanga ulimwengu wa binadamu. Jamii hutumia vikale kama malighafi ya kuviunda visakale. Kulingana na maelezo ya mtaalamu Plato, kunalo wazo duniani ambalo ni la kudumu na ni kamilifu na linaweza kufahamika tu kwa kupitia akili na wala si kwa kupitia hisia. Plato anasema kuwa, chochote binadamu hukiona au kukihisi kwa kutumia hisia ni nakala ambayo si kamilifu na iliyo na ukinzo wa kile ambacho ni kikamilifu. Kilicho kikamilifu anakiita kikale.

Jung anayapanua mawazo ya Freud kuihusu akili laza akisema kwamba, katika sehemu ya chini ya ubongo, kunayo mawazo ya kale ambayo binadamu wa wakati huu huwa nayo na ambayo yamefanana na ya mababu zake. Jung anasema mawazo haya yaliyomo kwenye akili laza ndiyo vikale. Vilevile, Jung anaeleza kuwa visasili ni njia ambayo kwayo vikale hujibainisha na kueleza akili tambuzi na aghalabu hujitokeza katika njozi za binadamu. Hivyo basi, jung alitambua kuwa kunao uhusiano kati ya sanaa, visasili na ndoto. Jung anasema hili ni kwa vile zote ni njia za kuwasilisha mawazo yaliyo akilini mwa binadamu, na njia hizi hupitia katika kikale na kufikia akili tambuzi. Jung anasema kuwa njia hizi humwezesha binadamu kuuwasilisha ulimwengu wa ndani na kuupitisha kwa ulimwengu wa nje.

Kulingana na maelezo ya Jung, binadamu wote duniani huitikia kazi yoyote ya kifasihi kwa namna iliyo sawa kwa kuwa, katika akili laza jumuishi kunazo kumbukumbu zenye kitovu kimoja. Kunazo kazi za awali za uhakiki wa vikale ambazo zilikuwa na misingi yake katika mawazo ya Jung ya akili laza jumuishi. Kulingana na Burton (1968), kazi ya Maud Bodkin (1934) ilitumia uhakiki wa vikale katika kuchunguza ruwaza zilizokuwa zinajirudiarudia kwenye tungo za kishairi. Wataalamu wengine waliotumia nadharia ya uhakiki wa vikale ni kama vile: Northrop Frye, Francis Fergusson, Robert Graves, Philip Wheelwright, James Frazer, Jessie Weston, Leslie Fiedler miongoni mwa wengine. Wataalamu kama vile Jessie Weston na James Frazer wamefanya utafiti kuhusu visakale na kung'amua kuwa tabia za wanajamii na utamaduni wao hufuata ruwaza iliyo sawa. Hili limedhihirika katika maeneo yote ulimwenguni katika vizazi vyote. Utafiti wa wataalamu hawa umeikuza nadharia hii ya uhakiki wa vikale na kuifikisha kiwango cha nadharia zilizo muhimu katika uhakiki wa kazi za kifasihi.

Kunaye mtaalamu mwingine, Campell (1969) aliyeiendeleza nadharia ya uhakiki wa vikale ya Jung alipoihusisha na visasili. Hii ni baada ya Campell kuchunguza sanaa, dini na ngano za ulimwengu. Joseph Campell alipata kwamba kunavyo vipengele fulani ambavyo huunganisha kazi hizi zote. Katika kazi hii yake, Campell alithibitisha kuwa visasili ni nyimbo za kila mwanadamu popote alipo na ni ithibati ya ndoto jumuishi ya binadamu.

Nadharia ya uhakiki wa vikale imetufaa katika utafiti huu wetu kwa kuwa ni nadharia iliyo na msisitizo kuwa kila mwanajamii huwa na fikra sawa. Hili ni kutokana na ubia wa ishara. Msisitizo huu hupatikana katika ishara na ruwaza zinazopatikana kwenye tungo. Visasili, ngano na ishara zote zinazo misingi yake katika masimulizi ya tajriba ambazo ni za awali za wanajamii. Mhakiki hivyo basi huwa ana lengo la kupata vikale ambavyo hujirudiarudia na kujitokeza na ambavyo aghalabu huchukuliwa kutoingiliwa na dosari yoyote. Vilevile, nadharia ya vikale hudhibiti muundo wa tungo. Hili ni kwa sababu maana ya kazi yoyote ya kifasihi husetiriwa katika imani za kisaikolojia na utamaduni wa jamii. Hii ina maana kuwa vikale ni miundo ambayo ni ya kimsingi na kamwe haiwezi kueleweka na ambayo hujitokeza tu kupitia ishara, ruwaza na taswira mbalimbali.

Nadharia ya uhakiki wa vikale imekuwa mwongozo mwema kwetu kwa kuwa vikale hujirudiarudia kuanzia mwanzo hadi mwisho wa ulimwengu na kuonyesha jinsi mwanajamii hukubali hali anamojikuta na kuwa hana uwezo wa kubadilisha hali zile. Msisitizo katika ruwaza ambazo hujirudiarudia kama vile za uhusika, mandhari na msuko wa kazi nzima hutumulikia tajriba za wanajamii. Ruwaza hizi za vikale pia hupatia hadhira hamu ya kushiriki katika imani na pandashuka za kipindi na wakati inamoishi. Kulingana na Sugg (1992), nduni za kivikale husaidia katika kuielewa matini na pia huchangia katika kufafanua viwango vya matamanio na dukuduku za mwanajamii.

### 1.6.2 Mihimili ya Nadharia ya Uhakiki wa Vikale

Mihimili miwili ya nadharia ya vikale ni; mhimili wa anthropolojia na mhimili wa saikolojia. Mhimili wa anthropolojia una usuli wake kutokana na kazi yake Frazer (1890) , iliyoangazia hadithi za kimila. Abrams (1971:11-12), anaeleza kwamba kazi hii iliangazia ruwaza za kimsingi na ambazo zilikuwa zikijirudia katika visasili kutoka jamii tofauti tofauti.

Anthropolojia huhamasisha akili za wanajamii juu ya vikale na vikale hivi humulika imani zao kuhusu mambo yoyote wanayoyajadili au kuyasoma. Katika kazi hii yetu, swala la ujagina katika jamii halina mpaka wazi. Ni swala linaloivuka mipaka ya wakati na utamaduni na hivyo kuonyesha ya kuwa wanadamu wote ni sawa popote walipo, hivyo binadamu ni tu mmoja. Mhimili huu wa kianthropolojia utatusaidia kuhakiki hali halisi ya maisha katika jamii. Ingawa jagina Nabii Isa ni wa kutoka jamii tofauti na jagina Sundiata, wazo hili la wanadamu wote ni sawa popote walipo litakuwa la muhimu sana katika kuuwangalia mfanano wa hawa majagina wawili.

Mhimili wa saikolojia kwa upande ule mwingine una usuli wake katika kazi yake Jung (2001) juu ya akili laza. Jung anasema kuwa vikale huwa ni kumbukumbu za picha za asili zinazorudiwarudiwa kwa ajili ya tajriba anayopitia mwanadamu katika maisha yake. Jung anasema kuwa picha au taswira hizi hurithishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine na kuwekwa kwenye akili laza jumuishi ya jamii.

Kulingana na Jung (khj), saikolojia ya nadharia ya vikale husaidia kuyaangazia maisha jinsi yalivyo hasa tunapojadili na kuchanganua mambo muhimu kuwahusu majagina na ujagina wao katika jamii. Katika kuangazia maisha ya jagina katika jamii, tunaona pandashuka wanazozipitia katika hali zote, za faraja na za dhiki. Hali za faraja na dhiki katika maisha yao ni picha halisi ya wanajamii. Vikale katika kazi yoyote hivyo basi hutuwezesha kujielewa sisi wenyewe kama wanajamii, yaani ukale wetu. Nadharia hii ya vikale hivyo basi inaleta dhana ya kuwa binadamu wote wamefanana na ni sawa mahali popote walipo. Mhimili huu wa saikolojia hivyo basi utatuongoza katika kuchanganua picha zinazotokea mara kwa mara katika akili za wanajamii. Wataalamu wa nadharia ya vikale wanaeleza kuwa umaarufu katika kazi yoyote ya kisanaa hutokana na wahusika wenyewe, taswira na maudhui yanayorudiwarudiwa katika kazi za kifasihi.

Katika kazi yetu, tumeongozwa haswa na mawazo ya Northrop Frye kuhusu vikale. Northrop Frye mwanzoni alikuwa mwanafunzi wa Teolojia kisha baadaye akawa wa fasihi. Aliinuka na kufikia kiwango cha mwandishi wa kimataifa na akaandika kitabu chake cha Anatomy Criticism ambacho kilimfanya kuwa mhakiki asilia, mashuhuri na mshawishi mkubwa katika uhakiki wa kisasa. Northrop Frye alifariki mnamo mwaka wa 1991 akiwa amechapisha vitabu takriban ishirini

kuihusu fasihi ya kimagharibi, utamaduni, hadithi za kikhurafa, nadharia ya vikale, vitabu vya dini na vilevile vya kijamii.

Frye alifasiri fasihi kwa kuangazia matabiko na hadithi. Aliigawa hadithi yoyote ile katika sehemu tatu; Uhakiki wa vikale, uchambuzi wa kuumba vipengele kutoka kwa kimoja kikuu na uchambuzi wa upunguzaji. Anasema kuwa, vikale ni ishara au picha ambayo hutokea mara kwa mara katika kazi za kifasihi na ambayo hujitokeza kama ishara ya tajriba aliyo nayo mwanajamii kuhusu jambo fulani.

Uhakiki wa vikale ni njia ambapo uelewaji wa maandishi hutokana na taswira za tamaduni zilizotumika ndani yake na taswira hizi huwa msingi wake ni hadithi na matambiko yanayopatikana katika jamii husika. Kulingana na mawazo ya Frye, kuna aina mbili za uhakiki; uhakiki wenye umuhimu na uhakiki uso umuhimu. Uhakiki uso umuhimu hauwezi ukamsaidia msomaji kukuza mawazo yenye mtiririko wa ujumbe uliopo kwenye matini yoyote ile. Katika ufasiri wowote wa kazi ya kifasihi, historia na falsafa ya jamii husika ni ala muhimu. Hivyo basi, uhakiki wa vikale una msingi wake katika falsafa na historia ya jamii. Uhakiki wa vikale ni aina ya uhakiki ulio na umuhimu.

Frye (khj) anaendelea kusema kuwa uhakiki vilevile unaweza kuwa wenye utaratibu wa kimuundo au wa kihistoria. Uhakiki umuundo humwezesha msomaji kuvielewa tu vipengele kadhaa kwenye matini. Ikiwa msomaji anadhamiria kuielewa matini na taswira mbalimbali zinazopatikana katika ile matini, basi hana budi kujihusisha na habari za kimsingi zinazohusishwa na matini ile. Huu ndio tunaouita uhakiki wa kihistoria. Uhakiki kimuundo utamwezesha msomaji kuielewa matini kisura tu lakini uhakiki wa kihistoria humwezesha msomaji kuielewa matini kiundani na kwa njia inayoeleweka zaidi. Katika uhakiki wa vikale, uhakiki kimuundo na uhakiki kihistoria huchanganywa.

Frye anasema kwamba, uhakiki umuundo humwezesha msomaji kuielewa kazi na kuichanganua kwa kuvivunja vipengele vikuu na kupata vingine vidogovidogo ilhali katika uhakiki wa kihistoria, mhakiki ufasiri kuzaliwa kwa ile matini ambako hutokana na utamaduni na mahitaji ya jamii katika

kipindi kile. Hivyo basi uhakiki wa vikale humsaidia msomaji katika kuielewa kazi ile ya kifasihi si tu ishara, maumbo na ngano zilizomo bali pia aina au kitengo cha kazi yenyewe.

Katika maelezo yake Frye anazidi kusema ya kuwa kila hadithi huwa na kitovu chake muhimu na mtambaji au mwandishi wa hadithi hiyo hujikita katika kitovu kile ambacho kinaweza kuwa Mungu, miungu au kiumbe mwenye nguvu zisizo za kawaida. Frye anainisha hadithi katika vitengo vinne:

i. Alfajiri, majira ya kuchipua na majira ya kuzaliwa
   Hii ni awamu inayoashiria kuzaliwa kwa shujaa, uamsho na ufufuo, kuangamizwa kwa nguvu za giza na kifo. Katika awamu hii, baba na mama wa shujaa huonekana katika hadithi.

ii. Kilele, majira ya joto, ndoa au ushindi
   Katika awamu hii, shujaa hukuzwa hata kiwango cha kuabudiwa na jamii. Wandani wa shujaa hushamiri katika awamu hii.

iii. Machweo, majira ya vuli na kifo
   Hapa shujaa huanguka na kuishiwa na nguvu. Jamii hufiwa na miungu wao, kifo ambacho huwa na nguvu nyingi humfika shujaa. Shujaa hutolewa dhabihu. Wahusika kama wasaliti hujitokeza katika awamu hii.

iv. Giza, majira ya baridi na ukiwa
   Hiki ni kipindi cha shujaa kushindwa ambapo wasaliti hushinda. Wahusika katika awamu hii ni kama vile mazimwi na wachawi.

Katika uchambuzi wake, Fyre anaeleza kuwa katika kuhakiki kazi ya kidini, mhakiki anapotumia uhakiki wa vikale anamchukulia Mungu kama kikale cha mwanajamii ambaye amesawiriwa kama shujaa katika kazi husika.

Frye aliiwekea mihimili nadharia ya uhakiki wa vikale kupitia kwa kazi yake Anatomy of Criticism. Frye alidhihirisha vile vikale vinavyohusu kuzaliwa, upanzi wa mimea na majira

mbalimbali kama vile kipupwe na kiangazi vinavyoathiri fasihi. Kulingana na Frye, mihimili ya nadharia ya uhakiki wa vikale ni:

i. Kuainisha vikale vyote vinavyopatikana katika kazi husika kwa mfano kama vile kikale cha wahusika, cha dhamira, usimuliaji, baba na mama, taswira, mpenzi, kifo miongoni mwa vingine.
ii. Umuhimu wa vikale vile katika kujengwa kwa kazi husika kwa kuonyesha jinsi ambavyo vikale vile vimetumiwa kuyajenga maudhui ya kazi nzima.

Katika nadharia ya vikale, kunaye nguli au jaribosi ambaye aghalabu huandaa safari katika maisha yake kuanzia utoto wake hadi katika utu uzima wake. Wakati mwingine safari yake inaweza ikawa ya kweli ambapo jaribosi anajaribu kukitafuta kitu fulani au hata kujisaka yeye mwenyewe. Katika utafiti wetu, nguli katika utenzi wa nabii Isa ni Nabii Isa mwanaye Maryam, bintiye Imrani. Katika riwaya ya Sundiata, mhusika nguli ni Sundiata ambaye ni mwanaye Konate mfalme wa ufalme wa Mandinka.

Kulingana na nadharia ya vikale, kunaye mhusika mkinzani ambaye ni mkinzani wa jaribosi. Mkinzani hufanya juu chini kuiangamiza na kuiboronga mipango yote ya nguli. Mkinzani wakati mwingine huwa hata mwenye nguvu kumshinda nguli kama vile tajiri mkuu. Sifa za mkinzani ni kama vile ulafi na uzinzi. Katika utenzi wa Nabii Isa, wahusika wakinzani ni mwanafunzi aliyemsaliti Nabii Isa na Wayahudi ambao walimtesa Nabii Isa. Katika riwaya ya Sundiata, wakinzani ni mamaye wa kambo Sassouma anayejaribu kumwangamiza Sundiata.

Katika nadharia ya vikale kunacho kikale cha mhusika mwenye hekima. Mhusika huyu hutumiwa katika kumwasa jaribosi. Katika utenzi wa Nabii Isa kunaye Zakaria ambaye aliishi naye na kuabudu naye msikitini mara kwa mara. Hii ilikuwa baada ya Zakaria kumchukua Isa kutoka kwa familia ya Imrani. Malaika Jibrili pia alikuwa kiongozi aliyemtabiria Mariam kuhusu kuzaliwa kwa Nabii Isa, alipomvivia nguo na kisha kupata mimba. Katika riwaya ya Sundiata, mhusika mwenye hekima ni Balla, Groit mtambaji ambaye Sundiata alipewa na babaye Konate. Balla alimwelekeza Sundiata kwa mengi na kumtambia mengi kuihusu jamii yao.

Kunacho kikale cha mhusika ambaye ni mwandani wa nguli au aliye na ukuruba wa karibu sana na nguli. Mhusika huyu hutumiwa kumwangamiza nguli. Sifa za mhusika huyu ni kujitakia makuu na mwenye ubinafsi. Katika utenzi wa Nabii Isa wanafunzi wake Isa ndio waliokuwa na ukuruba mkubwa naye na mwishowe alisalitiwa na kukanwa nao. Katika riwaya ya Sundiata, wandani wa nguli ni magroit wanaotumwa na Sassouma kumwangamiza Sundiata ingawa mwishowe hawakufanikiwa kumwangamiza. Kazi hii yetu itaongozwa na nadharia ya vikale. Nadharia ya vikale ni nadharia yenye ubia mwingi. Ubia huu wake umeifanya nadharia hii kuwa ya muhimu katika kutuongoza kuzilinganisha sifa za kijagina za Nabii Isa na Sundiata kwa mujibu wa sifa bia za mashujaa na kutathmini umuhimu wao katika jamii zao.

Utenzi wa Nabii Isa ni kisakale kimaudhui, vilevile hadithi kwenye Utenzi wa Sundiata. Hivyo nadharia ya vikale ambayo huhakiki kazi zenye taswira za kikale imetumulikia katika kutoa utaratibu mwafaka wa utafiti wetu. Katika utafiti wetu tumetumia mtazamo wa Jung katika kuzilinganisha sifa za kishujaa za majagina Nabii Isa na Sundiata. Ulinganifu huu unanuia kudhihirisha kuwa jagina ni kikale ambacho huwa katika akili laza ya wanajamii na utendakazi wake ni kuwa ni mwokozi wa jamii. Binadamu wote katika ulimwengu ni sawa. Tunapoangalia asasi zote zinazomzunguka binadamu ni kuwa, jamii za ulimwengu zina mfanano mkubwa kwa kuwa vipengele kama vile dini, uchumi, sheria, elimu, mapenzi, mapishi zinao mlandano mkubwa. Vipengele hivi huingiliana, hujengana na kukamilishana na hili huipa jamii kukamilika.

**1.7 Yaliyoandikwa kuhusu Mada**

Katika sehemu hii, tumezirejelea kazi kadha zinazowahusu majagina. Kazi zilizochapishwa zenye mada za ujagina katika lugha ya Kiswahili si nyingi. Kunazo zinazoyaangazia mambo ya kijumla kuhusu majagina. Ni kazi ambazo zitakuwa za muhimu katika utafiti huu. Kuna kazi zingine zinazoieleza historia ya dini za kiislamu na kikristo kwa mapana. Kunazo pia kazi zinazoangazia maudhui katika utenzi wa Nabii Isa. Aidha kunazo kazi zilizowalinganisha mashujaa mbalimbali. Kazi hizi zote zimekuwa za muhimu sana katika utafiti wetu.

Werner (1968), katika kazi yake ametoa maelezo kuhusu visakale na visasili vya wabantu ambapo anadai kwamba wabantu huwa na uhusiano ambao ni wa karibu kilugha, desturi na mila ambazo zina mfanano mkubwa. Kazi hii ya Werner umetusaidia katika kuangalia mfanano wa sifa za Nabii

Isa na zile za Sundiata. Hata hivyo, tofauti na kazi ya Werner, tumeangalia tofauti zilizopo kati ya kazi zetu mbili kisha umuhimu wa majagina hawa wawili katika jamii zao.

Mutiso (1985) aliwalinganisha mashujaa wengine na mtume Muhammad. Alirejelea Kasida ya Hamziya ili kutathmini usawiri wa Mtume Muhammad ambaye ni shujaa wa waislamu. Mutiso analinganisha sifa za jagina Muhammad na sifa za majagina wengine kwenye hurafa kutoka jamii tofautitofauti ili kutoa maelezo ya hurafa katika kasida ya Hamziyya. Katika kazi hii ya Mutiso, alieleza sifa za jagina kama vile utabiri wa kuzaliwa kwao, wenye akili pevu, wenye maisha ya dhiki tupu, aghalabu huwa wanaume, miongoni wa zingine. Kazi hii ya Mutiso imekuwa ya muhimu katika utafiti wetu kwa vile aliangazia sifa za jagina kwa jumla. Sifa hizi za jagina zimekuwa za msingi sana katika kazi yetu ya kuangalia taswira ya jagina tukiangazia Nabii Isa na Sundiata kama majagina wa jamii zao.

Mberia (1989), anauangazia ujagina wa Fumo Liyongo. Mberia anamwangalia Fumo Liyongo tu kama jagina katika ngano za masimulizi za Waswahili. Katika kazi hii, Mberia ametoa sifa tano za shujaa Liyongo ambazo anazichukulia kuwa ni bia kwa majagina wa jamii zote duniani. Sifa anazozitoa za Liyongo ni uhodari, akili pevu, nguvu za kimwili, ukoo na ujasiri. Kazi hii ya Mberia imeangazia sifa tano tu za jagina Liyongo, kazi yetu tulitarajia kupata sifa bia zaidi za jagina. Kazi hii ya Mberia imetusaidia katika kuzitambua sifa za kijagina za Nabii Isa na Sundiata. Ingawa Mberia alizitoa sifa tano za jagina, katika kazi tumepata sifa zaidi ya tano kama vile utabiri wa kuzaliwa kwa jagina, jina la jagina, jagina kwa kawaida huwa ni mwanamume, mahasidi wa jagina,kugura kwa shujaa, matendo ya kimiujiza miongoni mwa nyingine.

Katika kazi yake Mulokozi (1996), ameziharirí tenzi tatu. Haya ni katika kitabu chenye tenzi tatu alizozitolea maelezo. Kitabu hiki chake ni Tenzi tatu za Kale. Tenzi hizi tatu ni Pamoja na Utenzi wa Mwana Kupona, Utenzi wa Fumo Liyongo na Utenzi wa Al-Inkishafi. Katika kazi hii, ingawa Mulokozi ameangazia sifa chache za mashujaa, imekuwa ya muhimu kwetu kwani imetuongoza katika kuuwelewa utenzi wa Nabii Isa na kisa kwenye riwaya ya Sundiata na pia imetumulikia katika kulinganisha sifa za kishujaa za majagina hawa kwa mujibu wa sifa bia za mashujaa. Kazi yetu tofauti na ya Mulokozi, tumeangazia umuhimu wa majagina Nabii Isa na Sundiata katika jamii zao.

Mutiso (1999), analinganisha majagina wawili, Muhammad na Buddha. Katika kazi hii, Mutiso anawalinganisha Muhammad na Isa katika muktadha wa sifa bia za majagina. Ingawa Mutiso amewataja mashujaa wengine katika kazi hii akiwemo Isa, amewataja tu kuijenga kazi yake. Kazi hii ya Mutiso ni muhimu kwetu kwa vile inatueleza kuhusu hidaya walioletewa wanajamii na jagina wao ambayo ni sifa mojawapo ya jagina. Kazi hii ya Mutiso vilevile imeeleza kwa kina maana ya jagina kwa kuelezea aina za majagina ingawa anaeleza kuwa mpaka kati ya aina hizi za majagina ni finyu mno. Maelezo haya ya Mutiso yamekuwa ya muhimu kwetu sana katika kueleza maana ya jagina na kuielewa kwa kina taswira ya jagina. Katika utafiti wetu, tumeangazia taswira ya jagina kwa kuzilinganisha sifa za kishujaa za Nabii Isa na jagina Sundiata na kutathmini umuhimu wao katika jamii zao.

Kunao wataalamu wengine ambao kazi yao imekuwa ya muhimu sana katika kuangazia sifa za mashujaa. Njogu na Chimera (1999:156-168) wameangazia sifa za majagina huku wakitoa maelezo kuhusu majagina. Sifa walizoziangazia Chimera na Njogu zimetufaa sana katika kuzitambua sifa za kishujaa za Nabii Isa na Sundiata katika kuzilinganisha na sifa kwa mujibu wa sifa bia za majagina na vile vile kuangalia umuhimu wao katika jamii zao. Utafiti wetu ni tofauti na wao kwani waliangalia tu sifa za majagina na maelezo kuwahusu majagina.

Miehe na wenzake (2004), walikusanya mashairi ambayo yalikisiwa kutungwa na Fumo Liyongo wa jamii ya Waswahili. Walikusanya pia nyimbo katika machapisho ya awali kwenye hifadhi mbalimbali duniani. Nyimbo hizi zilikisiwa kutungwa na Fumo Liyongo. Wataalamu hawa vilevile walitoa ufafanuzi kuhusu mila na desturi za jamii alimokulia Fumo Liyongo. Kazi hii ya Miehe na wengine ilianzishwa baada ya kongamano lililoandaliwa Bayreuth huko Ujerumani miaka ya 2003-2004. Kusudi la kongamano hili ni kuzichambua nyimbo na mashairi yaliyohusishwa kutungwa na Fumo Liyongo kwa madhumuni ya kiusomi ulimwenguni. Kazi hii ya Miehe na wenzake imetufaa katika kazi yetu kwa vile imetusaidia katika kuuelewa mwingiliano wa vipengee muhimu katika jamii. Pia kazi hii imetuwezesha kuzielewa mila na desturi katika utamaduni wa Nabii Isa na Sundiata. Ingawa Sundiata si jagina wa Waswahili, mwingiliano uliopo wa vipengee tofauti tofauti katika jamii ya Waswahili katika kazi ya Miehe na wenzake, umetuwezesha kuuelewa mfumo wa jamii ya Afrika Magharibi ambayo ni jamii yake Sundiata.

Kazi yetu ni tofauti na hii ya Miehe na wenzake kwani tumewalinganisha na kuwatofautisha majagina kutoka jamii mbili tofauti.

Gichamba (2005), katika kazi yake, amewalinganisha majagina wawili ambao ni wa kihistoria. Gichamba amewalinganisha Fumo Liyongo ambaye ni jagina wa Waswahili na Shaka Zulu, jagina wa Wazulu. Katika kazi yake Gichamba, aliwalinganisha majagina ambao ni wa kihistoria na ambao wametoka eneo moja la Afrika. Kazi hii ya Gichamba umetufaa katika kuelewa jinsi ya kuwalinganisha majagina wawili. Imetusaidia katika kuainisha mfanano na utofauti uliopo wa sifa za kijagina za Nabii Isa na Sundiata. Utafiti wetu ni tofauti na huu wa Gichamba kwa sababu tumelinganisha sifa za jagina Nabii Isa ambaye ni jagina wa kidini na kihistoria na zile za Sundiata ambaye ni jagina wa kihistoria na kiutamaduni na kutathmni umuhimu wao katika jamii zao.

Katika kazi yake Achieng (2012), alirejelea sifa za kijagina za Lwanda Magere wa jamii ya Waluo na za Fumo Liyongo wa Waswahili kiulinganifu. Aliangazia umuhimu wa mashujaa hawa kwa jamii zao. Kazi hii ya Achieng inaangazia umuhimu wa majagina katika jamii zao. Ingawa tumeangalia umuhimu wa jagina katika jamii pana sio moja mahususi, kazi hii ya Achieng imetufaa katika kuelewa umuhimu wa majagina katika jamii zao.

Alipokuwa akiangazia jagina wa tendi, Ndumbaro (2013), katika utafiti wake, ameangazia shida anazokumbana nazo shujaa wa tendi maishani. Ndumbaro (khj), aliangazia shujaa wa tendi kwa jumla. Kazi hii inamsawiri shujaa kama mwenye uwezo wa kipekee kinguvu hata kiubashiri. Mtaalamu huyu anasema kwamba, jagina ana uwezo wa kufumbua shida zinazomkumba. Utafiti huu wa Ndumbaro umekuwa dira katika kazi yetu kwa kuwa umetumulikia jinsi jagina huyatatua matatizo ya jamii yake na pia yake binafsi. Kazi hii ya Ndumbaro ni tofauti na yetu kwani hatujajikita kwenye utendi peke yake kwani tumeangazia hadithi ya Sundiata ilioandikwa kiriwaya. Vilevile, tumeulinganisha ujagina wa majagina wawili, Nabii Isa na Sundiata.

Kalinjuma (2013), anawalinganisha majagina wa tendi za kiafrika na wale wa tendi za kimagharibi. Kalinjuma anahitimisha kazi yake na matokeo kuwa jagina wa tendi za kiafrika na tendi za kimagharibi wana mfanano mkubwa. Kazi hii inatudokezea kwamba, majagina wote huwa na sifa ambazo hukaribiana mno. Kazi hii ya Kalinjuma imetufaa katika utafiti wetu kwa vile

imetumulikia ubia wa sifa za jagina katika ulimwengu mzima kwa jumla tulipokuwa tukiwachunguza majagina Isa na Sundiata. Kazi ya Kalinjuma ni tofauti na yetu kwa vile tumeangazia umuhimu wa majagina katika jamii zao.

Kazi ya Owallah (2013), ndiyo tuliiona yenye kutupa mwanga zaidi kwa vile inaangazia maudhui katika utenzi wa Nabii Isa. Maudhui aliyoyaangazia Owallah ni pamoja na ushujaa, dini, miujiza,malezi, sharia za Torati, ndoa, maadili, dhuluma na usaliti, kifo na ufufukaji miongoni mwa mengine. Kazi hii ya Owallah, imetuongoza katika kuuangalia ujagina wa Isa kama unavyojitokeza katika utenzi wa Nabii Isa. Ingawa kazi ya Owallah imeufaa katika kuziangazia sifa za kijagina za Nabii Isa na Sundiata, ni tofauti na yetu kwani kazi yetu imelinganisha majagina wawili kwa mujibu wa sifa bia za mashujaa.

Hata hivyo tumeyaangalia makala mbalimbali kwenye vitabu vingine vya Biblia, kwenye Qurani na tovuti mbalimbali kwenye mtandao. Vilevile, tumeziangalia kazi za kifasihi ambazo zimeyaangazia maisha ya Isa kama vile, nyimbo, mashairi, majarida na magazeti. Kusudi letu la kutalii huku kwote ni kuyaelewa mazingira alimokulia Nabii Isa na utamaduni wa jamii yake. Ingawa kunazo tafiti nyingi ambazo zimefanywa kuhusu majagina wakiwemo Nabii Isa na Sundiata, hatujapata utafiti wowote uliowalinganisha. Katika utafiti huu wetu wa kuwatathmini majagina Isa na Sundiata kama majagina wa jamii zao, tulikuwa na lengo la kuliziba pengo la kiusomi ambalo limekuwepo. Tumewalinganisha Nabii Isa na Sundiata kwa mujibu wa sifa bia za mashujaa na umuhimu wao katika jamii zao.

**1.8 Mbinu za Utafiti**

Utafiti wetu umefanyika maktabani. Maktabani tumeyapitia mengi yanayohusiana na mada yetu. Kwanza tumeyasoma mengi kuihusu nadharia ya uhakiki wa vikale ambayo ndiyo kifaa muhimu chetu cha utafiti wetu. Tumevisoma vitabu na makala mengi ya kimapisi kuhusu historia ya wayahudi na jamii za Afrika Magharibi. Tumeyasoma mengi kuzihusu jamii zilizowazaa majagina Nabii Isa na Sundiata. Tumezipata habari ambazo zimesaidia kupata historia ya majagina Isa na Sundiata. Kati ya kazi nyingi tulizozisoma kumhusu Nabii Isa, tuliuchagua Utenzi wa Nabii Isa kwa vile umeandikwa na mwandishi Musa Mzenga ambaye kulingana na Abdalla Abdilatif anapohariri utenzi ule ni kwamba ni mshairi aliyebobea katika nyanja ile na hivyo tunaweza

kusema ni mwanajamii aliyeuelewa mfumo wa jamii. Mwanajamii huuelewa mfumo wa jamii yake kiukamilifu na maana kamilifu zilizosetiriwa na vikale mbalimbali. Kilichotuchochea kuchagua Utenzi wa Sundiata ni kwa sababu imeiangazia historia ya jagina Sundiata kwa mapana na marefu, kabla ya kuzaliwa kwake hadi kifo chake. Vikale vyote kwenye hadithi hii vinaichora taswira ya jagina aliyekamilika.

Tumeusoma utenzi wa Nabii Isa ulioandikwa na Musa Mzenga kwa kina huku tukiangazia vipengele muhimu kuhusu jagina Nabii Isa. Tumeyaangazia matukio mbalimbali ambayo yametuwezesha kuipata taswira kamili ya Nabii Isa. Vilevile, tumeyasoma makala mengi kumhusu Sundiata jagina wa Wamali. Tumeusoma kwa kina Utenzi wa Sundiata ulioandikwa na D. T Niane. Data tulizozipata tumezichanganua kwa kutumia nadharia ya uhakiki wa vikale. Vilevile, tumetambua jinsi ya kuwalinganisha majagina kwa mujibu wa sifa bia za mashujaa na hivyo habari hizi zimetusaidia katika kuwalinganisha majagina Isa na Sundiata..

Maktabani, tumevisoma vitabu vingi vinavyoangazia historia ya Isa. Makala yote yenye kutoa mwangaza katika utafiti wetu yamekuwa na umuhimu mkubwa kwa vile yametuwezesha kupata data ambazo tulihitaji katika utafiti wetu. Data hizi zimetuwezesha kuzilinganisha sifa za kijagina za Nabii Isa na Sundiata kwa mujibu wa sifa bia za mashujaa na kutathmini umuhimu wa majagina hawa katika jamii zao. Vilevile, tumetalii tovuti mbalimbali kwenye mtandao ambazo zimetupatia habari zaidi kuhusu utafiti wetu. Habari hizi vilevile zimetuwezesha kupata sifa zaidi za majagina Isa na na Sundiata na umuhimu wao katika jamii zao na pia kushadidia yote yaliyojitokeza katika kazi yetu.

Utenzi wa Nabii Isa umeandikwa kwa mtazamo wa dini ya Kiislamu na hivyo tumetalii tovuti nyingi mtandaoni na kupata maelezo yaliyotusaidia kuelewa utenzi huu. Tovuti mbalimbali zimetuwezesha kupata nyimbo, mashairi na makala mengi kuwahusu Nabii Isa na Sundiata. Hili limetuwezesha kuwaelewa kwa kina majagina hawa. Mtandaoni tumeyasoma mengi kuhusu nadharia ya uhakiki wa vikale ambayo ndiyo imekuwa mwongozo katika mchakato mzima wa utafiti wetu.

**1.9 Hitimisho**

Katika pendekezo la utafiti wetu, tumeangazia mambo ya kimsingi ambayo tumeyashughulikia katika utafiti wetu ambayo ni pamoja na: Utangulizi, Tatizo la Utafiti, Maswali ya Utafiti, Malengo na Madhumuni ya Utafiti, Sababu za Kuchangua Mada, Upeo na Mipaka, Msingi wa Kinadharia, Yalioandikwa kuhusu Mada na Mbinu za Utafiti. Mada yetu ya utafiti ni taswira ya jagina ambapo utafiti huu unalenga kuzilinganisha sifa za kijagina katika Utenzi wa Nabii Isa na Utenzi wa Sundiata kwa mujibu wa sifa bia za mashujaa na vilevile kutathmini umuhimu wa Isa na Sundiata katika jamii zao. Isa na Sundiata ni majagina wa maeneo, vipindi na jamii tofauti. Ingawa kunazo kazi nyingi ambazo zimewalinganisha majagina, ulinganishi wa Nabii Isa ambaye ni jagina wa jamii nyingi na Sundiata wa jamii ya Afrika Magharibi haujafanywa hapo mbeleni na hivyo utafiti wa namna hii unachangia katika kuthibitisha mfanano uliopo wa majagina wa jamii pana na wa jamii ndogo ulimwenguni kote na pia unadhihirisha umuhimu wa majagina hawa katika jamii zao na hata katika jamii pana.

## SURA YA PILI

## MAPISI YA NABII ISA NA SUNDIATA PAMOJA NA HISTORIA YA JAMII ZILIZOWAZAA NA KUWAKUZA.

### 2.0 Utangulizi

Katika sura ya kwanza tumeeleza kuwa mashujaa huzuka katika na kipindi na hali fulani na kwa malengo mahususi katika jamii. Majagina tunaowatafitia, Nabii Isa na Sundiata, walizuka katika jamii zao katika mfumo na hali fulani mahususi. Ni muhimu kuijua na kuielewa historia ya jamii zao. Historia hii yao huwa ya muhimu katika kuwaelewa majagina Isa na Sundiata vizuri hasa jamii zilizowazaa, wakati na kipindi walipozuka na vilevile maisha yao kwa jumla. Tumeangazia pia kazi waliozitenda, misukosuko katika maisha yao na uhusiano wao na wanajamii wengine.
Historia ya majagina hawa tumeiangazia katika hali tatu: kabla ya kuzaliwa au kuzuka kwao, wakati wa maisha yao na maisha baada ya vifo vyao. Katika kuangazia hali hizi tatu, tutaweza kuwaelewa majagina Isa na Sundiata vizuri na umuhimu wao katika jamii zao.

### 2.1 Historia ya wayahudi

Asili ya Nabii Isa ni jamii ya Wayahudi, ambayo pia huitwa Israeli. Jamii ya Israeli ina kitovu chake kutoka kwa baba yao, Ibraham. Ibraham alikuwa mwanawe Yitshak na Yitshak huyu alikuwa mwanawe Yaaquub (aliyeitwa pia Israeli). Jamii ya Wayaudi (Israeli) iliishi katika nchi ya Kanaani, ambayo baadaye iliitwa Israeli. Jina hili Israeli lilitokana na mtume wa Mungu aliyeitwa Yaaquub.

Jamii ya Israeli ilikuwa imetumiwa mitume wengi na Mwenyezi Mungu. Mitume hawa walikuwa wanatumwa mmoja baada ya mwingine. Kwa mfano; mtume Musa alikuwa ameteremshiwa kitabu Taurati, ambacho kilikuwa na amri za Mwenyezi Mungu kwa jamii ile. Mitume Daud kitabu cha Zaburi naye Nabii Isa aliwaletea kitabu cha Injili. Kwa kawaida Mungu alikuwa akiwatuma mitume katika jamii. Kwa mfano, Jamii ya Waislamu ilitumiwa Mtume Muhammad (s,a,w) aliyewaletea kitabu ambacho ni Qurani Tukufu.

Ingawa jamii hii ilikuwa imetumiwa mitume wengi na Mwenyezi Mungu, ilizidi kuwa kaidi na yenye udanganyifu mwingi. Iliwatesa mitume na hata kuwaua wengine. Kwa mfano, baada ya

Nabii Musa kuwakomboa kutoka kwa Firauni aliyekuwa amewaadhibu kwa adhabu kubwa hawakumwamini wala kufuata maagizo ya Mwenyezi Mungu kupitia kwa nabii wake Musa. Baada ya ukombozi wao kutoka kwa Firauni, njiani wakielekea nchi ya ahadi, walikutana na waabudu masanamu na hivyo wakawaiga na kuanza kuwaabudu masanamu kama wao. Hivyo basi, wakamwomba nabii Musa awatengenezee masanamu yao ili wayaabudu.

Kulingana na Biblia ( Wafalme 2, na Isaia 10) jambo hili lilimuudhi Mwenyezi Mungu pale alipowaua wengi wao kwa umeme wa radi. Baadaye Mungu aliwahuisha tena ili wamshukuru. Mungu alitaka kuwaingiza nchi ya ahadi (L-Qudsi) kwa kumwamrisha Musa Waisraeli wapambane na majabari kwa mikono yao. Waisraeli walikataa na kumwambia Musa aende pamoja na Mungu wake wakapambane na hao majabari wao wakiwa wamemngoja pale walipokuwa.

Mwenyezi Mungu alikasirika na kutaka kuwaangamiza wote lakini Musa alimwomba msamaha kwa niaba yao. Hata hivyo, Mungu aliwapa adhabu ya wao kutoingia nchi takatifu kwa kipindi cha miaka arubaini. Nabii Musa alipokufa, mtume Youshua alichukua usukani wa kuwaongoza Waisraeli. Hangaiko la miaka arubaini lilikuwa limewanyenyekesha mbele za Mwenyezi Mungu. Youshua aliwaongoza kuingia nchi ya ahadi. Hata hivyo, waliingia kwa kiburi na ukaidi mwingi. Jambo hili lilimuudhi Mungu alipowatumia ugonjwa wa tauni na kuwaangamiza wanajamii sabini elfu kwa saa moja.

Kulikuwa pia mtume Hezaqiil na wakati wake Mwenyezi Mungu akawaamrisha wakapigane vita. Wengi wao walitoroka majumbani kwao na kukimbilia jangwani. Sababu kuu yao ya kukimbia kwao ilikuwa, waliogopa kufa. Mungu aliwaulia huko jangwani ambapo mtume Hezaqiil aliwaombea msamaha kwa Mungu naye akawahuisha tena na wakaelewa kuwa mauti hayatokani tu na kupigana vita pekee.

Baada ya Nabii Hezaqiil, Mungu aliwatumia Nabii Ilyaas. Nabii Ilyaas alihiimiza jamii ya Wasraeli kumwabudu Mungu mmoja na kuwahimiza wasiyaabudu masanamu. Jambo hili halikuwafurahisha na wakapanga njama ya kumuuwa. Ilyaas alimwomba Mungu naye akawaadhibu kwa makali ya njaa na kuwanyima mvua kwa miaka mitatu. Mwenyezi Mungu

aliwatumia mtume Al-yasa`a aliyewaongoza katika kumwabudu Mungu mmoja kama vile tu mtume Ilyaas alikuwa amewaitia ibada ile. Walimwamini Al-yasa`a na kumtukuza.

Baada ya mtume Al-yasa`a Mungu akamtuma nabii Dhil-kifl. Kwa muda huu wote wa mitume hawa wa Mungu kupokezana hatamu, sanduku la taurati (Tabuut) lilikuwa likirithishwa mtume baada wa mwingine. Katika wakati huu wa nabii Dhil-kifl, Waisraeli walikuwa na uasi mwingi. Hivyo Mungu aliwapa nguvu L-Amaalika ambao waliwanyang`anya Waisraeli sanduku la taurati mpaka pale Mungu alipomtuma nabii Shamueli. Nabii Shamueli alifuatwa na nabii Daud na nabii Suleiman na manabii wengineo kama vile nabii Zakaria na nabii Yahya waliouawa. Nabii Isa akafuata pale walimuudhi na kupanga njama ya kumuuwa. Hawakutimiza mipango yao kwani Mungu alimpaza Nabii Isa mbinguni.

### 2.2 Misukosuko ya Kivita Iliyoikumba Jamii ya Wayaudi

Jamii ya Wayaudi ilipitia misukosuko mingi mikononi mwa jamii nyingine. Katika utangulizi wa Utenzi wa Nabii Isa (uk.2), Abdilatif Abdala anapouhariri utenzi huu anasema kuwa ni utenzi unaohusu Nabii Isa: kuzaliwa kwake, kupawa utume kwake, na misukosuko kadha anayoipitia katika kuiongoza jamii yake kwenye njia ya uongofu. Hivyo ni jamii iliyopitia misukosuko mingi katika historia yake.

Mwaka wa 587 k.k., kulikuwako na jeshi la Babiloni ambalo liliingia katika mji wa Jerusalem na kuliharibu hekalu na vilevile kuwateka nyara Wayahudi na kuwapeleka kwao Babiloni. Katika mwaka huo (khj) na kipindi hicho, kulidhihirika mabadiliko makubwa katika jamii ya Wayaudi kwani walitawaliwa na nchi zilizokuwa na uwezo mkubwa zaidi yao kwa zamu, taifa moja baada ya jingine. Mataifa haya ni pamoja na Babiloni, Shamu, Ugiriki, milki ya Roma na Byzantini, himaya ya Ottoman na vilevile Uingereza.

Babiloni ilipoanza kuwatawala mwaka wa 587 k.k., hekalu la kwanza liliharibiwa. Miaka kati ya 587-333 k.k., walitawaliwa na Shamu. Wayaudi waliokuwa wametekwa mateka walirejea Uyahudi na hekalu la pili kujengwa. Majeshi ya Ugiriki yalichukua hatamu ya kuiongoza Uyahudi kati ya mwaka wa 333 na 63 k.k., yakiongozwa na Alexander. Jeshi la Warumi nalo liliivamia

Jerusalem chini ya uongozi wa Tito na kuliharibu hekalu la pili. Katika uvamizi huo, Wayahudi walichuliwa mateka na hivyo kuhamishwa ughaibuni.

Mwaka wa 132 k.k., Barkokhba alivipanga vita ambavyo vilikuwa na nia ya kukataa utawala wa Warumi. Katika vita vya Bethar, Barkokhba aliuawa katika mlima wa Judea. Mpango huu wa Barkokhba wa kususia uongozi wa Warumi uliwafanya Warumi kupanga kuiangamiza kabisa jamii ya Wayahudi. Walifanikiwa kufanya hili walipobadilisha jina la mji wa Jerusalem na kuuita Aelia Capitolina na ule wa Judea kuuita Palestina. Wayahudi waliobakia waliguria miji na nchi nyingine kama vile Kaskazini mwa Galilee, Afrika kusini na wengine Uropa. Hata hivyo, Wayaudi hawakuiacha dini na tamaduni zao katika maeneo mapya walimohamia.

Wayaudi wakiwa katika nchi zao za ugenini, walizipitia shida na taabu nyingi. Hivyo walimtamani shujaa aliyekuwa ametabiriwa na Nabii Isaya katika Agano la kale. Nabii huyo kwa jina Masihi, walimtamani aje kama shujaa wa kivita ili awapiganie na awaongoze katika kuanzisha himaya ambayo walikuwa wametabiriwa kuwa  nayo.

### 2.3 Historia ya Nabii Isa

Utenzi wa Nabii Isa ni kisa kinachohusu Nabii Isa. Masimulizi haya yanaanzia katika maisha ya mamaye Maryamu, aliyekuwa bintiye Imrani. Maryam na mamake waliabudu msikitini kila wakati. Baadaye Maryamu alichukuliwa na mtume Zakaria ambaye aliishi naye na kumpatia mafunzo mengi ya dini na hata kumwongoza katika ibada za kila mara msikitini. Baadaye Maryamu alikutana na malaika ambaye alimtabiria kuzaliwa kwake Nabii Isa na hapo akamvivia nguo na baadaye akapata mimba bila ya kukutana na mwanamume kimwili. Mimba hii ilikuwa ya mwana wa kiume ambaye ni Nabii Isa.

Utenzi wa Nabii Isa unahusu maisha ya Nabii Isa ambaye amesawiriwa kwa misingi ya mafundisho ya dini ya kiislamu. Usawiri wa Nabii Isa katika utenzi huu wa Nabii Isa ni sawa na ule wa Nabii Isa katika Qurani tukufu. Ingawa kunavyo vitabu vinginevyo vya dini ya kiislamu ambavyo vina maelezo kuhusu dini hii, kitabu wanachokitumia katika ibada zao ni Quran tukufu. Matukio katika Quran tukufu yanalandana sana na matukio katika Biblia ya Wakristo.

Ingawa utenzi wa Nabii Isa umekuwa wa msingi katika kuiangalia historia ya Nabii Isa, tutameirejelea Quran tukufu na vilevile Biblia ili kupata habari na maelezo Zaidi. Nabii Isa katika Qurani tukufu ametajwa mara nyingi sana. Kunazo aya takriban 93 zinazomtaja Nabii Isa. Ingawa aya hizi zinamhusu Nabii Isa, hazijaandikwa kwa mtiririko wa maisha na pia mafundisho yake. Katika jamii ya Waislamu, nabii ni mmojawapo wa mitume wa Mwenyezi Mungu waliotumwa ulimwenguni kwa wanadamu na habari za kumpwekesha Mungu na kumwabudu yeye pekee.

Qurani inasema kuwa mitume au manabii hawa wa Mwenyezi Mungu walikuwa 124,000. Walitumwa wakati ule kwa vipindi mbalimbali na makundi mbalimbali, Adamu akiwa wa kwanza na Muhammad (s.w.a) akiwa wa mwisho. Nabii Isa ni miongoni mwa mitume wakuu waliopewa kitabu na Mwenyezi Mungu. Yeye alipewa kitabu ambacho ni injili.

**2.4 Kuzaliwa kwa Nabii Isa**

Nabii Isa alizaliwa na mamake Maryamu binti Imrani. (Surat "Maryam" 19, 16-35) Familia hii ilikuwa imetoka katika ukoo wa Israeli. Kuzaliwa kwake Isa kulikuwa kwa kimiujiza kama vile majagina wengine huzaliwa kimiujiza. Nabii Isa alizaliwa pasipo mamake kukutana na mwanamume kimwili. Mwenyezi Mungu alimtuma malaika Jibrili kumpasha habari za kumzaa mtoto mtukufu na kumvivia nguo ili apate ujauzito wa Nabii Isa.

Kuzaliwa kwa Nabii Isa hivyo kumetabirirwa. Katika kazi hii yetu hapo baadaye tutaona kuwa kuzaliwa kwa majagina aghalabu huwa kumetabiriwa. Katika Quran na Biblia, kuna taarifa kuwa kuzaliwa kwa Isa kulikuwa kumetabiriwa. ( Quran 3: 45 na Marko 6: 3-4)

Pindi tu Nabii Isa alipozaliwa alikutana na vikwazo kuwa mamaye alilaumiwa kupata mtoto bila mume na jamii yake. Mungu alimwezesha Nabii Isa kuzungumza angali 'kitandani' (mchanga) na kuwajuza kuwa yeye alikuwa mtume wa Mungu, jambo lililomwondolea lawama mamaye Maryam. (Quran, Surat Maryam 29-49)

Katika Biblia, Yesu alikutana na kikwazo cha kuuawa na mfalme Herode pindi tu alipozaliwa. Mfalme Herode alihofia kutwaliwa katika ufalme wake shujaa Yesu atakapokuwa amekua (Mathayo 2:13). Shujaa Yesu aliokolewa pale malaika wa Mungu alipomtokea Yusufu ndotoni na kumwambia ya kuwa amchukue mtoto Yesu na mamake Maryam na wakimbilie usalama nchi ya

Misri. Mashuja kwa kawaida huwabidi wagure nchi yao wakati wa misukosuko inawazidia na kukimbilia usalama kwingine.

Nabii Isa anapozaliwa anazungumza angali kinda mikononi mwa mamake. Hili pia hutokea miongoni mwa majagina. Huu ulikuwa muujiza ambao ulidhihirisha kuwa Nabii Isa hakuwa mtoto wa kawaida. Katika Quran takatifu, Surat 'Maryamu' (19) aya za 16-35, inaeleza kuhusu kuzaliwa kwa Nabii Isa. Quran tukufu inasema;

Na mtaje Maryamu katika Kitabu,
pale alipojitenga na jamaa zake
mahali upande wa mashariki
na akaweka pazia kujikinga nao.
Tukampelekea Roho wetu,
akajifananisha kwake sawa na mtu.
(Maryamu) akasema: Hakika mimi najikinga
kwa Mwingi wa Rehema aniepushe nawe
, ukiwa ni mcha Mungu.
(Malaika) Akasema: Hakika mimi
ni mwenye kutumwa na Mola wako
ili nikubashirie tunu ya mwana aliyetakasika.
Akasema: Nitampataje mwana
hali mwanamume yeyote hajanigusa,
wala mimi si kahaba?
(Malaika) akasema: Ni kama hivyo!
Mola wako mlezi amesema: Haya ni mepesi kwangu!

Kuzaliwa kwa njia hii Isa alizaliwa kwayo ni mfano mmojawapo wa aina nne za uumbaji. Aina nyingine ni pale Mungu anamuumba Adamu bila baba na mama, anamuumba Hawa bila baba na mama na akaumba wanadamu wengine wote kutokana na njia ya baba na mama.

Nabii Isa alikuwa ametumwa kuleta kitabu injili. Ujumbe wake ulikuwa ule ule uliotumwa mitume na manabii waliomtangulia kuwa Mungu ni mmoja na kuwa hana mwenzake na yeye peke yake ndiye anayepaswa kuabudiwa. Kitabu hiki Injili kilichoteremshiwa Nabii Isa kilikuwa na ujumbe uliolenga jamii ya Wayahudi kama vile Allah S.W anasema kwenye Qurani kuwa;

"msadikishaji wa yale yaliyokuwa
kabla yangu katika Taurati,
na ili niwahalalishieni baadhi ya yale
mliyoharimishiwa, na nimewajieni
na Ishara kutoka kwa Mola wenu,
kwa hiyo mcheni Mwenyezi Mungu na mnitii". (Qurani sura ya 3, aya ya 50)

Kwa kawaida, Mwenyezi Mungu huwatunukia Mitume kipawa cha miujiza ili kuwasaidia katika kazi yao ya utume. Mashujaa aghalabu hufanya miujiza na kuyafanya mambo yenye uhalisiajabu. Nabii Isa aliifanya miujiza mingi. Kwa mfano; aliwaumba ndege kwa udongo na akawahuisha na wakapaa angani, aliwaponya wagonjwa kama vile wa ukoma, aliwaponya vipofu, akawafufua wafu na akawateremshia wafuasi au umati wake chakula kutoka juu mbinguni.

Katika Utenzi wa Nabii Isa, Ubeti wa 289 na wa 299 unaeleza kuwa Nabii Isa alichukua muda wake mwingi msikitini akiwa ibadani. Wengi wa Wayahudi hawakuacha ibada zao za masanamu na walitafuta njia nyingi za kuhalalisha ibada hiyo ya masanamu. Haya ni kwa mujibu wa ubeti wa 310. Kuna ambao hawakuamini kuwa Nabii Isa alikuwa mtume wa Mwenyezi Mungu. Jambo hili liliteta tofauti nyingi miongoni mwao. Kuna kundi lililomchukia na kumshutumu na kisha kupanga njama ya kumuua.

Katika Biblia (Marko 15:1-37), waliopanga njama ya kumuua Yesu walimtumia mwanafunzi wakeYuda kwa kumpa vipande vya fedha (vipande 30) ili awasaidie kumkamata. Yuda alimsaliti Yesu kwa kuwaelekeza kuwa atakayembusu ndiye Yesu. Yuda alimwendea Yesu na kumbusu ili kumtambulisha. Walimkamata Yesu na kumsulubu hadi kifo. Baada ya Yesu kufa, alifufuka baada ya siku tatu na kupaa juu mbinguni. Wakristo huamini kuwa Yesu yu mbinguni na ameketi katika mkono wa kulia wa Mungu na ya kuwa atarudi duniani siku ya mwisho na kuwahukumu waliokufa na watakao kuwa hai.

Maelezo ya Qurani tukufu nayo ni tofauti na haya ya Biblia kwani inaeleza kuwa Isa hakufa msalabani bali alichukuliwa na Mungu akapaishwa juu mbinguni. Mwenyezi Mungu

aliyakamilisha haya kwa kumfananisha mtu mwingine na Isa aliyesulubiwa wakidhani ni Isa. Katika Qurani (an-Nisaa:157-159) inasema;

> Na kauli yao: Hakika sisi tumemuua
> Al-Masiyh `Iysaa mwana wa Maryam, Rasuli wa Allah.
> Na wala hawakumuua wala hawakumsulubu
> lakini walishabihishiwa tu. Na hakika wale
> waliokhitilafiana katika hayo, kwa hakika wamo katika shaka nalo.
> Hawana ujuzi nalo kabisa isipokuwa kufuata dhana tu.
> Na kwa kwa Yakini hawakumuua. Bali Allaah alimnyanyua kwake.
> Na Allaah daima ni mwenye hikmah wa yote
> na hakuna yeyote katika Ahlil-Kitaabi ila
> atamwamini kabla ya kufa kwake.
> Na siku ya Qiyaamah atakuwa shahidi juu yao.

Hata hivyo, katika simulizi hizi mbili za Waislamu na Wakristo ni dhahiri kuwa Nabii Isa alipaa mbinguni na wote huamini kuwa atarudi duniani kuimalizia kazi yake. Haya ni kwa mujibu wa Qurani na Biblia. Majagina kwa kawaida hukamilisha kazi yao kwani hata baada ya kugura kwao, wao hurejea kwenye jamii zao na kukamilisha kazi zao za ukombozi.

### 2.5 Historia ya Himaya ya Mali

Himaya ya Mali ilikuwa himaya katika eneo la magharibi mwa Afrika. Himaya hii ilikuwa kubwa kwani ndiyo nchi za Guinea, Mali, Senegali, Gambia , Mauritania, Niger na Guinea Bissau ya leo. Ilikuwa na utawala wa kifalme. Mji mkuu wa himaya hii ulikuwa unaitwa Niani. Kulikuweko na miji mingine midogo midogo kama vile Timbuktu, Gao, Djenne na Walata.

Himaya ya Mali ilidhibiti njia za kibiashara kanda ya jangwa la Sahara mpaka Uropa na Mashariki ya Kati. Biashara katika himaya hii ilikuwa hasa ni ya dhahabu. Wanabiashara walitembea kwa makundi au walitumia ngamia. Dini yao ilikuwa ni ya utamaduni wa kiafrika kisha baadaye ikawa ya Uislamu.

Historia kwa kawaida hueleza kuhusu mambo yaliopita. Historia ya himaya ya Mali ya kale inahusu kisa cha shujaa Sundiata, mfalme wa Mali. Mali ya kale ilikuwa na watambaji wa kihistoria waliokuwa wanaitwa groit ambao waliipitisha historia ya Mali kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Groit walikuwa wanapelekwa mafundishoni kama ilivyo kawaida ya kazi yoyote ile. Kazi ya groit hasa ilikuwa kuhifadhi historia ya jamii na kuhakikisha ya kuwa jamii haikupoteza hata chembe ya historia yao.

Historia ya jamii za Afrika haianzi pale ustaarabu wa kuandika na kusoma ulipofika Afrika. Kabla ya ustaarabu wa kusoma na kuandika, watu wengi katika himaya za Afrika walikuwa hawajui kusoma na kuandika. Hivyo basi, usimulizi wa kiutamaduni ndiyo iliyokuwa elimu. Himaya ya Mali ya kale kama himaya nyinginezo ilikuwa na utamaduni, imani, mfumo wa utawala na thamani ya jamii yao. Kazi za groit zilikuwa kuzipitisha tamaduni, imani, mfumo wa utawala na thamani ya jamii kwa vizazi vya baadaye.

Utawala wa himaya ya Mali ulikuwa ule wa kurithishwa. Kulikuwapo na wafalme watangulizi ambao walikuwa wa ukoo wa Sundiata. Wafalme walikuwa na groit wao wa kibinafsi na hao groit wa wafalme walikuwa wanarithishwa kutoka kwa ukoo mmoja. Katika jamii hii ya Mali, wafalme walikuwa na groit kutoka ukoo wa Kouyatds. Mamoudou alikuwa groit wa mfalme Maghan Konate (babake Sundiata) naye Balla aliyekuwa groit wa Sundiata alikuwa mwanaye Mamoudou. Historia ya Mali ya kale iliyosimuliwa na Mamoudou Kouyate iliaminika kuwa yenye ukweli usiokuwa na doa. (Niane 1960)

Historia iliyopitishwa kwa jamii ya Mali ni kwamba, mwanzoni nchi ya Mali ilikuwa sehemu ya utawala wa wafalme wa Bambara. Wakazi wa Mali wanaojulikana kama Mandingo sio wenyeji asilia wa Mali bali walikuwa wametoka mashariki. Bilali Bounama, aliyekuwa wa ukoo wa Keitas, alikuwa mfuasi mwaminifu wa Mtume Muhammad (s.a.w). Bilali alikuwa na wana wa kiume saba na waliishi mji mtakatifu wa Mecca pale ambapo yule wa kwanza alihamia nchi ya Mali na kukaa huko. Ni kutokana na ukoo huu ambapo kulitokea ufalme wa Mali. Ukoo huu ndio ukoo wa Sundiata Maghan. Kiongozi wa jamii hii ya Mali alikuwa anaitwa ‘Mansa’

Dini katika Mali ya kale ilikuwa ya kiutamaduni na historia inaeleza kuwa Mali ya kale ilikuwa imejaa shida, dhiki na hofu ambapo Mansa Barmandana alipoelekezwa kwenye dini ya Uislamu ili kuzimaliza dhiki za Wamandinka. Sundiata alipouchukua usukani, aliufufua uchumi wa Dola ya Mali. Kwanza aliumaliza uongozi wa kukandamiza wa Soumaoro mfalme wa Sosso. Baadaye aliinua biashara ya dhahabu na chumvi. Vilevile, alianzisha mfumo mpya wa kubadilishana utamaduni na nchi nyingine za kigeni. Jambo hili liliinua amani katika himaya ya Mali.

Wafalme wa Mali walikuwa wawindaji hodari. Katika uwindaji wao, walikuwa wakiwasiliana na majini (walioaminika kuwa roho za miungu). Majini hawa walikuwa kama waelekezi wao. Kwa mfano mmoja wa huu ukoo, Mamadi Kani ndiye aliyevumbua firimbi ya wawindaji na kuanza kuwasiliana na jini wa msituni. Jambo hili lilimwezesha kupata wafuasi wengi ambao walitengeneza jeshi kubwa. Alikuwa analikusanya jeshi hili msituni na kuwafunza mambo kama vile utabibu wa miti shamba. Walielewa majani yaliyotibu vidonda na kuponya magonjwa. Mamadi akawa mfalme wa wafuasi wake.

Maghan Konate alirithi ufalme kutoka kwa ukoo wake kama ilivyokuwa desturi. Alikuwa na wake watatu. Wa kwanza alikuwa anaitwa Saussoma aliyekuwa mamaye Dankaran Touman na Nana Triban. Mke wa pili alikuwa anaitwa Sogolon, mamake Sundiata, Kolonkan na Djamarou. Mke wa tatu alikuwa anaitwa Namandje mamake Manding Bory (rafiki wa karibu sana wa Sundiata).

**2.6 Historia ya Sundiata**

Sundiata alikuwa jagina wa kiutamaduni wa himaya ya Mali katika kanda ya Afrika Magharibi. Alijulikana kama shujaa wa makabila mengi katika eneo hilo. Eneo hili la Afrika Magharibi lilitumia lugha ya Kimande. Lilihusisha Wabambara, Wasoninke, Wangara, Wandemka na Mandinka. Jagina Sundiata alitambulika kama mwanzilishi wa himaya ya Mali. Historia inasema kuwa alikuwa mmoja wa wafalme wakuu katika himaya pana ya Magharibi mwa Sudan.

Kunazo kazi nyingi zilizomzungumzia shujaa Sundiata, ambazo nyingi ni simulizi kama vile, hadithi mbalimbali, tendi kwa mfano Utendi wa Sunjata na hata kazi za kiriwaya. Jagina Sundiata amepewa majina tofauti tofauti katika kazi hizi. Mwandishi Niane Djibril Tamsir anamwita `jagina wa majina mengi`. Ingawa tutayagusia mengi kutoka kwa waandishi wengine, kazi yetu imejikita

katika Utenzi wa Sundiata ulioandikwa na Niane Djibril Tamsir (1960). Kazi hii ya Niane ni usimulizi wa kihistoria unaohusu maisha ya jagina Sundiata, kabla ya kuzaliwa, kuzaliwa kwake na matukio yote ya ujagina katika maisha yake.

Djibril Tamsir Niane ni mwanahistoria, mwandishi wa michezo ya kuigiza na mwandishi wa hadithi fupi. Niane alitafsiri hadithi ya Sundiata kutoka kwa groit wa Mali Djeli Mamoudou Kouyate. Ingawa kazi za tafsiri wakati mwingine hupoteza ile maana asilia, kazi hii ya Niane ni kisa kinachomsawiri shujaa wa himaya ya Mali.

Sundiata alikuwa mwanawe Maghan Konate ambaye alikuwa mfalme wa nchi ya Manden (Mali). Maghan ambaye alikuwa babake Sundiata alikuwa na wake watatu na watoto sita. Watoto wa kiume watatu na wa kike watatu. (uk 5) Maghan Konate alitabiriwa kumwoa mwanamke wa pili mwenye sura mbaya atakayemzalia mtoto wa kiume ambaye atakuwa mrithi wa ufalme wake.
Kuzaliwa kwa Sundiata kama ilivyo katika kuzaliwa kwa majagina wengi, kulikuwa kumetabiriwa. Maghan Konate alimwoa mwanamke mwenye sura mbaya aliyeitwa Sogolon na ambaye alimzalia mwana wa kiume Sundiata. (uk 7-13)

**2.6.1 Kuzaliwa kwa Sundiata**

Wakati wa Sogolon kujifungua, mfalme Maghan aliamrisha kuletwa kwa makungwi stadi tisa katika mji wa Niane. Walitarajiwa kumwangalia Sogolon na kumtunza vyema wakati wa kujifungua. Mfalme Maghan aliwaondoa wote kwenye kasri lake ila groit wake Gnankouman Doua. Kimya kilitanda pale kasrini. Mara hali ya anga ikabadilika na wingu jeusi kutanda na kufunika jua. Radi na ngurumo zilisheheni na matone mazito mazito ya mvua yakaanza kuanguka kutoka angani na vilevile upepo mkali ulivuma.

Baada ya hayo, mwangaza mkali ukamulika ghafla kutoka mashariki mpaka magharibi na kuangaza anga. Mvua ikaacha kunyesha na jua kuwaka kama ilivyokuwa mwanzoni. Wakati huo huo kungwi mmoja akatoka chumbani alikokuwa Sogolon na kumletea mfalme Maghan habari kuwa Sogolon amejifungua mtoto wa kiume. Jambo hili hata hivyo halikubadilisha hisia za mfalme kamwe kwani yule mwindaji mtabiri alikuwa amemjuza haya yote. (uk 13)

Sherehe za kuzaliwa kwa mtoto wa Sogolon zilifanyika. Mfalme Maghan aliandaa sherehe kubwa ambayo ilikuwa haijaandaliwa kwa mtoto wa bibi wa kwanza Sassouma. Magroiti walitunga nyimbo na kuziimba. Wananchi walihudhuria sherehe hiyo takriban kutoka kila pembe za Niani. Baada ya siku nane, sherehe ya kumpa mtoto jina iliandaliwa na hidaya kutoka kwa wananchi zikaletwa. Tamaduni za kumpa mtoto jina zikafanywa kama vile kunyolewa kwa mtoto. Maghan akampa jina Mari Djata Maghan.

### 2.6.2 Utoto wa Sundiata

Utoto wa Sundiata haukuwa wa kawaida kwani alitembea baada ya miaka saba. Alikuwa na kichwa kikubwa na macho makubwa. Alikuwa na sura mbaya na alikuwa mlafi aliyekila chakula kingi na kila mara alitambaa na sahani yake ya chakula. Ulemavu wa Sundiata ulimfurahisha sana mamake wa kambo na kwa upande ule mwingine kumsumbua akili sana mfalme Maghan na Sogolon.

### 2.6.3 Kifo cha Mfalme Maghan

Siku moja Maghan alimwita mwanawe Sundiata na kumsemesha kama mtu mzima. Kwanza alimpa groit wake wa kibinafsi aliyeitwa Balla. Groit alitakiwa kumwelekeza Sundiata katika mambo mengi na kumpa historia ya nchi yao. Maghan akamwosia Sundiata huku akimrithisha ufalme wake. Baada tu ya kumwousia mwanawe, akaaga dunia.

Mfalme Maghan alipokufa, Sassouma alipanga njama ya mwanawe Dankara Touman kumrithi babaye. Hivyo Touman akawa mfalme wa Niani ingawa Maghan alikuwa amemwachia Sundiata ufalme. Sassouma alisema ufalme wa Niani hauwezi kuachiwa mtu aliyekosa nguvu miguuni.

### 2.6.4 Muujiza wa Sundiata Kutembea

Siku moja Sogolon alihitaji majani ya mbuyu na ikabidi akamwombe Sassouma ambaye alimuudhi kwa kumwambia kuwa mwanawe Dankaran Touman anaweza kutembea, kuchupa na kurukaruka kila mahali hivyo humchumia majani ya mbuyu na anayo mengi ya kumgawia. Hili lilimuudhi Sogolon. Aliporudi kwake alimchapa mwanawe kwa uchungu aliokuwa nao. Alikimbia chumbani na kulia kwa uchungu. Sundiata kuona hivyo, alimwita groit wake Balla na kumwagiza amtafutie chuma.

Chuma kililetwa, kilichokuwa kizito kiasi cha kubebwa na watu sita. Sundiata alikitumia kujinyanyua. Alijaribu kunyanyuka na alijisaidia na kile chuma. Alitumia nguvu nyingi na jasho jingi likamtoka. Balla, mamake na wote waliokuwamo walitazama kwa mshangao. Sundiata alitumia kile chuma mpaka akasimama, chuma kile nacho kikajipinda. Mamake alifurahi na kuimba:

Oh siku, siku ya kupendeza
Oh siku, siku ya furaha
Allah Mwenyezi, hukuumba
Siku iliyoshinda hii
Ni kweli mwanangu atatembea! (T.Y)

Sundiata alisimama wima kama mwanajeshi. Akatembea hatua zake za kwanza zilizokuwa na kishindo kikuu. Groit Balla akaimba:

Njia, njia, tengenezeni njia!
Simba ametembea
Paa wajifiche,
Mwondokeeni njiani! (T.Y)

Sundiata alitembea kuelekea nyuma ya Niani. Aliung'oa mbuyu pamoja na mizizi yake akampelekea mama yake. Sundiata alipotembea alipokezwa elimu nyingi ikiwemo ya uwindaji, historia ya wafalme na uganga wa miti shamba. Walimu wake wakuu walikuwa Sogolon na groit wake Balla. Ni katika umri wa miaka kumi ambapo jina lake liligeuka kutoka Mari Djata na kuwa Sundiata. Hili mwandishi Niane anasema lilichangiwa na mabadiliko ya haraka ya lugha ya Mandingo.

Uongozi wa Touman na mamake Sassouma uliiletea taabu na dhiki nyingi familia ya Sogolon. Kwa mfano, Sassouma aliwaagiza wachawi tisa kumuua Sundiata. Sundiata aliiokoa roho yake kwa ukarimu mkubwa aliouonyesha kwa wachawi wale. Pia, mfalme Touman kwa njama ya mamaye aliamua kumtuma Balla kama balozi katika nchi ya Sosso. Hili lilikuwa na nia ya kumpokonya Sundiata groit aliyepewa na babaye Maghan Konate. Jambo hili lilimghadhabisha sana Sundiata.

Sogolon na wanawe waliamua kugura Niani misukosuko ilipokuwa mingi. Hawakumwacha nyuma nduguye wa kambo Manding Bakari kwa vile alikuwa mwandani wa karibu sana wa Sundiata na hangesazwa na chuki ya Sassouma. Kama ilivyo kawaida ya majagina, wao huhama kwao misukosuko inapowazidia, kwa mfano jagina Fumo Liyongo aligura kwao alipohofia kungamizwa na aliyekuwa mfalme wa Pate Daudi Mringwari. Sundiata, mamaye na ndugu zake walihama kutoka nchi yao. Mwandishi anasema:

> Miguu yao ilichimba mchanga na vumbi la barabarani.
> Walipitia mateso na matusi ambaye ni
> tu wakimbizi wanaweza kuyaelewa.
> Walifungiwa milango na
> wafalme kuwafukuza kutoka kwa nchi zao.
> Hata hivyo, hayo yote yalikuwa sehemu tu
> ya takdiri kuu wa Sundiata (uk 28) . (T.Y)

Walipohama Niani, Sogolon na wanawe walihamia nchi ya Djedeba ambako kulikuwa na mfalme Mansa Konkon, mchawi mkuu. Walikaa Djedeba kwa muda wa miezi miwili. Wakati walipokuwa kwake, Mfalme Konkon alimshirikisha Sundiata katika mchezo wa wori ambao aliutumia kama mtego. Sundiata angeshindwa katika mchezo huu angeuawa. Baada ya mchezo Sundiata alishinda na hili likamfanya mfalme Konkon kuwafukuza. (uk 29)

Sogolon na wanawe walihamia nchi ya Tabon, wandani wa nchi ya Niani. Baada ya Tabon wakaenda Ghana na mwishowe wakafika nchi ya Mema. Sundiata alikulia Mema na kufikia umri wa miaka kumi na saba.

> Miaka saba ilipita na Sundiata akakua.
> Mwili wake ukamea misuli na
> changamoto zikaunoa ubongo wake.
> Akawa mwanaume…kama vile mche,
> alichipuka kuelekea juu angani. (uk 28) (T.Y)

Nguvu za ajabu za Sundiata zilidhihirika katika uwindaji wake na nyuta zake zisizoweza kupindwa na yeyote. Baada ya miaka mitatu wakiwa Mema, mfalme wa Mema akamteua Sundiata kama msaidizi wake. Hata hivyo Sundiata aliamua kuacha wadhifa wake na kurudi Niani kuikomboa

nchi yake kutoka mikononi mwa mfalme wa Sasso Soumaoro Kante. Ni wakati huohuo mamake alipokufa. Sundiata aliomba nafasi ya kumzika mamake katika nchi hiyo ya Mema lakini mfalme alikataa kwa kuwa hakufurahishwa na wazo la Sundiata kurudi Niani.

Mfalme Moussa Tounkara alidai malipo ya ardhi atakapozikwa Sogolon kutoka kwa Sundiata. Sundiata alimletea manyoya ya kanga,vigae vya nyungu na mabua. Jambo ambalo mshauri wa Tounkara alimwonya mfalme kuwa ni ishara ya uharibifu wa uongozi na nchi. Hili lilimfanya mfalme amkubalie Sundiata kumzika mamaye na akafunga safari yake kurudi nyumbani kwao Mali.

Baada ya kurejea nyumbani, Sundiata alikuwa na kiu kuu ya kuziunganisha falme za Afrika Magharibi ambazo zilikuwa zimegawika tangu pale ufalme wa Ghana ulipoanguka. Alitaka kuyaunganisha makabila takriban yote ya Afrika Magharibi. Alionesha haki katika kugawa ardhi na katika kutoa majukumu katika himaya yake. Historia inasema kuwa mfalme Sundiata ndiye aliyekuwa mwanzilishi wa mwongozo uliokuwa na haki za kibinadamu ulioitwa Kouroukan Fouga. Sundiata vilevile alikuwa jabari katika vita, jambo lililomsaidia katika kuijenga himaya ya Mali.

Sundiata alipokufa katika mwaka wa 1255 B.K., mwanawe Wali alichukua usukani lakini aliegemea sana upande wa maendeleo ya kilimo. Anayejulikana sana baada ya mfalme Sundiata ni mfalme Mansa Musa ambaye utawala wake ulikuwa wa takriban miaka 25. Aliimarisha ufalme wa Mali mara tatu kibiashara. Mali ya kale ilisifika kwa sanaa ya uumbaji na elimu. Chuo cha kwanza kilijengwa Timbuktu na vilevile shule za kifahari. Baada ya Mansa Musa kufa, himaya ya Mali ilipungua.

## 2.7 Hitimisho

Sura hii ya pili imeshamiri historia, nyakati na mazingira yaliyowazaa na kuwakuza majagina Nabii Isa na Sundiata. Katika sura ya kwanza, tulitanguliza kusema kuwa jagina huzuka katika kipindi fulani na kutatua matatizo ya wanajamii. Sura hii ya pili tumeonyesha sababu za majagina Isa na Sundiata kuzuka katika jamii zao wakati ule na matarajio ya jamii zao kwao.

## SURA TA TATU

## KULINGANISHA SIFA ZA KIJAGINA ZA NABII ISA NA SUNDIATA

### 3.0 Utangulizi

Tenzi nyingi zinazoandikwa kuwahusu mashujaa na masuala mengine katika jamii husika huwa zimeshamiri masuala muhimu ya kihistoria. Haya ni kwa mujibu wa Gichamba (2005) akiwanukuu Chiraghdin, Baruwa na Nabhany (1975:63). Wataalamu hawa wanaendelea kusema kuwa maudhui katika tenzi nyingi katika fasihi tofauti tofauti za ulimwengu aghalabu husifia na kutukuza utaifa katika historia za jamii. Kazi hizi vilevile huwatukuza wanajamii walioaminika kumatendo makubwa (majagina) katika maisha yao. Katika sura hii tunazitazama sifa za kishujaa za Nabii Isa na Sundiata. Tunaangalia mfanano uliopo katika sifa hizi za kijagina kati ya Nabii Isa na Sundiata. Vilevile tunaangazia kutofautiana kwao.

Katika kupata sifa za kijagina za Nabii Isa tumeurejelea Utenzi wa Nabii Isa, Musa Mzenga mtunzi wa utenzi huu, amejikita katika dini ya Kiislamu. Ni utenzi ambao umejikita katika mafunzo ya Qurani tukufu. Ingawa kazi yetu ya msingi ni Utenzi wa Nabii Isa, tumevirejerelea vitabu vingine ambavyo vimetumulikia zaidi katika utafiti wetu. Vitabu hivi ni pamoja na Biblia na vitabu vya hadithi kumhusu Nabii Isa.

Vilevile tumetalii mitandao mbalimbali ambayo imetusaidia katika kuyaelewa maisha na historia ya Nabii Isa. Katika kupata sifa za kijagina za Sundiata, tumeurejelea Utenzi wa Sundiata ulioandikwa na D.T Niane. Aidha, tumevirejelea vitabu vingine vyenye visa vya Sundiata. Tumerejelea mitandao tofauti inayochangia historia na maisha ya Sundiata.

### 3.1 Kuzuka kwa Majagina

Jamii huwa na asasi nyingi na mojawapo ya asasi hizi ni mashujaa. Mashujaa wana umuhimu katika jamii kwani huchukuliwa kama zawadi kutoka kwa Mungu kwa wanajamii. Kunazo aina kadha za mashujaa kama vile tulitanguliza katika sura ya kwanza kama vile mashujaa wa kihistoria,  wa kidini na hata wa kitamaduni. Majagina katika jamii hawazuki katika ombwe tupu bali huzuka katika kipindi, wakati na mazingira fulani kwa madhumuni maalumu katika jamii. Aghalabu majagina huzuka kuwatatulia wanajamii shida  fulani na kuwaondolea dhiki na hangaiko

fulani katika kipindi hicho mahususi. Shujaa huaminika kuishi hadi atakapotimiza wajibu wake. Kwa wanajamii, shujaa huwa hafi kwani hata baada ya kifo chake wao huamini kuwa anaishi miongoni mwao.

Majagina wengi aghalabu huzuka katika kipindi ambamo mna vita. Kwa mfano Fumo Liyongo ambaye ni jagina wa jamii ya Waswahili alizuka wakati palikuwepo na misukosuko mingi ya vita kati ya jamii ya Waswahili na majirani zao. Luanda Magere naye alizuka katika jamii yake wakati ambapo palikuwepo na mashambulizi mengi kutoka kwa jamii ya Wanandi. Nabii isa naye alizuka wakati jamii ya Wayahudi ilikuwa imetawaliwa na mataifa mengine ambapo ilikuwa imefanywa hata watumwa. Sundiata naye alizuka pale jamii yake ya Mali ilikuwa imetawaliwa na mfalme wa Sasso Soumaoro Kante. Jagina huwa ni mwanajamii ambaye huchukuliwa kama mwokozi katika jamii husika. Ni kikale kilichoko katika akililaza ya wanajamii.

### 3.1.1 Utabiri wa Kuzaliwa kwa Mashujaa

Kuzaliwa kwa majagina aghalabu huwa kumetabiriwa. Mutiso (1999:4), anaeleza ya kwamba kuzaliwa kwa jagina huwa kumetabiriwa kabla ya jagina kuzaliwa. Mutiso (khj), anaendelea kusema kuwa kutabiriwa huku hata kusipofanyika, huthibitishwa baada ya shujaa kuzaliwa. Kwa mfano, Mutiso (khj), anasema kuwa kuzaliwa kwa Gautama Buddha kulikuwa kumebashiriwa na wabashiri sitini na wanne ambao waliitafsiri ndoto ya mamake kabla ya kuzaliwa kwake. Kutabiriwa kwa kuzaliwa kwa shujaa ni tendo ambalo hudhihirika sana katika jamii. Kama tulivyoeleza hapo juu kuhusu kuzuka kwa majagina na kwa wakati upi, utabiri wa kuzaliwa kwa jagina huipa jamii tumaini la kupata mwokozi na hili huitia jamii moyo na kuuongeza uvumulivu wao. Watabiri katika jamii huenziwa na huaminiwa sana na wanajamii kwani huchukuliwa kuwa ngazi kati yao na Mungu. Mungu na Mitume wake ni vikale katika jamii.

Kuzaliwa kwa Nabii Isa kulikuwa kumetabiriwa na Malaika Jibrili kabla ya kumvivia Maryam nguo (ubeti 10-15) Katika Biblia, utabiri wa Nabii Isa ulifanywa na manabii wengi kama vile Isaya (Isaya 7:14), Yeremia (Yeremia 23:5) na Micah (Micah 5:2). Isaya anasema; Kwa hiyo Bwana mwenyewe atawapa ishara, tazama, bikira atachukua mimba, atazaa mtoto mwanamume, naye atamwita jina lake Imanueli. (7:14) Utabiri huu wa manabii hawa ulitimia pale Nabii Isa alipozaliwa.

Luka 2:8-11, inasema:

Na katika nchi ile kulikuwa na wachungaji ambao
walikuwa wakichunga kundi lao
makondeni kwa zamu usiku.
Malaika akawatokea na kuwaambia,
Msiogope kwa maana nimewaleteeni
habari njema ya furaha kuu
ambayo itakuwa kwa watu wote.
Maana leo katika mji wa Daudi
amezaliwa kwa ajili yenu Mwokozi,
ndiye Kristo Bwana.

Huku kutokewa kwa wachungaji na malaika ni ishara kuwa shujaa amezaliwa. Shujaa anapozaliwa, panakuwapo na ishara. Nabii Isa anapozaliwa chini ya mtende, tende mbivu zinaanguka na chini yake pakatokea kijito kidogo cha maji. Hii ilikuwa ishara kuwa anayezaliwa ni shujaa. Ishara ni aina ya kikale katika jamii. Kunazo ishara tofauti zinazoashiria mambo tofautitofauti katika jamii. Kunaye ndege fulani katika jamii ya Wakamba ambapo akitoa sauti fulani karibu na kijiji fulani, ni ishara ya kutokea kwa kifo katika kile Kijiji.

Kuzaliwa kwa Sundiata kulikuwa kumetabiriwa. Mwindaji alikuwa akiwinda karibu na malango ya mji wa Mandingo, nchi ya Mali. Mnyama aliyemfuma alikuwa ameanguka karibu na ukuta wa mji wa Mfalme Maghan Konate. Ilikuwa kati ya mila za nchi zile kuwa mnyama akianguka karibu na nchi jirani angewagawia majirani mawindo yake. Alipompelekea mfalme nyama, alimtabiria kuzaliwa kwa shujaa atakayemrithi.

Mrithi wa ufalme wako bado hajazaliwa.
Nawaona wawindaji wawili wakiingia malangoni mwako.
Naona wametoka nchi ya mbali,
na tazama, nawaona wakiandamana
na mwanamke mwenye sura mbaya,
mwenye kuificha siri kuu, mwenye nundu mgongoni
na macho yake mithili ya mazimwi.
La ajabu ni kuwa mwanamke huyu ataolewa

> na mfalme Maghan Konate na ndiye
> atakayemzalia mrithi wake ambaye
> ataifanya Mali himaya kuu na isiyokuwa na mwisho. (uk. 6).

Utabiri wa mwindaji unatimia pale Sundiata anapozaliwa. Kuzaliwa kwa Sundiata vilevile kulikuwa na ishara kwani hali ya anga iligeuka kighafla wakati wa kuzaliwa kwake. Niane anasema:

### 3.1.2 Jagina Hutokana Ukoo wa Kifalme au Familia Bora

Mutiso (1999:4) anaeleza ya kwamba, kuzaliwa kwa shujaa kwa kawaida huwa kumetabiriwa na kama hakujatabiriwa huwa kunathibitishwa baada ya jagina kuzaliwa. Mutiso (khj), anasema kuwa ithibati ya atakayezaliwa au aliyezaliwa atatokana na ukoo wa Sakya, Kureshi, Ameterasu, Gandhi, Daudi, Omikami n.k. Koo hizi ni za kifalme kwa mfano; Gautama Buddha kutoka ukoo wa Sakya na Mtume Muhammadi kutoka kwa ukoo wa Kureshi. Mara nyingi jagina hutoka katika mlango au ukoo unaochukuliwa kuwa ni mteule na Mungu. Aghalabu ukoo huu huchukuliwa kuteuliwa na Mungu kuikomboa jamii husika kutoka kwa shida na dhiki zinazoikumba.

Kwa kawaida kila jamii huusifu na kuusujudia ukoo wa jagina wao. Mutiso (1994) anasema kuwa kila mwanajamii hutilia maanani umuhimu wa ukoo huu na katika kuitaja shajara yake, hujihisi hivi kwamba amezaliwa upya. Kiongozi anapokufa katika jamii, mwanajamii mmoja kutoka ukoo wa kiongozi aliyekufa ndiye aurithio uongozi. Jagina hivyo basi hutokana na ukoo wa kiufalme au ukoo bora na aghalabu hurithi uongozi kutoka kwa jamaa zake. Hata hivyo uongozi huu hutetewa ili kuupata kwani hutokea utetezi wa uongozi wenyewe hivyo jagina hujizatiti kuutetea.

Nabii Isa alikuwa ametoka katika ukoo wa mfalme Daudi. Biblia inamwita Yesu mwana wa Daudi. Hii ni kwa sababu Yusufu ambaye ni babake Yesu alikuwa wa ukoo wa Daudi ambaye alikuwa mfalme maarufu wa angano la kale. Sundiata alikuwa mwanawe mfalme Maghan Konate. Maghan Konate alikuwa mfalme wa himaya ya Mali na alikuwa amurithi ufalme wake kutoka kwa babaye Bello Bakon.

### 3.1.3 Jina la Jagina

Mutiso (1999:16), anaeleza ya kwamba, shujaa huwa anapewa jina pindi tu anapozaliwa. Yumkini anaweza kupewa jina ambalo ni la muda na wazaziwe baada ya kuzaliwa. Akikua, anaweza kujipa jina lake mwenyewe au apewe jina na Mungu au apewe jina na mwanajamii mwenye uwezo mkubwa katika jamii. Mara nyingi jagina hupewa jina la kimajazi kutegemea jamii husika. Kwa mfano; Orkoiyot jagina wa jamii ya Wanandi na Wakipsigis ni jina lenye maana ya mwenye nguvu, Achillesi humaanisha ujasiri, Musa ni jina lenye maana ya aliyetupwa, Fumo Liyongo ni jina lenye maana nyingi kama vile mkuki wenye ncha mbili, kitendo cha kuchoma kwa mkuki, mfalme miongoni mwa maana nyingine. Maana haya ya majina ya wanajamii huwa ni vikale katika jamii. Jamii huwapa watoto kutegemea mambo mengi. Inaweza kuwa ni msimu waliozaliwa, rangi ya ngozi ya mtoto, tabia za babuye au nyanyie miongoni mwa mengine.

Katika utenzi wa Nabii Isa, Nabii Isa anarejelewa kwa majina mengi kama vile, Mtume katika ubeti wa 347 na Rasuli katika ubeti wa 792. Katika Biblia Isa ana majina mengi kama vile Luka 19:10, Luka anamwita Mwana wa Adamu. Mwana wa Adamu alikuja kuokoa na kutafuta kilichokuwa kimepotea. Majina mengine ni kam vile, Neno, Emanueli, Mfalme wa Wayahudi, Kuhani mkuu, Mkate wa uzima, Nabii, Alfa na Omega, Nyota ya asubuhi, Mwalimu, Bwana miongoni mwa majina mengine.

Sundiata jamii yake ya himaya ya Mali ilikuwa imempa majina mengi, D. T Niane anamwita mfalme wa majina mengi. Siku ya nane baada ya kuzaliwa kwa Sundiata alipewa jina Maghan Mari Djata na Doua aliyekuwa mmoja wa magroiti katika himaya ya Mandingo. Majina mengine ni kama vile, Mfalme Simba, Mfalme Nyati, Simbon (Mwindaji Mkuu), Sundiata, jina alilolipata akiwa na miaka kumi miongoni mwa majina mengine. Haya majina ya Nabii Isa na Sundiata ni dhihirisho kuwa jagina huwa na majina yakimajazi na majina haya huwa na nia ya kumkuza yule jagina katika jamii yake.

Jina la mwanajamii ni kikale ambacho huashiria matukio fulani katika jamii. Haya ni kwa mujibu wa Musyimi (2011). Jina linaweza kuwa ni kutokana na msimu mwanajamii alipozaliwa, kazi fulani katika jamii ile, tabia za wanajamii, njia ya maombi kwa Mungu au miungu yao, sehemu fulani katika jamii yao miongoni mwa mambo mengine. Kwa mfano, jamii ya wakamba ina majina yafuatayo:

| Jina | Maana |
|---|---|
| Mutuku | Usiku |
| Wambua | Msimu wa Mvua |
| Muimi | Mkulima |
| Munyoki | Mlevi |
| Mwatu | Mfuga nyuki |
| Masaku | Mji |
| Mboya | Maombi |

### 3.1.4 Jagina kwa Kawaida huwa ni Mwanamume

Mashujaa wengi ulimwenguni aghalabu huwa ni wanaume na pale ambapo mwanamke amerejelewa kama shujaa huwa hana sifa bia za kijagina ambazo wanazo majagina wanaume. Kwa mfano, jamii ya Wakamba inaye shujaa mwanamke kwa jina Syokimau. Sifa za kishujaa alizo nazo Syokimau tangu kuzaliwa kwake hadi kifo chake ni chache mno. Alizokuwa nazo ni kama vile kipawa cha kutabiri na misuli ya kiume.

Aghalabu kote ulimwenguni mashujaa huwa wa kiume kwa mfano; Fumo Liyongo, Buddha, Mtume Muhammadi, Musa, Samsoni, Luanda Magere miongoni mwa wengine. Vilevile, jamii nyingi duniani huamini Mungu kuwa ni shujaa wa kiume na ni shujaa wa mashujaa. Hili hutokana na akililaza ya jamii kuwa mwanamume huwa na nguvu nyingi kuliko wanawake na kila wakati yuko juu ya mwanamke na hivyo basi ukombozi wa jamii hutokana na mwanamume. Katika akililaza pia, mwanamke huchukuliwa kuwa dhaifu na mwoga na hivyo kutoyaweza makali yanayotokea katika jamii.

Mashujaa Nabii Isa na Sundiata walikuwa wanaume. Malaika Jibrili anapomtokea Maryam na kumvivia nguo, anamtabiria kuzaliwa kwa mtoto wa kiume atakayewakomboa Waisraeli. Shujaa huyu ndiye Nabii Isa. Mwindaji anapomtabiria mfalme Maghan Konate kuhusu kuzaliwa kwa mrithi wake, anamwambia kuwa atamwoa mke wa pili atakayekuwa na sura mbaya na ambaye atamzalia mtoto wa kiume atakayeurithi ufalme wake na kuifanya himaya ya Mali kubwa zaidi. Mtoto huyu alikuwa Sundiata.

### 3.1.5 Utoto na Ujana wa Shujaa.

Utoto na ujana wa jagina mara nyingi huwa hauelezwi. Pale ambapo utaelezwa huwa si kwa kina. Aghalabu maelezo ya utoto na ujana huelezwa kwa kuyachanganya na kuzaliwa kwa shujaa. Kuzaliwa, utoto na ujana hufanywa kuwa kitu kimoja. Kwa kawaida, shujaa anapozaliwa hukua kama mwanajamii tu wa kawaida. Upekee wa shujaa hutokea pale matendo ya kishujaa yanapoanza kuonekana na wanajamii kugutuka kuwa yule hakuwa mtu wa kawaida. Baada ya kugutuka huku kwa jamii kumhusu jagina huyu, wanaanza kumkuza na kumtukuza na hivyo kumuumba kuwa jagina wao.

Utoto na ujana wa Nabii Isa umeelezwa tu kijuujuu na Musa Mzenga katika utenzi wake wa Nabii Isa. Baada ya kunena kama mtu mzima alipozaliwa ili kumwondolea lawama mamaye, miujiza yake inaonekana baada ya miaka thelathini alipoianza huduma yake kirasmi. Utenzi wa Nabii Isa pia unaeleza kuwa Nabii Isa hakushiriki michezo ya watoto kwa mfano;

288. kwa wadogo si katiti,
Alikuwa tafauti,
Hakupoteza wakati,
Machezo hakuhudhuria.

289. mchezo wake thabiti,
Alo akijisharuti,
Ni yeye si msikiti,
Ibada kuhudhuria.

Katika Biblia, utoto na ujana wa Nabii Isa haujatajwa kwa kina ila pale aliposahaulika hekaluni na wazazi wake.

Na alipopata umri wa miaka kumi na miwili,
walipanda kama ilivyokuwa desturi ya sikukuu.
Na walipokwisha kuzitimiza siku,
wakati wa kurudi kwao,
yule mtoto Yesu alibaki nyuma huko Yerusalemu,
na wazee wake walikuwa hawana habari. (Luka 2:42-43)

Utoto na ujana wa Sundiata pia haujaangaziwa kwa kina ila kuna vijisehemu katika kukua kwake vimetajwa ambavyo vinadhihirisha miujiza. Kwa kawaida, Sundiata alikuwa na damu ya mwanamke Nyati aliyewahangaisha wanakijiji kwa kuwaua. Kwa mfano:

Nimewaua wawindaji mia moja na saba,
na kuwatia majeraha sabini na saba.
Kila siku naua mwanakijiji wa Do na mfalme. (uk. 8).

Huku kutajwa kwa maumbile ya Sundiata na mwandishi kunadhamiria kuonyesha chimbuko la uhalisiajabu wa Sundiata. Kwa mfano miaka ya kwanza baada ya kuzaliwa hakukua kama mtoto wa kawaida kwani alitembea akiwa na miaka saba. Utoto wake pia umetajwa pale D. T Niane anapoeleza mwonekano wa kitoto kilichopenda kula na chenye kichwa kikubwa na macho makubwa. Anasema:

Akiwa na miaka mitatu
alikuwa angali anatambaa kwa miguu minne
ingawa watoto wa rika lake walikuwa wamekisha kutembea.
Hakuwa na urembo wowote wa babaye Maghan.
Alikuwa na kichwa kikubwa kilichoushinda mwili kukistahimili.
Alikuwa na macho makubwa ambayo
yangefunguka pale ambapo yeyote
angeingia katika chumba chao.
Angetambaa kila mahali
alkitafuta chakula kwani alikuwa mlafi. (uk. 15)

### 3.1.7 Utetezi wa Cheo

Kila jagina huwa ana jukumu la kuikomboa jamii yake kutoka kwa shida fulani au la kuiondolea jamii yake dhiki fulani. Katika kulitimiza jukumu lake, anahitaji kuwa na wadhifa wa uongozi. Mara nyingi jagina huwa hakipati cheo hiki cha uongozi kwa njia rahisi. Mara nyingi hupitia changamoto nyingi katika kukipigania cheo chake kwani maadui huwa kikwazo. Jagina hutumia njia nyingi na anaweza kufanya chochote kuhifadhi nafasi yake ya uongozi hata wakati mwingine anaweza kuua.

Nabii Isa kama majagina wengine hakupata nafasi ya uongozi kwa njia ya moja kwa moja ingawa alikuwa wa ukoo wa Daudi. Hata hivyo hakujihusisha na vita vya kimwili kama vile majagina wengine kama vile Fumo Liyongo walivyofanya. Maadui waliomtolea upinzani aliwakabili kwa vita vya kiroho. Aliwakabili kwa mafumbo na kwa mafundisho. Kwa wengi mafundisho hayo yaliwasuta wakiwemo watawala. Wengi walimpinga na kumkataa.

Sundiata alikuwa mfalme wa himaya ya Mali aliyeijenga himaya kubwa kabisa katika Afrika Magharibi. Hata hivyo, hakuupata uongozi kwa njia rahisi. Ingawa babaye Maghan Konate alikuwa amemwachia ufalme ule, wapinzani wake wakuu walikuwa mamaye wa kambo Saussouma na nduguye wa kambo Dankaran Touman. Saussoma alifanya kila aliloliweza kumwangamiza Sundiata hata kupanga njama ya kumuua. Sundiata alikuwa mkakamavu na akaamua kukitetea cheo chake cha uongozi. Kwa mfano; wakati walikuwa wakigura nchi yao misukosuko ilipowalemea, Sundiata anamwambia Dankaran Touman:

> Kakangu Dankaran Touman,
> umemchukua groit wangu Balla Fasseke
> kutoka kwangu na unajua ni mojawapo
> ya urithi wetu kama wana wa mfalme.
> Balla hakuwa wako lakini popote alipo
> atabaki kuwa groit wa Sundiata.
> Na kwa vile hututaki hapa,
> tutaondoka tutoke Mali twende
> mbali sana na hapa lakini nitarudi.
> Nitarudi, unasikia? (U.k 27)

### 3.1.8 Mahasidi wa Jagina

Katika sura ya kwanza, tuliangazia jukumu la jagina kuwa ni kuikomboa jamii kutokana na dhiki fulani. Dhiki na shida katika jamii mara nyingi husababishwa na maadui wa jamii husika. Katika kumjenga jagina katika jamii yake, maadui huwa ni muhimu sana kwa kuwa ujagina wake hudhihirika vyema anapokabiliana na maadui au adui katika kuikomboa jamii yake. Njogu na Chimera (1999:156), wanasema ya kwamba hakuna shujaa yeyote duniani asiyekuwa na adui.

Kila mtu au mwanajamii huwa na wanaomuunga mkono katika mambo na kumpenda au wanaopinga juhudi zake na kutompenda. Mungu ambaye ni jagina wa majagina pia anao wanaompenda na wasompenda. Kwa mfano; adui wa Mungu ni shetani.  kwa hivyo ni jambo la kawaida sana jagina kuwa na adui au maadui kwani shujaa hawezi kuwepo kama hakuna waoga, mtu mzuri hawezi kuwepo kama hakuna watu wabaya. Hivyo basi shujaa hawezi kuwepo kama hakutakuwa na maadui.

Aghalabu maadui wa shujaa humwogopa na kumwogopa huku huwafanya wapange njama za kumwangamiza. Nabii Isa kama shujaa wa jamii ya Wayahudi alikuwa na maadui wengi. Katika utenzi wa Nabii Isa, maadui wake waliyapinga mafundisho yake na kupanga njama ya kumuua. Mola wake alimwepushia kifo pale alipombadilisha mmoja wao na kumfanya afanane na Nabii Isa kisura. Mtu huyo aliyebadilishwa aliteswa, akasulubiwa msalabani na akauawa.

Katika Biblia, kunao Wayahudi na Mafarisayo ambao walikuwa maaadui wa Isa. Walimchukia kwa vile walidai alijisifu kwa kujiita mwana wa Mungu. Watawala nao walihofia kung`atuliwa kutoka kwa nyadhifa zao za uongozi na hivyo wakawa maadui wa Nabii Isa. Walioyapinga mafundisho ya Isa walimtesa, wakamsulubu msalabani na kumuua. Hata hivyo siku ya tatu alifufuka na kupaa mbinguni.

Katika kisa cha Sundiata, alikuwa na maadui wengi tangu akiwa tumboni mwa mamaye Sogolon. Sogolon akiwa mjamzito, ujauzito wake ulitunzwa kwa njia ya kipekee na babaye Maghan Konate. Jambo hili halikumfurahisha mamaye wa kambo Sassouma. Kuzaliwa kwake pia kulisherehekewa na ufalme wa Mandingo kwa kuandaliwa sherehe kubwa na mfalme Maghan. Sassouma na mwanawe Dankaran Touman wakawa maadui wa kwanza wa Sundiata. Maadui hawa walipanga njama nyingi za kumwangamiza Sundiata lakini hawakufanikiwa. Moyo mzuri wa Sundiata, wepesi wa akili na ushupavu aliokuwa nao ni baadhi na mambo yaliomsaidia kuepuka mitego yote ya kifo. Kwa mfano; Saussoma anawatuma wachawi wakamuue Sundiata. Anasema:

> Nataka kumuua Sundiata.
> Mustakabali wa mwanangu wa
> uongozi unahatarishwa

na Sundiata na lazima auawe
kabla ya muda kuyoyoma.
Mkifanikiwa kulitekeleza hili,
nawaahidi zawadi nono.
Kwanza kabisa, kila mmoja wenu
atapata ng`ombe wa maziwa
pamoja na ndama wake ifikapo kesho.
Kisha katika ghala letu,
kila mmoja atapewa kipimo kikubwa
cha mchele pamoja na chakula cha mifugo. (uk. 24)

Adui ni kikale katika jamii. Jagina ambaye ni nguli huwa na mkinzani wake ambaye huwa na nia ya kuiharibu mipango yake yote. Kwa kawaida shujaa huwa mshawasha wa kuzikiuka na kuziharibu kanuni za jamii husika ambazo ni za kidhanishi na kuziibua kanuni zake za kimaadili. (Nietzsche et al., 1961)

### 3.1.9 Shujaa huwa mwenye Akili Pevu

Kwa kawaida, mashujaa huwa na akili pevu. Wao huwa na uwezo wa kung`amua mambo kwa upesi. Wepesi huu wa kung`amua mambo huwasaidia kuiepuka mitego ya maadui wao. Akili pevu vilevile humwezesha shujaa kutabiri mambo katika jamii na kuiwezesha jamii hiyo kuchukua tahadhari ifaayo. Akili pevu ya Nabii Isa inadhihirika kutokana na mafundisho yake. Alitumia mafumbo yaliyofumbwa kwenye hadithi alizozitoa na kuufanya umati wa watu kumfuata. Katika Utenzi wa Nabii Isa tukaelezwa:

544. Kwa maneno ya kutimu,
Fasaha na ya ilimu,
Kutujuza tufahamu,
Kuwa yeye ni nabia.

546. “Ni mwingi wa taaluma,
Wala sana hakusoma,
Na mambo chungu nzima,
Yeye yanamuelea.

Sundiata alikuwa na akili pevu. Kuwa na urahisi wa kung`amua mambo kulimwezesha kuiepuka mitego ya maadui zake. Kwa mfano, mitego ya mamaye wa kambo Saussoma. Sausomma aliwaagiza wachawi wa Mandingo kumua Sundiata. Sundiata aling`amua njama na kuwapokea wale wachawi kwa upendo mwingi, jambo ambalo liliwagusa wale wachawi mioyo na kumjuza kuhusu njama yao ya kumjaribu ili wamuue. Vilevile, njama ya Saussoma na mfalme wa Djedema Mansa Konkon haikufanikiwa kwa sababu ya upevu wa akili wa Sundiata. Akili pevu ya Sundiata ndiyo iliyomsaidia kuijenga himaya kubwa ya Mali.

### 3.2 Kugura kwa Shujaa

Mashujaa hugura makwao misukosuko inapowalemea. Maadui wao ambao aghalabu huwa watawala huhofia kunyang`anywa nyadhifa zao na huwaandama mashujaa wao kwa kutaka kuwaangamiza. Kwa kawaida safari humwezesha jagina kutekeleza wajibu wake katika jamii. Mutiso (1999:31), anasema kuwa shujaa huwa na safari katika maisha yake. Mutiso (khj), anaendelea kusema kuwa safari hii inaweza kuwa ya kisaikolojia, kiwakati au hata kimahali. Safari ya kisaikolojia ni safari ya kifikra pale ambapo shujaa anapojiwa na fikra fulani mpya labda kutokana na maadiliko ya kielimu ambayo huipitisha kwa jamii yake.

Jagina anapogura, huenda sehemu nyingine nje ya jamii yake. Sehemu hizi zinaweza kuwa nchi nyingine. Nje ya jamii yake, jagina hukumbana na mazingira mapya na ambayo huenda yakawa tofauti na ya jamii yake. Mazingira haya humpa mtazamo tofauti wa mambo. Ingawa jagina hupitia changamoto nyingi katika mazingira yake mapya, changamoto zile humnoa zaidi. Mara nyingi mashujaa wengi hurejea makwao baadaye ingawa kuna wale hugura na wasirejee. Kwa mfano, kulingana na maelezo ya Hemedi'l Ajjemy (1962), shujaa wa Wasambaa aliyeitwa Mbega hakurejea kwao Nguu baada ya kugura.

Kugura kwa Nabii isa hakujaelezwa kwa kina katika Utenzi wa Nabii Isa lakini katika Biblia kunadhihirika. Nabii Isa anapozaliwa, anakutana na njama ya kuuawa na mfalme Herode aliyehofia kunyang`anywa ufalme wake. Yusufu ambaye alikuwa babaye Isa alijiwa ndotoni na malaika wa Mungu aliyemwamrisha amchukue Isa na mamaye Maryam na wakimbilie nchi ya

Misri. Nabii Isa alikaa Misri hadi pale Mfalme Herode alipokufa ambapo walirejea kwao Galilaya. Kwa kawaida, jagina hugura misukosuko inapokuwa mingi.

Sunduata naye anagura baada ya Sogolon (mamaye Sundiata) kuhofia usalama wa wanawe chini ya uongozi wa Dankaran Touman na mamaye Saussoma. Wanapogura wanatua nchi baada ya nyingine. Mwandishi D. T. Niane anasema:

Miguu yao ilitifua vumbi la barabara.
Walipitia changamoto na matusi wayajuayo wakimbizi.
Walifungiwa milango na wafalme
waliwafukuza kutoka himaya zao.
Lakini haya yote yalikuwa sehemu
ya mustabali mkuu wa Sundiata. (uk. 28)

### 3.2.1 Majagina kwa Kawaida huwa ni Washairi

Aghalabu majagina huwa ni washairi. Washairi huwa na falsafa nzito kuihusu jamii. Mutiso (1999:21), anaeleza kuwa majagina ni washairi, wenye elimu (hata kama jagina hajasoma), wanafalsafa na wenye sifa za ubaya au za uzuri. Mutiso (khj), anasema kuwa ubaya wa jagina huonekana tu na mahasidi wake. Majagina wana sifa nyingine kama vile ujasiri, ujanja, akili pevu, ufadhili, ustahamilivu, urembo, usamehevu, ufasaha wa kunena miongoni mwa nyingine. Mashairi hukubalika katika jamii na hupitishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Mashairi yaliotungwa na majagina huchukuliwa kama zawadi na wanajamii na hudumu katika jamii ile hata baada ya kifo cha jagina.

Ingawa hatujapata shairi lolote lililotungwa na Nabii Isa, mafundisho yake yalikuwa na falsafa nzito. Alitumia hadithi na ngano katika mafundisho yake, jambo lililowafanya wafuasi wake kumwita mwalimu. Sundiata pia hakuwa mshairi lakini usemi wake vilevile ulisheheni falsafa nzito na alizungumza kwa mafumbo. Kuna vijisehemu alikuwa anatunga nyimbo kwa mfano, alipokuwa ametegewa mtego na mfalme wa Djedeba Mansa Konkon kupitia mchezo wa wori anaimba:

I don don, don don kokodji
Kitambo wageni walikuwa watakatifu.
I don don, don don kokodji

Lakini dhahabu ilikuja tu jana
Ilhali nilikuja kabla ya jana (uk. 38) (TY)

### 3.2.2 Maisha ya Shujaa huwa ni Dhiki Tupu

Shujaa huwa na dhima ya kuikomboa jamii yake kutokana na shida zinazoikumba. Shujaa huyu huwa hatulii mpaka pale atakapoona amelitimiza lengo lake. Jamii nayo huwa na matarajio yake kutoka kwa jagina wao na hivyo wanajamii hujaribu kumtia shime shujaa wao na kumkuza. Jambo hili humfanya shujaa kujitolea uhai wake na anaweza kufanya jambo lolote lile hata kama ni hatari ili aikomboe jamii yake.

Katika jitihada hizi za ukombozi, mashujaa wanapitia changamoto nyingi na wao hukumbana na mateso na upinzani mkubwa. Mateso wanayoyapitia ni kama vile, kusalitiwa, kudhulumiwa, kusingiziwa na wakati mwingine kuuawa. Maisha ya jagina kwa kawaida huwa ni dhiki tupu tangu kuzaliwa kwake hadi kufa kwao.

Kuzaliwa kwa Nabii Isa kulikuwa chini ya mtende. Mazingira haya si mazingira yafaayo ya kuzalia mtoto. Pia, katika Biblia, Isa alizaliwa katika hori la ng`ombe. Kuzaliwa kwa Nabii Isa katika mazingira haya ni ishara ya maisha ya dhiki ya jagina. Achieng (2012), anasema kuwa mashujaa hupitia shida nyingi katika maisha yao. Katika Utenzi wa Nabii Isa, Nabii Isa alikumbwa na shida nyingi. Kunao waliotofautiana naye kuhusu unabii wake, kuna wale walihitilafiana iwapo yeye alikuwa nabii au la. Wakati mwingine alipitia vipindi vya njaa pamoja na wanafunzi wake kwani hakuwa na maskani yake. Nabii Isa vile vile alisalitiwa na mwanafunzi wake.

Maisha ya Sundiata kama yalivyo ya majagina wengine yalikuwa yamejaa dhiki. Sundiata alipozaliwa, hakuweza kutembea hadi pale alipotimu miaka saba. Alikuwa na kichwa kilichoushinda mwili kukibeba. Walipitia matusi mengi na mamaye kutoka kwa mamake wa kambo kwa kutotembea kwake. Babake anaaga dunia Sundiata angali mchanga na mfalme Dankaran Touman ampokonya groit wake aliyeachiwa na babaye Maghan Konate. Misukosuko inakuwa mingi na wanagura kutoka kwa nchi yao. Ugenini wanapitia shida nyingi wanazozipitia wakimbizi kama vile kufukuzwa.

### 3.2.3. Maisha na Matendo ya Jagina huwa ni ya Kimiujiza.

Kulingana na Mdee na wenzake (2011), wanaueleza muujiza kama jambo lolote ambalo si la kawaida. Wanasema muujiza ni kioja, nduli, shali au dungudungu. Gathara (2012:16) naye anasema muujiza ni dhana ambayo ina sifa ya uhalisi ajabu. Wamitila (2003:274), anaelezea dhana ya uhalisi ajabu kama dhana iliyobuniwa na Mjerumani ambaye alikuwa msanii kwa jina Franz Roh. Wamitila (khj) anasema uhalisi ajabu huhusishwa na sifa zinazoelezea matukio ya kifantasia au kiuchawi ambayo kwa namna fulani yanaonekana kama ya kawaida. Anasema kuwa mpaka uliopo kati ya mambo ya kawaida yapatikanayo katika ulimwengu wa kawaida na ya yale yasokuwa ya kawaida (miujiza) huwa ni finyu sana.

Kuzaliwa kwa Nabii Isa na matendo yake yalikuwa yana uhalisia ajabu mwingi. Kuzaliwa kwa Nabii Isa kulikuwa ni kwa miujiza kwani alizaliwa bila baba. Jambo hili ni kinyume na matarajio ya wanajamii. (ubeti wa 588). Malaika wa Mungu alimvivia Maryam nguo ambapo alipata mimba ya Isa. Vile vile, Nabii Isa aliifanya miujiza mingi katika maisha yake. Aliwaponya vipofu (ubeti wa 422 na 425). Katika Biblia, muujiza huu umeangaziwa katika kitabu cha Mathayo 9:27-31.

Katika beti za 452, 472 katika Utenzi wa Nabii Isa, Nabii Isa aliwaumba ndege kwa kutumia udongo ambao alipowarusha juu angani walipaa. Jambo hili ni la kiuhalisi ajabu. Muujiza mwingine unajitokeza pale Nabii Isa alipomweleza mmoja wa hadhira yake juu ya chakula alichokuwa amekila wakati wa jioni na asubuhi, maji aliyokuwa ameyatumia, hela alizokuwa nazo mfukoni na akiba aliyokuwa nayo nyumbani. Huu ni muujiza uliowashangaa wengi pale ambapo mtu huyo alithibitisha kuwa aliyoyanena Nabii Isa ulikuwa ukweli. (beti 380-382). Nabii Isa pamoja na wanafunzi wake walipewa chakula jangwani baada ya kuomba. Chakula hiki kilikuwa kimeteremshwa na Allah S.W kutoka mbinguni, kilikuwa kinaitwa maida na mwandishi anasema kilikuwa kitamu sana, utamu ambao hungeweza kufananishwa na chakula kingine. (beti 746-761).

Maisha ya mfalme Sundiata yalikuwa yenye uhalisi ajabu. Kwa mfano, siku ya kuzaliwa kwake anga ilibadilika kutoka hali ya kiangazi na kukanyesha kighafla. Na punde tu kitoto kilipozaliwa, anga ikarudi tu vile ilivyokuwa awali. Hili ni jambo la kimiujiza. Siku ya Sundiata ya kutembea, kujiinua ili kusimama alikipinda chuma kikubwa ambacho kilikuwa kimebebwa na watu sita (uk.

20-21). Vilevile, kutembea kwake kulikuwa ni kama kwa jitu kwani hatua zake ziliitikisa ardhi kwa kishindo. (uk. 21).

### 3.2.4 Majagina huwa Hawaeleweki kwa Uwazi.

Kila jamii humuumba jagina wao kwa kumkuza. Katika kumkuza jagina, jamii ina uhuru wa kumuumba watakavyo. Mara nyingi jamii humlimbikizia sifa nyingi ambazo wakati mwingi zimetiwa chumvi. Kama tulivyoona hapo awali, jagina huwa na maadui. Maadui wa jamii humtolea sifa ambazo ni hasi. Huku kusawiriwa tofauti tofauti na wanajamii humpa shujaa sifa ya kutoeleweka kwa uwazi.

Nabii Isa hakueleweka vyema na jamii ya Wayahudi. Wayahudi walitarajia wapate shujaa ambaye ni amri jeshi mkuu, watakaye enda naye vitani na atakayewakomboa kutoka kwa utawala wa Warumi ambao walikuwa wamewasumbua kwa miaka mingi. Nabii Isa alipowajia, alikuwa wa vita vya kiroho. Ingawa alionekana kuwatatulia shida zao, kwao hakueleweka kwa uwazi kwani wakati mwingine alikuwa akiwacharaza alipowakuta hekaluni wakifanyia biashara ndani.

Sundiata ambaye alikuwa ametabiriwa kama kiongozi atakayekuwa mkuu hata kumshinda Alexander the Great, alizaliwa na ulemavu. Jambo hili lilionekana kuwakanganya Wamandingo. Maumbile yake vilevile yalikuwa yanaleta kutoeleweka vyema na jamii kwani alikuwa na kichwa kikubwa ambacho mwili wake ulishindwa kukibeba. Kwa kawaida, mwana wa kiume wa kwanza ndiye aliyekuwa anaurithi uongozi wa babaye na Sundiata hakuwa wa kwanza wa mfalme Maghan Konate. Baada ya kifo cha Maghan, kakake Dankaran Touman alichukua usukani na hivyo kuwa mfalme kwa Sundiata lilikuwa jambo ngumu. Sundiata hakueleweka kwa uwazi na jamii yake ya Mali.

### 3.2.5 Mapenzi ya Mama Mzazi kwa Shujaa.

Kunazo dhana za kisaikolojia ambazo ni Oedipal complex na Electra complex. Dhana hizi zina maana kuwa mtoto mvulana huwa anavutiwa kimapenzi na mzazi wake wa kike (Oedipal complex) na mtoto wa kike huvutiwa kimapenzi na baba yake (Electra Complex). Shujaa kwa kawaida huwa kipenzi cha mamaye. Kunayo mengi ambayo huwa siri kati ya shujaa na mama

yake. Aghalabu ni mama anayemtuliza mwanaye (jagina) misukosuko inapokuwa mingi. Vilevile, mama atamhimiza mwanaye katika jambo lolote gumu analolipitia au kulifanya.

Nabii Isa alikuwa rafiki wa karibu na mamaye Maryam. Nabii Isa akiwa angali mchanga, alizungumza kumwondolea mamaye lawama kutoka kwa wanajamii. Katika Biblia, kunao muujiza wa kwanza alioufanya Nabii Isa wa kubadilisha maji kuwa divai katika mji wa Kana, Galilaya. Mamaye alipoona divai imepungua, alimshinikiza mwanawe kuutenda ule muujiza. Baada ya kifo cha Isa pale msalabani, mamaye Maryam alikuwa mmojawapo wa waliokuwa wakiomboleza. Baada ya kuzaliwa kwa Nabii Isa, alizungumza angali kitandani, jambo ambalo lilimwondolea lawama mamake Maryam. (Ubeti 178-179)

Sundiata alikuwa kipenzi cha mamaye Sogolon tangu kuzaliwa kwake. Ingawa Sundiata alikuwa na ulemavu na alitembea baada ya miaka saba, mamaye hakumtupa au kumtelekeza mwanaye. Hatua za kwanza za Sundiata zilisababishwa na huruma aliomwonea mama yake alipotukanwa na mamaye wa kambo Saussoma. Mara nyingi mamaye Sundiata alimlinda kwa kumwosia ya kutenda. Wazo la kugura kwao lilikuwa la mamaye Sundiata. Vilevile alimhimiza Sundiata kwa mengi kama vile katika kutotembea kwake, Sogolon alimpa moyo kuwa siku moja atakuwa mfalme. Hili ni dhihirisho kuwa Sundiata alikuwa kipenzi cha mamaye.

### 3.2.6 Kimo na Nguvu za Jagina

Majagina wengi huwa na vimo vya kiajabu. Wanaweza kuwa majitu makubwa yenye vimo virefu na nguvu nyingi au wawe wenye vimo vifupi kuliko vya kawaida. Mutiso (1999:12) anaeleza ya kuwa jagina anaweza kuzaliwa na ulemavu. Ulemavu huu ni onyo kuwa mtu huyu si kiumbe tu wa kawaida kwani uwezekano ni kuwa atakuja kuwa na nguvu nyingi sana baadaye. Jagina awe na kimo kirefu au kifupi, yeye huwastaajabisha wanajamii.

Nabii Isa alikuwa na kimo cha wastani. Hakuwa na nguvu za kimwili bali alikuwa na nguvu za kiroho. Alikuwa anafanya mambo makuu kama vile kutumia udongo kuumba ndege waliopata uhai na kuruka juu angani. Sundiata alikuwa na kimo kifupi lakini alikuwa na nguvu zisizo za kawaida. Siku yake ya kwanza kusimama na kuchukua hatua za kwanza, alitumia chuma ambacho kilikuwa kimebebwa na watu sita kujisaidia kusimama. Chuma kile kilipinda, dalili ya nguvu

alizokuwa nazo. Siku ya kwanza kutembea, aliung'oa mbuyu mzima na kuubeba, kumletea mamake majani ya mbuyu. Mwandishi Niane vilevile anasema kuwa hakuna aliyeweza kuuvuta uta wa Sundiata kufuma. Hii ni ishara kuwa alikuwa na nguvu nyingi, zisizokuwa za kawaida.

**3.2.7 Mashujaa mara nyingi huwa Magwiji Vitani**

Lengo la mashujaa huwa ni kuzikomboa jamii zao kutoka kwa maadui zao. Majagina aghalabu huwa na mioyo thabiti na huwa hawana uoga na wanaweza kukabiliana na lolote. Vitani, majagina huwa magwiji na wanapoziongoza jamii zao katika vita, ndipo ujagina wao hudhihirika. Majagina wengi huwa mashujaa wa kivita kwa mfano, Fumo Liyongo, Lwanda Magere, Shaka Zulu, Dedan Kimanthi, Samson wa Bibilia miongoni mwa wengine.

Kinyume na majagina wengine, Nabii Isa hakutumia nguvu za kimwili katika kukabiliana na maadui wa jamii yake. Hili halionyeshi kuwa hakuwa jasiri kwani alipambana na mahasidi wake katika vita vya kiroho. Sundiata alikuwa gwiji vitani. Alipigana vita na mfalme wa Sosso Soumaoro Kante na kuikokomboa nchi yake ya Mali.

**3.2.8 Jagina na Suala la Ndoa**

Majagina kwa kawaida hawaoi na pale ambapo wataoa, hawataitia maanani ndoa ile. Lengo la jagina kama tulivyotanguliza kusema ni kuikomboa jamii kutoka kwa maadui. Hivyo maisha ya jagina huwa si ya kutulia mahali pamoja na huwa na misukosuko mingi. Jagina kwa kawaida huwa hana muda wa kutosha wa kushughulikia ndoa. Ndoa vilevile huwa na mahitaji yake ambayo wakati mwingine hayawezi kumpa jagina uhuru wa kutekeleza lengo lake. Kwa kawaida, jagina 'huoa' jamii.

Mashujaa ambao huoa kwa kawaida huwa na ndoa isiyokuwa thabiti. Mifano ya mashujaa waliooa ni kama vile, Fumo Liyongo, Lwanda Magere, Dedan Kimanthi miongoni mwa wengine. Nabii Isa hakuoa na wala hakuwa na watoto lakini Sundiata alioa na kupata Watoto. Alimrithisha mwanawe wa kwanza aliyeitwa Wala ufalme wake.

**3.2.9 Kifuasi cha Jagina**

Vifuasi vya jagina huwa ni vitu vyovyote vile jagina huandamana navyo na ambavyo humsaidia katika kazi yake. Vifuasi vinaweza kuwa, mtu, mti, mnyama kama vile mbwa, jiwe, kijana, dhana

fulani, mdudu miongoni mwa vingine. Mwanamke pia anaweza kuwa kifuasi cha jagina ingawa wengi huwa wapelelezi waliotumwa na maadui wa jagina. Majagina wengi huandamana na vifuasi vyao na huwa ni muhimu kwani huwa kama wasaidizi wa shujaa. Katika jamii, vifuasi huwa maana tofauti tofauti. Kuna vile vya kiuchawi kama hirizi na kuna vingine huambatanishwa na vyeo kama fimbo. Maana hizi huwa akilini mwa wanajamii.

Jagina Musa katika Bibilia alikuwa shujaa wa Waisraeli alikuwa na kifuasi chake aina ya kijiti. Musa alitumia kifuasi hiki katika kuitenda miujiza kama vile, kiligeuka na kuwa nyoka. (Kutoka 4:1-5). Werner (1968:133) anatoa maelezo kuhusu kifuasi cha shujaa wa jamii ya Wasambaa aliyeitwa Mbega. Mbega alikuwa anatembea na mbwa wengi na kati ya mbwa hao kuna mmoja aliyemwita ‘Chamfuu’ ambaye aliandamana naye kila mahali. ‘Chamfuu’ alikuwa akimsaidia katika kazi yake ya uwindaji wa nguruwe na wanyama wengineyo.

Fumo Liyongo alikuwa na kifuasi cha mkoba kilichokuwa kinabeba mishale na vitu vinginevyo vya vita. Nabii isa alikuwa na kifuasi cha wanafunzi wake ambao aliandamana nao popote alipoenda na hata wakati anaposalitiwa alikuwa pamoja nao. (Ubeti 785-790). Kulingana na Biblia, Nabii Isa vilevile alikuwa na kifuasi cha Roho mtakatifu aliyemwezesha kutenda miujiza. (Luka 3:22). Sundiata alikuwa na kifuasi cha kakake Manding Bory aliyekuwa akimsaidia kwa mambo mengi. Vilevile alikuwa akiubeba uta wake popote alipoenda.

### 3.3 Jagina huwa wa Jamii Nyingi

Shujaa kwa kawaida huwa na jamii yake mahususi alikozaliwa lakini matendo yake makuu na ya kimiujiza humpa sifa na umaarufu na basi kumpa sifa ya jagina wa jamii nyingi. Hii ni kwa sababu jamii nyingi humtambua kama jagina wao. Kwa mfano, majagina wa kidini huwa majagina wa jamii nyingi. Mtume Muhammad ni jagina wa Waislamu wote duniani. Buddha ni jagina wa Wahindu wote duniani. Yesu Kristo ni shujaa wa Wakristo wote duniani.

Fumo Liyongo alikuwa jagina wa Waswahili, jamii kama vile Wabajuni, Wasegeju na Wapokomo hudai kuwa alikuwa shujaa wao. Nabii Isa ni jagina wa jamii pana kwani hakuna jamii isiyomjua hata wasiofuata mafundisho yake. Kwa mfano sherehe ya Krismasi inayosheherekewa duniani karibu yote ni ithibati kuwa Isa ni jagina wa jamii pana (jamii nyingi). Sundiata alikuwa jagina wa

jamii ya Mali lakini popote historia ya Afrika inapotajwa, Sundiata ni jina ambalo halitakosekana katika historia ile. Sundiata hivyo basi ni jagina wa jamii za Afrika Magharibi.

### 3.3.1 Usaliti na Kifo cha Jagina

Jagina kwa kawaida huwa shupavu, mwenye nguvu nyingi na mwenye matendo ya kimiujiza. Kushindwa na kuanguka kwa shujaa si jambo rahisi. Usaliti ni njia itumiwayo mara nyingi na maadui kama silaha ya kumwangamiza jagina. Kunao majagina wengi wanaoangushwa kwa kusalitiwa kwa mfano, Samson katika Bibilia aliyesalitiwa na mwanamke Delila. Fumo liyongo alisalitiwa na mwanawe, Lwanda Magere pia alisalitiwa miongoni mwa wengine.

Katika njama yoyote ya usaliti, usaliti huo huwa na pande mbili, yaani kunaye anayepata manufaa kutokana na usaliti wenyewe na kuna yule anayepata hasara. Motifu ya dhambi pia hujitokeza pale jagina anaposalitiwa kwani anayetumiwa kumsaliti jagina pia naye huvikwa na makuu na hili huashiria kati ya mapigano ya wema na ubaya, wema kila wakati hushinda. Vilevile katika usaliti wa jagina, jagina huonyeshwa kudhurika na kitu kimoja au hali moja tu ya kipekee. Kwa mfano, Samson wa Bibilia angedhurika tu na kunyolewa nywele za kichwani, Fumo Liyongo angedhurika na kudungwa sindano ya shaba kitovuni na wala si sindano ya aina nyingine.

Usaliti katika Utenzi wa Nabii Isa unaonekana pale mmoja wa wafuasi waliokula nao na kushirikiana kwa mambo mengi, mmoja wao ndiye aliyemsaliti kwa wahalifu waliopanga njama ya kumuua ingawa Mungu anamwepushia hilo kwa kumleta mtu mwingine waliofanana kisura na Nabii Isa aliyesulubiwa na kumpaisha Isa mbinguni (Ubeti wa 785-790). Kifo cha Sundiata hakijaangaziwa kwa kina na groit Mamoudou Kouyate labda hii ni kwa sababu ilikuwa mwiko katika jamii ya Mandinka kuzungumzia vifo vya wafalme wao. Hata hivyo, Sundiata alisemekana kuzama mtoni Sangarani karibu na mji wa Niani alipokuwa anauvuka kwani historia inasema kuwa paliwekwa madhabahu ambayo hata leo yamesimama pale.

Majagina huamini kuwa hawawezi kudhurika au hata kufa. Wao huamini wataishi milele. Haya ni kwa mujibu wa Mutiso (1999:37) Mutiso anaendelea kusema ya kuwa majagina hutafuta visingizio vya vifo vyao. Wao husema kuwa vifo vyao vilikuwa vimetabiriwa au wanajitolea kufa ili wazikomboe jamii zao. Kwa mfano, Wakristo husema kifo cha Isa kilikuwa kimetabiriwa kwani

baada ya wanadamu kuanguka dhambini Mungu aliamua kuwarudia lakini ni Yuda Iskarioti aliyesababisha kifo cha Isa.

Yuda Iskairoti alimsaliti Isa kwa kupewa ahadi ya vipande thelathini vya fedha. Yuda alikuwa ambusu Isa ili amtambulishe kwa Wayahudi, Mafarisayo na Waandishi, waliomkamata na kumsulubisha Yesu. Yesu alipokufa msalabani, kifo chake kilichukuliwa kama malipo ya dhambi za jamii ya Wakristo na kuwa yeyote amfuataye Yesu atakuwa na uzima wa milele. Kifo ni kikale ambacho huwa akilini mwa wanajamii kuwa ndiyo njia ya kuvuka upande ule mwingine baada ya ulimwengu huu.

### 3.3.2 Kurudi kwa Jagina katika Safari ya Mwisho

Jagina anapokufa, huwa ni pigo kubwa kwa jamii yake. Wanajamii huomboleza kwa kumpoteza shujaa wao. Kwa mujibu wa Bibilia, Isa alipokufa, wanafunzi wake walisikitika sana hata kujifungia chumbani ambapo waliongea kwa sauti ya chini. Nabii Isa alikuwa jagina wa kidini. Mutiso (1999:39), anasema kwamba jagina wa kidini kwa kawaida katika mafundisho yake huwa kuna ulimwengu mwingine baada ya kifo. Anaendelea kudai kuwa, katika ulimwengu huo mwingine, jagina wa kidini hueleza kuwa waliotenda mambo mema ndio watakaoenda ulimwengu huo baada ya kifo. Katika ulimwengu huo wa pili hakuna dhiki, taabu, magonjwa wala kifo ila shibe na furaha.

Mutiso (khj), anasema kuwa ulimwengu huo una majina kulingana na jamii. Kulingana na dini ya Usiva unaitwa Kilaisa, Waislamu wanauita Peponi nao Wakristo wanauita Mbinguni. Anaendelea kusema kuwa, katika ulimwengu huu ndio makao ya Mungu, miungu na mashujaa. Mutiso (khj) anasema kuwa ni Mungu, majagina na miungu pekee wanaoweza kufika huko na wanaotenda mema watafika huko tu siku ya mwisho.

Majagina wa kidini wakifa (ingawa jamii huamini kuwa hawafi), wao huenda katika ulimwengu huu mwingine na kuwa atarudi ulimwengu huu tunaoishi kuwachukua na kuwaongoza waliozitii sheria zake katika ulimwengu huo wa pili wenye raha na shibe. Vivile atarudi kuwahukumu wale ambao hawakutii sheria zake. Hii ndio safari ya mwisho ya jagina. Akija anatarajiwa kuwafufua wafu na kuwaadhibu waasi.

Jamii za Wakristo na Waislamu huamini ya kwamba Isa atarudi tena ulimwenguni ili kuikamilisha kazi yake. Wakristo huamini jagina Isa yu Mbinguni na amekaa katika upande wa kuume wa Mwenyezi Mungu na ya kwamba, atarudi katika safari yake ya kuwachukua walio wake ili wakaishi naye maisha ya raha mustarehe. Walioasi mafundisho yake watapelekwa jehanamu kwenye moto wa milele. Jagina Sundiata hakuwa jagina wa kidini bali ni wa kiutamaduni. Baada ya kifo chake, masimulizi ni kuhusu matendo aliyoyatenda akiwa hai na wala hatujapata habari zozote kumhusu baada ya kifo chake.

Kutokana na ulinganisho tulioufanya hapo juu, kunazo tofauti za sifa za kijagina kati ya Nabii Isa na Sundiata nazo ni pamoja na: jagina kuwa mshairi, kimo na nguvu za jagina, jagina kuwa gwiji vitani, jagina na swala la ndoa, usaliti na kifo cha jagina na kurudi kwa jagina katika safari ya mwisho. Kama tulivyotanguliza kueleza kuwa ushujaa ni mojawapo wa vikale katika jamii, tofauti zilizopo kati ya sifa za kijagina kati ya Nabii Isa na Sundiata huenda zimetokana na mazingira ya jamii zilizowazaa na mila na desturi za jamii hizo. Mutiso (1999), anapoeleza aina tatu za majagina, aina moja ni kiumbe aliye wa ukweli, aliyekuzwa na jamii na pia kujikuza mwenyewe na hivyo Nabii Isa na Sundiata ni mifano ya aina hii ya jagina. Tofauti zao chache zinaweza kutokana na jamii na mazingira yaliyowakuza.

### 3.4 Hitimisho

Mambo tuliyoyaangazia katika sura hii ni kuzilinganisha sifa za shujaa Nabii Isa na zile za shujaa Sundiata. Katika ulinganifu huu, mfanano wa sifa zao ni pamoja na: kuzaliwa kwao kulitabiriwa, wote walikuwa wanaume, majagina hawa walitoka katika ukoo wa kifalme, wote walikuwa na maadui, walikuwa vipenzi vya jamii zao, walikuwa na majina mengi ya kuwasifu, walikuwa na akili pevu, maisha yao yalikuwa yenye dhiki tupu, walikuwa majagina wa jamii nyingi (pana), hawakueleweka kwa uwazi, walikuwa na vifuasi vilivyowasaidia katika kazi zao na akina mama zao walikuwa na mapenzi kwao.

Majagina Nabii Isa na Sundiata vilevile walitofautiana kwa sifa chache zifuatazo: Sundiata alizaliwa akiwa na ulemavu lakini Nabii Isa hakuwa na ulemavu. Ingawa majagina takriban wote huwa na ulemavu ambao mara nyingi hauonekani, katika kazi hii yetu tuliangazia ulemavu

unaoonekana kwa macho ya mwanadamu. Sundiata alikuwa mwenye nguvu za kimwili lakini Nabii Isa alikuwa na nguvu za kiroho. Utoto wa Sundiata umeangaziwa sana kuliko wa Nabii Isa. Sundiata alioa na akapata watoto lakini hatujapata habari zozote kuhusu ndoa ya Nabii Isa wala kupata wayoto kwake.

Sundiata alikufa na wala hatujapata ushahidi wowote wa kufufuka kwake. Nabii Isa hakufa bali alipaishwa juu mbinguni na Mwenyezi Mungu (kwa mujibu wa Utenzi wa Nabii Isa) na kwa mujibu wa Bibilia, Isa alikufa na siku ya tatu akafufuka na kupaa mbinguni (Marko 16:1-14). Waumini wanaamini kuwa Isa atarudi katika safari ya mwisho kutoa hukumu ya mwisho ambapo walioyafuata mafundisho yake wataenda naye mbinguni wakaishi maisha ya milele na walioyaasi mafundisho yake watapelekwa jehanamu.

# SURA YA NNE

# UMUHIMU WA NABII ISA NA SUNDIATA KWA JAMII ZAO.

## 4.0 Utangulizi

Majagina hupewa nafasi kubwa sana katika jamii zao kwani ujagina ni mojawapo ya asasi katika jamii kama tulivyotanguliza kuelezea. Kwa kawaida, jamii humtegemea pakubwa jagina wao. Kufikia hapa katika utafiti wetu, tumeziangazia sifa bia za mashujaa kwa kuwarejelea majagina Nabii Isa na Sundiata. Tumekwisha kuielezea historia yao na hivyo basi itatubidi kupiga hatua mbele na kuelezea umuhimu wa majagina hawa katika jamii zao na katika jamii pana (ulimwengu wote) kwa jumla.

Kama tulivyoelezea, jamii huwa ni mfumo ulio na mifumo au taasisi nyingine ndogondogo ndani yake. Taasisi hizi ndogondogo huwa na uamilifu wake ambapo kila taasisi huingiliana na kukamilishana ili kuunda jamii iliyokamilika. Ujagina kama taasisi katika jamii huwa na lengo haswa la kuleta mabadiliko chanya katika jamii. Majagina husawazisha hali fulani katika jamii na aghalabu huchukua nafasi kubwa sana katika jamii. Uamilifu wa ujagina huwa ni kuubadilisha mfumo wote wa jamii kwa manufaa ya jamii nzima. Katika sura hii, tunaangazia umuhimu wa Nabii Isa na Sundiata kwa jamii zao.

### 4.1.1 Historia ya Jamii/Kioo cha Jamii

Jagina aghalabu kwake huwa kumesitiriwa historia ya jamii. Majagina huwa kama kiunzi ambapo maelezo kuihusu historia ya jamii huandikwa. Hali zote zinazoikumba jamii huonekana katika dhiki zote anazozipitia jagina. Kwa kuiangazia na kuielewa historia ya jagina wa jamii fulani, tunaweza kupata picha ya mfumo wa ile jamii. Maisha ya jagina tangu kuzaliwa, kukua, dhiki anazozitipia hadi kifo chake ni taswira nzuri ya hali ilivyo katika mfumo wa ile jamii. Mifumo kama vile utamaduni, siasa, uchumi miongoni mwa mingine hudhihirika baada ya kuangazia maisha ya jagina wa jamii hiyo. Tunaweza kusema kuwa jagina ni kioo cha jamii kama ilivyo fasihi. Katika kipindi ambacho jagina huzuka na kuwa mwanajamii wa jamii ile, yeye huwa kiwakilishi cha ile jamii. Kwa kuangazia maisha ya jamii ile kabla ya kuzaliwa kwake, wakati wa kuishi kwake na ukombozi anaouleta hadi kifo chake, husaidia katika kuielewa ile jamii na historia yake.

Katika kuangazia historia na sifa za Nabii Isa na Sundiata, tumeweza kuhakiki jamii ya Wayahudi na ya Wamali. Kwa kuangazia maisha yao, tumeelewa kuwa jamii hizi mbili zilikumbwa na misukosuko ya dini, uongozi, uchumi, utamaduni miongoni mwa mingine. Kunazo nyimbo na mashairi yaliyotungwa kuwasifia mashujaa hawa na nyimbo hizi zimetusawiria mazingira yaliyowazaa majagina hawa. Kwa mfano, kunavyo vifaa na vyakula vingi vilivyotajwa kama vile nyungu, udongo, nyuta na mishale, vyakula kama mchele, tende na vilevile mashamba ya mboga, majani ya mbuyu na mengine mengi kwenye yale mazingira.

Kwa kawaida, jagina huleta mabadiliko katika jamii na hivyo ni dhahiri kuwa asasi fulani katika jamii inaweza kubadilika. Utamaduni hivyo basi, ni asasi inayoweza kubadilika kutokana na mambo mengi kama vile mpito wa wakati, vipindi mbalimbali, elimu, dini na hata kutokana na mlandano wa jamii na jamii nyingine. Jagina huwa na nafasi kubwa ya kuleta mabadiliko katika jamii yake jinsi apendavyo. Hili ni kwa sababu, jamii humpa hadhi ya juu na kumkuza.

Mbali na kuzikomboa jamii zao, majagina Nabii Isa na Sundiata waliyaleta mabadiliko mengi hasa katika asasi ya utamaduni wa jamii zao. Waliikuza imani ya wanajamii kwa kuwa watetezi wao. Kwa mfano, Nabii Isa alikuwa na mafundisho mengi yaliyobadilisha mila na desturi za wanajamii wake. Alikuwa kielelezo kwa ulimwengu mzima. Kama jagina wa kidini, anaenziwa na Waislamu na Wakristo ambao ni wanajamii wa dini mbili zilizo na wanajamii (wafuasi) wengi sana duniani. Sundiata alileta utangamano katika nchi ya Mali na ushirikiano wa Mali na nchi nyingine.

### 4.1.2 Kitambulisho cha Jamii

Jagina huitambulisha jamii yake. Jagina huwa kiunzi katika mfumo mzima wa jamii yake. Ujagina huwa taasisi kuu katika mfumo mzima wa jamii. Jina la jagina likitajwa tu huwa linarejelea jamii nzima iliyomzaa jagina huyo. Jina la jagina likiondolewa katika jamii fulani, basi jamii hiyo hubaki bila utambulisho wake na hata huenda isijulikane. Wakristo wanajulikana kote ulimwenguni kwa sababu ya jagina wao Nabii Isa. Vilevile, jamii ya Afrika Magharibi ina utambulisho wake kutoka kwa himaya ya Mali. Nayo himaya ya Mali utambulisho wayo ni jagina Mfalme Sundiata. Mfumo wote wa jamii hujulikana kutokana na jina la jagina wao.

Nabii Isa ana umuhimu mkubwa sana katika kuitambulisha jamii yake. Jamii ya Wakristo, jina lake ni kitambulisho cha jamii yake. Jina la Nabii Isa bado linaathiri nyoyo na nafsi za wanajamii wake pakubwa. Hata hivyo, kunao wanajamii waliokuwa maadui zake na walidai kuwa alikufuru kujiita 'mwana wa Mungu' lakini wafuasi wake humchukulia ni Masihi na Mkombozi wao. Kulingana na Utenzi wa Nabii Isa, mwandishi hajamsawiri Nabii Isa kama Mungu bali anasema kuwa alikuwa na Imani katika dini na hivyo aliubiri na kutenda miujiza kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu (beti 320-527).

Kunao wahusika katika jamii ambao huzitambulisha jamii zao. Kwa mfano majagina. Shujaa ni kikale katika jamii. Jamii huwaenzi mashujaa wao na kujitambulisha nao.

### 4.1.3 Mabadiliko katika Mfumo wa Jamii.

Jagina huleta mabadiliko katika mfumo wa jamii yake. Hili hufanyika baada ya kuikomboa jamii yake. Baada ya ukombozi, jagina huweka msingi wa kuleta mabadiliko na hivyo huwa na mikakati mwafaka ya kuyaleta mabadiliko hayo. Kanuni zilizowakandamiza wanajamii huziondoa na kuleta nyingine mpya. Baadhi ya mabadiliko anayoyaleta jagina katika jamii yake ni pamoja na sheria, mabadiliko katika vita, mahusiano na maingiliano na jamii nyingine, kuzalisha mali, dini, biashara miongoni mwa nyingine.

Nabii Isa aliziondoa sheria zilizowakandamiza watu kwa mfano kutoza ushuru kusiko na kiasi kwa mfano katika kisa cha Zakayo katika Bibilia (Luka 19:1-10). Kutochukua sheria mikononi ni mabadiliko mengine aliyoyaleta kwa mfano kisa cha yule mwanamke sherati (Yohana 8:1-11). Mabadiliko mengine aliyoyaleta Nabii Isa katika jamii ya Wayahudi ni kama vile elimu, usamehevu, huruma, uvumilivu, utu na dhana ya watoto.

Katika Utenzi wa Nabii Isa, sheria za maadili katika jamii zimepewa kipaumbele. Mwandishi ameyaonyesha maadili kuwa ndio msingi wa maisha ya wanajamii. Maryam alilelewa kwa maadili na Zakaria na kumwelekeza katika kuabudu msikitini (ubeti 87). Nabii Isa naye alionyesha uadilifu katika kuendeleza dini kwa kuhubiri mahakamani na misikitini. Sheria ni mojawapo ya vikale vya kianthropomofia katika jamii. Katika akililaza ya mwanajamii huwa kumehifadhiwa mema na maovu katika jamii.

Sundiata aliyaleta mabadiliko katika jamii yake ya Wamali. Aliwaunganisha wanajamii na alileta mahusiano mema ya jamii yake na jamii nyingine. Aliimarisha biashara, aliwaunganisha wajamii katika vita, aliondoa mfumo wa kuwanyanyasa wanyonge katika jamii na kuimarisha elimu katika jamii ya Wamali. Katika pilkapilka za jagina kuleta mabadiliko katika jamii yake, kunao wasiomuunga mkono kwani jagina kila wakati huwa na wanaopinga mawazo yake. Nabii Isa na Sundiata ni majagina walioleta mabadiliko katika mfumo wa jamii zao na mabadiliko haya yalileta umoja katika jamii.

### 4.1.4 Ukombozi na Muungano wa Jamii

Jamii hukumbwa na matatizo na shida fulani katika kipindi na hali fulani. Shida zinazoikumba jamii yoyote ile ni pamoja na uongozi au utawala mbaya, kuvamiwa na maadui, matatizo ya kiuchumi, kunyanyaswa kwa maskini au wanyonge, dhuluma za kijinsia, ukabila, njaa na ukame, ukosefu wa usalama, mapambano au vita vya kidini miongoni mwa matatizo mengineyo.

Majagina huwa wanazuka katika kipindi na hali fulani katika jamii zao. Majagina hawazuki katika ombwe tupu kwani wao huzuka katika jamii zao kwa lengo la kuzikomboa jamii zao dhidi ya misukosuko fulani katika kipindi kile. Jagina anapozuka katika jamii kama tulivyosema hapo juu, huyaleta mabadiliko. Katika mabadiliko haya, jagina huielekeza jamii yake katika mambo mengi kama vile ya kidini, kivita, kiuchumi, kielimu, kiafya, muungano na amani miongoni mwa mengine. Huenda ikawa jagina asipozuka katika kipindi kile, jamii yake ingebakia na misukosuko na shida yazo.

Kulingana na Utenzi wa Nabii Isa, Nabii Isa alinusuriwa na Mwenyezi Mungu baada ya kusalitiwa pale alipompaisha mbinguni. Jamii ya Waislamu huamini ya kuwa Nabii Isa atarudi tena duniani katika safari yake ya mwisho kuimalizia kazi yake aliyoianzisha ya kuikomboa jamii yake. Wakristo nao huamini kuwa Nabii Isa atarudi ulimwenguni mara ya pili kuwachukua wapae naye mbinguni kwani aliwakomboa alipokufa msalabani. Kulingana nao, kifo chake msalabani kutawawezesha kuurithi ufalme wa mbinguni usiokuwa na kikomo. Hivyo basi jagina huchukuliwa kama hidaya kutoka kwa Mwenyezi Mungu iliyo na kazi ya kuikimboa jamii. Kwa

kawaida, majagina huabudiwa hata baada ya kifo chao kwani ni zawadi inayoenziwa sana na wanajamii.

Sundiata kulingana na kisa cha Niane D. T, huaminika kuwa mwanzilishi wa himaya ya Mali na kiongozi au mfalme aliyeleta muungano katika jamii hiyo. Aliyaunganisha mataifa ya Afrika magharibi kwani panapotajwa historia ya Afrika Magharibi, jina la Sundiata halikosekani. Sundiata hukumbukwa hata baada ya kifo chake kama shujaa aliyeijenga himaya kubwa kabisa katika eneo la Afrika Magharibi.

### 4.1.5 Fahari ya Jamii

Huwa ni jambo la kuridhisha mtu moyo anapokionea fahari kilicho chake. Uwezo ilio nao jamii huipa fahari kuwa hata jamii yenyewe inatambulikana katika ramani ya eneo fulani au ya ulimwengu. Kuna mambo mengi ambayo kwayo jamii hujivunia. Jambo kuu mno ni kule kujivunia jagina au majagina wake. Jagina anapoutekeleza wajibu wake wa kuikomboa jamii ifaavyo, basi yeye huenziwa na kuonewa fahari na jamii yake katika maisha yake na hata baada ya kifo chake. Kazi na matendo yake hukumbukwa dahari.

Katika sura ya kwanza tulitoa maelezo kuwa kila jamii huwa na majagina wake. Jamii huwakuza majagina wao kufikia mwonekano wa kuwa wao si watu wa kawaida. Jamii huwaonea fahari majagina wake. Kazi anayoitenda jagina katika jamii yake aghalabu hufurahiwa na wanajamii wake na hili humpa jagina sifa ya kukumbukwa milele. Jamii humtungia jagina wake nyimbo, mashairi hata hadithi ambazo hupitishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Jamii nyingine huwa na walimu ambao kazi yao kuu ni kuupitisha utamaduni wao kwa vizazi vya baadaye na dhana ya ujagina ni kuu sana katika utamaduni wowote ule. Kwa mfano katika jamii ya Wamali, kulikuweko walimu walioitwa groit waliokuwa wanaifunza jamii historia yao na ya majagina wao.

Katika bara la Afrika, wakoloni waliichukulia jamii hii kama jamii isiyostaarabika na yenye tamaduni za kishenzi lakini kwa kuitazama dhana hii ya ujagina, waafrika walikuwa na mifumo bora ya uongozi wao kwani walikuwa na majagina waliowaenzi na waliokuwa na uwezo mkubwa wa kuleta mabadiliko yafaayo katika nchi zao. Majagina wa kihistoria wakiwemo Nabii Isa na Sundiata walikuwa na uwezo wa kuzipanua jamii zao, kuleta utangamano katika jamii zao,

mipangilio inayofaa ya kivita, uimarishaji wa dini katika jamii zao, ulinzi wa wanajamii miongoni mwa mikakati mingine.

Waafrika waliionea fahari jamii yao. Walipenda kujinasibisha na majagina wao na kuzionea fahari tamaduni zao. Waliamini kuwa tamaduni zao zilikuwa zimepigwa msasa na majagina wao wakati wa kuyaleta mabadiliko katika jamii. Kwa mujibu wa Kenyatta (1922), Waafrika walikuwa na mfumo faafu wa uongozi kama vile, uzalishaji mali, uamuzi wa kesi, utozaji kodi, njia za kuabudu, katika ndoa, kupasha tohara, kuhifadhi misitu na wanyama, njia za mazishi miongoni mwa tamaduni nyingine. Majagina hivyo basi walikuwa fahari ya jamii zao. Nabii Isa na Sundiata walikuwa fahari ya jamii zao za Wayahudi na Wamali mtawalia.

### 4.1.6 Mfano Bora wa Kufuatwa na Jamii

Majagina kwa kawaida huwa watu shupavu wanaojitolea kuzitumikia jamii zao na kila mara huwa tayari kuhatarisha maisha yao kwa faida za wanajamii. Majagina huwa na mapenzi sana kwa jamii zao na kila mara jamii hupenda kujinasibisha na majagina wake. Majagina vilevile huacha alama katika maisha ya mwanajamii kwa kuathiri jinsi anavyotazama na kuyachukulia mambo. Aghalabu mwanajamii hubadilisha mtazamo wake kuhusu jambo fulani baada ya kuvutiwa na matendo ya jagina wao.

Sifa za jagina pamoja na matendo yake hupitishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine kama tulivyoeleza katika hoja tangulizi. Matendo na sifa za shujaa hupitishwa kwa vizazi vya baadaye kupitia kwa hadithi, masimulizi, maandishi, filamu, nyimbo na hata mashairi. Mashujaa hivyo basi huwa ruwaza bora kwa wanajamii waliopo na wa baadaye.

### 4.1.7 Ukuzaji wa Utamaduni wa Jamii

Senkoro (1976:74) anasema kuwa utamaduni ni njia zinazoundwa na wanajamii za kuishi na huundwa katika kutangamana kwa wanajamii na mazingira yao. Senkoro (khj) anaeleza kuwa utamaduni si tu ngoma wanazozicheza wanajamii na mila zao tu bali hujumlisha imani zao, njia za uzalishaji mali, sayansi, dini, mahusiano ya kijamii na masuala yote katika jamii husika. Kila jamii huwa na utamaduni wake mahususi na unaofuata muundo wa jamii hiyo husika.

Jagina huwa na nafasi kubwa, uwezo na wakati mrefu katika jamii na katika kipindi anamoishi. Jamii humtegemea katika kila jambo na hali na hivyo huwa ana nafasi kubwa ya kuibadilisha jamii vile apendavyo na hivyo kuwa wa muhimu katika kuukuza utamaduni wa jamii yake. Nabii Isa aliyabadilisha mengi katika jamii yake na kuubadili mkondo wa utamaduni wa Wayahudi. Sundiata aliikomboa jamii yake kutoka mikononi mwa mfalme Soumaoro Kante wa nchi ya Sosso na kubadilisha vipengele vingi vya utamaduni wa Wamali. Nabii Isa na Sundiata walizifanya tamaduni za jamii zao imara zaidi kwa kukuza tamaduni zilizoiweka mifumo ya jamii zao kwenye mfumo mmoja imara. Hata leo jamii yoyote hutambulikana kwa utamaduni wake imara.

**4.2 Hitimisho**

Katika sura zilizotangulia, tumetoa maelezo kuwa kazi nyingi zinazohusu ushujaa huwajenga mashujaa wake kwa kuwafungamanisha na misukosuko inayozikumba jamii zao. Hili huonyesha kuwa jagina ni zao la jamii na hivyo atakabiliana na hali zote ngumu katika jamii yake kama tu wanajamii wengine katika jamii ile. Kazi hizi zinazowahusu mashujaa vilevile huusawiri ushujaa wa shujaa katika kukabiliana na matatizo yanayoikumba jamii na hivyo kumtofautisha na wanajamii wengine. Fauka ya hayo, usawiri huu wa jagina huwaondolea hofu wanajamii kwani panakuwepo uhakikisho kuwa wako salama kwani jagina ana uwezo mkubwa wa kuwatetea wanapoandamwa na maadui wao.

Mchango wa jagina katika jamii haswa huwa ni kuleta mabadiliko kutokana na shida zinazoikumba jamii. Mfumo wa ujagina hufungamanishwa na mifumo mingineyo katika jamii kama vile uchumi, sheria, utawala dini, ndoa, kilimo miongoni mwa mingineyo ili kusawazisha hali katika jamii. Ujagina ni nguzo muhimu katika kuusawazisha mfumo wa jamii na usipokuwepo, jamii haiwezi kuwa imara.

Katika sura hii ya nne tumethibitisha umuhimu wa majagina Nabii Isa na Sundiata katika jamii zao. Kama tulivyotangulia kuona, ujagina ni nguzo muhimu katika kusawazisha hali katika jamii na pasipokuwepo na ushujaa, jamii haiwezi kuwa imara. Tumejaribu kuuchambua ujagina wao kama unavyojitokeza katika Utenzi wa Nabii Isa na Riwaya ya Sundiata. Mchango wa jagina katika jamii yoyote ile huwa ni kuleta mabadiliko katika kuzitatua shida zinazoikumba jamii.

Umuhimu wa majagina Nabii Isa na Sundiata ni kama vile kioo cha jamii, kitambulisho cha jamii, mabadiliko katika mfumo wa jamii, ukombozi na muungano wa jamii, fahari ya jamii, mfano bora wa kufuatwa na jamii na ukuzaji wa utamaduni wa jamii. Ujagina wa Nabii Isa na Sundiata umefungamanishwa na mifumo mingineyo katika jamii zao kama vile uchumi, sheria, utawala, dini, ndoa, kilimo miongoni mwa mingine ili kusawazisha hali katika jamii zao.

# SURA YA TANO

# HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 5.0 Utangulizi

Utafiti wetu ulikuwa na malengo kadhaa ambayo tulikusudia kuyatekeleza. Katika sura hii, tunaangazia matokeo ya utafiti wetu kwa jumla. Tunayarejelea malengo tuliotarajia kuyatekeleza huku tukiyafungamanisha na matokeo ya utafiti wetu. Vilevile tunayaangazia masuala mengine ambayo yalijitokeza katika mchakato mzima wa utafiti wetu.

Suala la mashujaa ni pana mno na huhitaji uelewa mzuri wa mazingira yaliyowazaa mashujaa hawa, historia yao na falsafa zao za maisha kwa jumla. Mada ya ushujaa ni mada yenye mvuto sana hususan inapoangaliwa kwa mkabala wa kiulinganishi. Mashujaa wa aina yoyote ile huwa na mchango mkubwa katika jamii zao na jamii pana kwa jumla. Ushujaa ni mojawapo ya asasi zenye mchango mkubwa katika jamii. Mashujaa wa kidini, kihistoria na vilevile kiutamaduni hivyo wana mchango wao mkubwa katika kuwepo kwa hali mbalimbali katika jamii za leo na hivyo basi wanapaswa kutazamwa kwa makini na kwa jicho pevu ili mchango wao ueleweke vyema na vizazi baada ya vizazi katika jamii husika.

## 5.1 Muhtasari

Katika utafiti huu wetu, tuliangazia masuala kadhaa ambayo yalitusaidia sana katika kutoa taswira bayana ya majagina katika jamii. Sura ya kwanza imechukua nafasi ya mambo au masuala muhimu ya jumla ambayo yalikuwa ya kutuongoza katika mchakato mzima wa utafiti wetu ili tuafikie malengo ya utafiti wenyewe. Katika sura ya pili, tuliangazia historia ya Nabii Isa pamoja na ile ya Sundiata huku tukiangazia historia za jamii zilizowazaa. Katika sura hii tumeonyesha mazingira, hali na vipindi walimoishi katika jamii zao. Baada ya uchunguzi wa historia zao na ile ya jamii zao tulipata kuwa majagina hawa walizuka kutokana na mahitaji fulani katika jamii zao. Katika kuiangazia historia ya jamii zao, ni dhahiri kuwa katika kila kipindi maalumu kulikuwepo na majagina wa nyakati hizo na walizuka wakati au vipindi maalumu kutokana na hitaji fulani katika jamii yao. Majagina Nabii Isa na Sundiata walizuka wakati na vipindi maalumu ambapo palikuwepo na misukosuko katika jamii zao na kwamba walizuka ili kuitatua.

Katika sura ya tatu, tulizitalii na kuziangazia sifa za majagina Nabii Isa na Sundiata kiulinganishi. Katika ulinganishi wetu, tulipata kuwa sifa za Nabii Isa na Sundiata zinalingana pakubwa. Kunao mfanano mkubwa wa sifa zao. Ingawa kuna tofauti, ni chache na finyu mno ambazo ni pamoja na suala la ulemavu na ndoa. Kutokana na matokeo ya utafiti wetu, tumetoa mchango kuchangia kuwa sifa za majagina kote ulimwenguni ni karibu sawa. Sifa ya kipekee katika utafiti huu wetu ni kuwa jagina anaweza kuwa na ulemavu ambao ni ishara ya onyo kuwa jagina huyu atakuwa hatari baadaye na hivyo kuashiria kuwa ulemavu husitiri nguvu za kipekee.

Kunao wasomi ambao hudai kuwa kila jagina kote duniani huwa na ulemavu ambao mara nyingi hauonekani kwa macho ya kawaida na pale ambako huonekana, jamii hujaribu kuupuuza kwa sababu ya ile dhana ya kumkuza jagina wao. Katika kazi yake Matugu (2019), alipokuwa akiangazia taswira ya ulemavu katika kazi zake Said Ahmed Mohammed na Euphrase Kezilahabi anasema kwamba, taswira za ulemavu huwa na lengo la kuwasilisha jumbe ambazo huwa na uzito kwa hadhira. Anaendelea kusema kuwa ulemavu hutumiwa kwa lengo mahususi ambalo ni kuwasilisha maudhui fulani kwa njia ya kipekee. Maudhui haya aghalabu huwa kuhusu maswala ambayo hayajitokezi waziwazi kwa hadhira.

Nabii Isa na Sundiata wana sifa za kijagina zilizo na ukaribu mwingi sana. Kunazo sifa za kiuhalisi ajabu ambazo ziliwapa kukuzwa na wanajamii wao. Kwa kawaida, kila jamii humkuza jagina wake wapendavyo. Kunao wanaopiga chuku sifa za jagina wao na kunao wanaozipuuza. Wanaozipuuza sifa za jagina wao huwa ni maadui wa jagina huyo. Kuzaliwa kwa Nabii Isa na Maryam aliyekuwa mwanajamii wa kawaida tu huwafanya baadhi ya wanajamii kupuuza iwapo alikuwa mwana wa Mungu. Kama tulivyosema hapo juu kuwa jamii humsawiri jagina wao jinsi wapendavyo na hivyo yeyote anayekuzwa na jamii na kujikuza yeye mwenyewe na kuikomboa jamii kutokana na dhiki zao basi huwa jagina.

Katika sura ya nne tumeangazia umuhimu wa jagina katika jamii yake. Tumepata kuwa jagina huzuka ili kutekeleza jukumu fulani katika jamii yake. Umuhimu wa jagina hujitokeza pale hukamilisha kazi yake ya ukombozi na mara nyingi hujitokeza baada ya mauko yake. Sifa moja ya jagina ni kuwa yeye huwa 'hafi' kwani hata baada ya kifo chake jamii huamini bado yu miongoni mwao akiwatazama wanajamii na matendo yao.

**5.3 Hitimisho**

Kutokana na matokeo ya utafiti wetu, taswira ya jagina imedhihirika katika maisha ya Nabii Isa na Sundiata. Imedhihirika bayana kuwa Nabii Isa na Sundiata ni mifano mizuri ya majagina wa kidini na kiutamaduni. Utafiti umedhihirisha kuwa majagina Nabii Isa na Sundiata wana nafasi ambayo ni muhimu katika historia ya dunia. Aidha utafiti wetu umetuwezesha kupata matokeo kuwa sifa za mashujaa huwa zimefanana kwa kiasi kikubwa. Vilevile, utafiti huu umedhihirisha kuwa majagina wana umuhimu mkubwa katika jamii zao na haswa mfumo wa jamii hauwezi kukamilika pasipokuwa na taasisi ya ushujaa.

Matokeo ya utafiti wetu vilevile yamelingana na maswali yetu ya utafiti wetu. Mazingira ya kijamii yaliyowazaa Nabii Isa na Sundiata ni mazingira yaliyokuwa na misukosuko mingi ya kijamii; jamii ya Wayahudi na jamii ya Wamali. Majagina Nabii Isa na Sundiata wana sifa za kijagina zilizolingana na vilevile sifa zilizotofautiana. Sifa za kijagina zilizofanana ni kama vile: utabiri wa kuzaliwa kwao, kufanya miujiza, kuwa na vifuasi, kutokana na ukoo wa kifalme, majina ya kimajazi, walikuwa wanaume, walikuwa na mahasidi, wenye akili pevu, waligura kwao, maisha yenye dhiki tupu, kutoeleweka kwa uwazi, majagina wa jamii nyingi na kusalitiwa kwa jagina.

Ingawa utafiti wetu umeonyesha mfanano mkubwa wa sifa za kijagina za Nabii Isa na Sundiata, kunazo tofauti chache za sifa za kijagina nazo ni: swala la ndoa. Sundiata alioa na kupata watoto, Nabii Isa hakuoa. Kurudi kwa jagina katika safari ya mwisho. Nabii Isa anatarajiwa kurudi tena ulimwenguni ili kukamilisha kazi yake. Hatujapata maandishi yanayodokezea kuhusu kurudi kwa jagina Sundiata mara ya pili ingawa jamii nyingi huamini kuwa majagina wao hawafi. Kimo na nguvu za jagina; Nabii Isa alikuwa na kimo cha wastani ilhali Sundiata alikuwa na kimo kifupi. Sundiata alikuwa na nguvu za mwili naye Nabii Isa alikuwa na nguvu za kiroho.

Kunazo kazi tulizozirejelea katika kuzipambanua sifa za kijagina za Nabii Isa nazo ni pamoja na; Utenzi wa Nabii Isa, Qurani,Bibilia pamoja na nyimbo na hadithi zinazomhusu Nabii Isa. Tumeitalii mitandao pia ili kuwelewa zaidi Nabii Isa. Kwa upande wa Sundiata, tulikirejelea kisa cha Sundiata kilichoandikwa na Niane Djiril Tamsir (1960). Kunavyo visa vingi vilivyoandikwa na wandishi wengi kumhusu sundiata ambavyo pia tumeviangalia na kuvirejelea. Vitabu kuhusu

historia ya Afrika Magharibi pia vimekuwa vya msaada katika huielewa historia ya jamii iliyomzaa Sundiata.

Katika kuwalinganisha mashujaa hawa wawili, wa kidini na wa kiutamaduni, hatukuwa na nia yoyote ya kuipigia debe au kuidhalilisha dini yoyote au imani ya watu wa jamii fulani au mtu binafsi. Tulikuwa na nia ya kuzichanganua sifa za majagina ambazo ni bia na hudhihirika kote ulimwenguni na katika aina zote za majagina. Hakuna utafiti wowote tulioupata uliomlinganisha Nabii Isa kama jagina wa kidini na Sundiata kama jagina wa kiutamaduni na umuhimu wao katika jamii zao. Ni matumaini yetu kuwa pengo lililokuwepo la kiusomi limezibwa na utafiti huu.

**5.3 Mapendekezo ya Utafiti**

Utafiti wetu umewalinganisha majagina wawili. Mmoja wa kidini ambaye ni Nabii Isa na mwingine wa kiutamaduni ambaye ni Sundiata. Majagina hawa waliishi vipindi viwili tofauti na walikuwa wametoka mazingira mawili tofauti. Sifa za majagina hawa pamoja na za majagina walioangaziwa awali kama vile Fumo Liyongo, Buddha, mtume Muhammad, Shaka Zulu, Luanda Magere miongoni mwa wengine ni bia.

Tumeona kuwa majagina huzuka katika kipindi na hali fulani mahususi ili kutatua shida fulani katika jamii zao wakati huo. Je, huwa jamii za leo zinakumbwa na misukosuko? Na je, majagina huzuka na hutatua aje matatizo hayo? Tungependekeza utafiti zaidi ufanywe haswa wa majagina wa hatamu hii ambapo nchi nyingi zimejipatia uhuru na ambayo ina mabadiliko mengi ya kiuchumi na kiteknolojia.

Jamii za Afrika zinao majagina wengi ambao hawajafanyiwa utafiti wa kutosha. Mashujaa wa Bara la Afrika walichangia pakubwa katika kulikomboa kutoka mikononi mwa wakoloni na hivyo walikuwa na umuhimu mkubwa kwa jamii zao. Majagina hawa wanapaswa kufanyiwa utafiti na mchango wao kuwekwa wazi kwa vizazi vijavyo. Majagina hawa ni kama vile Wangari Mathai, Nelson Mandela, Kwame Nkrumah, Jomo Kenyatta, Patrice Lumumba, Steve Biko, Mahatma Gandhi, Mansa Musa miongoni mwa wengine. Utafiti wa kutosha kuwahusu mashujaa tuliowataja hapo juu haujafanywa na iwapo utafanywa zaidi, utaliziba pengo kubwa la kiusomi ambalo linastahili kujazwa.

## MAREJELEO


Abed A.K (1954) *Sheria za Kutunga Mashairi*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Abrahams, M. H. & Harpham, G. G. (1981) A Glossary of Literature. New York: Half, Rinehart and Winston.

(1993) *A Glossary of Literary terms.* 6th Edition. New York: Hartcourt & Brace.

(1999) *A Glossary of Literary Terms*. 7th Edition, New York: Heile & Heile.

Achieng, O. B. (2012) "Sifa za Mashujaa na Umuhimu wao Kwa Jamii zao: Ulinganifu wa Fumo Liyongo na Lwanda Magere" Tasnifu ya uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi.

Burton, W. (1968) *Systems, States, Diplomacy and Rules,* London and New York: Cambridge University Press.

Butler, O (1979) *Kindred*, Boston: Beacon Press.

Campell, J. (1991) *The masks of god: Primitive mythology.* New York, NY: Penguin Compass.

Grenville, F. (1962) *The East African Coast: Select Documents from the First to the Earlier Nineteeth Century*, London, Oxford University Press.

Frazer, J. G. (1890) *The Golden Bough: A Study in Comparative Religion,* Volume 2 (Vol. 2). Macmillan.

Frye N. & Denham (1990) *The Grand Vision of a Liberal-Arts Education*. London: Palgrave Macmillan.

Gathara, F. K. (2015) "Taswira ya Jagina katika Tendi: Ulinganishi wa Fumo Liyongo na Nabii Isa" Chuo Kikuu cha Nairobi. https//erepository.uonbi.ac.ke

Gibbe, G. A (1980) *Shaaban Robert: Mshairi. Dar es Salaam*: Tanzania Publishing House.

Gichamba, J.M (2005) "Sifa za mashujaa na umuhimu wao kwa jamii zao: Ulinganishi wa Fumo Liyongo na Shaka Zulu" Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu Cha Nairobi.

Jung, C. N.W (1969) *The archetypes & Collective unconsciou, translated by R. F. C. Hull* (2nd Edition) Princeton, NJ: Princeton University Press.

Jung, C. G. (1990) *The basic writings of CG Jung*. Bollingen Series (General).

Jung, C. G (2001) *Modern Man in search of Soul.* Bollingen Series (general)

Jung, C. & Kerényi, K. (1972) *The trickster: A study in American Indian mythology* (Vol. 351). Schocken.

Jung, C. (1959) *Basic Writings*: New York, Modern Library.

Kalinjuma, D. (2013) "Jaala ya Shujaa wa Tendi za Kiafrika na Ulaya" Dar es Salaam: Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Kunene, D. P. (1972) *Heroic poetry of Basotho*. Oxford: Clarendon Press. Google Scholar.

Landman, J. (2006) *The Trend of a White Man's Foot: Australian Pacific Colonialism and the Cinema*, 1925-62, Pandanus, Canberra.

Mberia, K. (1989) Fumo Liyongo: *Mulika*, Jarida la Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar-es-Salaam. (21) 25-43.

Miehe N.W. (2004) *Liongo Songs: Poems Attributed To Fumo Liyongo*. Koln: Grudiger Koppe Verlag.

Mulokozi, M.M (1996) *Fasihi ya Kiswahili,* Dar es Salaam: Open University of Tanzania.

Mulokozi, M.M. (1999) *Tenzi Tatu za Kale. Dar es salaam:* Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.

Mushi, S. (1971) *Mfalme Edipode*. Nairobi, Oxford University Press.

Musyimi M.D. (2011) "Maana ya Majina ya Watu katika Jamii ya Wakamba" Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Kenyatta. Haijachapishwa.

WaMutiso, K. (1985) "Hurafa na uyakinifu katika Hamziyyah" Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi. Haijachapishwa.

______ (1990) "Fumo Liyongo na kazi zake" Haijachapishwa.

______ (1999) "Sira ya Majagina Buddha na Muhammed" Swahili Kolloquim Universitat, Bayreuth. Mei 14-15. Haijachapishwa.

Mzenga, M. (1977) *Utenzi wa Nabii Isa*. Nairobi: Fountain Books Ltd.

Ndumbaro, E (2013) "Shujaa wa Tendi na Matatizo ya Kijamii" Dar es Salaam: Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Niane, D. T. (1960) *An Epic of Old Mali*, United Kingdom, Longman African Writers.

Nietzsche N.W (1961: 49-111) *Subjectified Culture and the End of History.* Chicago: University of Chicago Press.

Njogu, K na Chimera, R (1999) *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Njogu, K na Wafula, R (2007) *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Onchwati, J. S. (2016) "Uhalisiajabu unavyojitokeza katika Ukawafi wa Miiraji na Utenzi wa Fumo Liyongo" Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi.

Owallah, K. O. (2013) "Uhakiki wa Maudhui Teule katika Utenzi wa Nabii Isa" Tasnifu ya uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi.

Muhammad, T. (1999) *The Noble Qur'an; Interpretation of Meanings of the Noble Qur'an in the English Language.* India. Dar-es-Salam Publications.

Sengo, T. (2009) *Fasihi za Kinchi, Dar es Salaam*: AERA Kiswahili Researched Products.

Al-farsy, A. (1984). *Qurani Takatifu.* Nairobi: The Islamic Foundation Publication. Chapa ya nne.

Sugg, R. P. (1992) *Jungian Literary Criticism*. Evanston, Northwestern University Press.

United Bible Societies (1952) *Bibilia.* Nairobi: Scripture Union.98

Wamitila, K.W. (2002) *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele Vyake.* Nairobi: Phoenix Publishers.

Wamitila, K. W. (2003). *Kichocheo cha Fasihi Simulizi na Andishi*. Nairobi. Focus Publications.

Werner, A. (1932) *Hadithi ya Mikidad na Mayasa,* Amedstead Hemshire: The Azania Press

Werner, A. (1968) *Myths and Legends of the Bantu* (Vol. 65). Psychology Press.